# RIPOTI YA MAPENDEKEZO YA WANANCHI JUU YA UTATUZI WA MGOGORO WA ARDHI

## TARAFA ZA LOLIONDO NA SALE WILAYA YA NGORONGORO ARUSHA



# RIPOTI YA MAPENDEKEZO YA WANANCHI JUU YA UTATUZI WA MGOGORO WA ARDHI TARAFA ZA LOLIONDO NA SALE WILAYA YA NGORONGORO ARUSHA

MEI, 2022

# YALIYOMO


VIFUPISHO Vii
SHUKRANI Viii
TAARIFA KWA UFUPI iX


## SURA YA KWANZA
## TAARIFA ZA AWALI

1.0 UTANGULIZI 1
1.1. Mahali ilipo Wilaya ya Ngorongoro 1
1.2 Ukubwa wa Tarafa ya Sale na Loliondo 2
1.3 Idadi ya Mifugo 5
1.4 Malengo ya Taarifa 6
1.5 Muundo wa Taarifa 6
1.6 Mchakato wa Upatikanaji Wa Taarifa 7
1.8 Vikwazo Katika Ukusanyaji wa Taarifa 11

## SURA YA PILI
## HADHI YA ARDHI YA VIJIJI VYA TARAFA ZA SALE NA LOLIONDO KISHERIA

**2.0 UTANGULIZI** **14**

2.1 Historia ya Utawala na Usimamizi wa Ardhi 14
2.1.1 Utawala wa Ardhi kabla ya Wakoloni 14
2.1.2 Usimamizi wa Ardhi wakati wa Utawala wa Wajerumani 1886-1918 15
2.1.3 Usimamizi wa Ardhi wakati wa Utawala wa Waingereza 1919-1961 15
2.1.4 Utawala na Usimamizi wa Ardhi baada ya Uhuru 1961-1989 17
2.1.5 Uanzishwaji wa Wilaya Ngorongoro na Usajili wa Vijiji 19
2.1.6 Utawala na Usimamizi wa Ardhi Kuanzia Mwaka 1990- 2022 19
2.1.6.1 Upimaji wa Vijiji na Kupata Hati/Vyeti vya kumiliki Ardhi 20
2.1.6.2 Tume ya Rais ya Uchunguzi wa Masuala ya Ardhi -1991 20
2.1.6.3 Sera ya Taifa ya Ardhi na Sheria za ardhi za 1999 21

2.1.6.4 Hadhi/Uhalali wa Hati za Ardhi za Vijiji kisheria 24
2.1.5.5 Sheria Ndogo za Vijiji 25

2.2 Historia ya Sheria za Wanyamapori 27
2.2.1 Sheria za Uhifadhi Baada ya Uhuru 28
2.2.2.2 Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009 29

2.3 Mifumo Ya Kimila Na Desturi Za Kimaasai Katika Usimamizi Wa Ardhi Na Maliasili 31
2.3.1 Mahusiano ya Mila za kimaasai na Wanyamapori 31

**SURA YA TATU**

**HISTORIA NA JITIHADA ZA UTATUZI WA MGOGORO WA ARDHI TARAFA ZA LOLIONDO NA SALE**

**3.0 UTANGULIZI** **34**
3.1 Historia na Chanzo cha Mgogoro wa Ardhi Tarafa ya Loliondo na Sale 34
3.2 Jitihada za Kutatua Mgogoro wa Ardhi ya Loliondo 52
3.3 Madhara Yatokanayo na Jitihada za Kuchukua Ardhi ya Vijiji (sq km 1500) kwa Jamii 55
3.4 Mgogoro Wa Vijiji Na Kampuni Ya Thompson Safari /Tcl 63

**SURA YA NNE**

**UCHAMBUZI WA HOJA ZA SERIKALI**

**4.0 UTANGULIZI** **64**
4.1 Hoja ya Ushoroba 64
4.2 Hoja ya Mazalia ya Wanyama 65
4.3 Hoja ya Eneo la 1500 kuwa ni Eneo la wazi na si Ardhi ya Vijiji 66
4.4 Hoja ya Kulinda vya Vyanzo vya Maji 69
4.5 Hoja ya Uharibifu wa Mazingira 71
4.6 Hoja ya Uwekezaji/Uwindaji na Utalii 73

**SURA YA TANO**

**MAPENDEKEZO YA JUMLA NA HITIMISHO**

**5.0MAPENDEKEZO YA WANANCHI** **76**
5.1 HITIMISHO 78
6. MAREJEO 79
7. VIAMBATANISHI 84



1. Hati Za Usajili Wa Vijiji 84
2. Vyeti Vya Ardhi 86
3. Hati Ya Kumiliki Ardhi Ya Kijiji 89
4. Sheria Ndogo Za Vijiji 95
5. Kamati Ya Viongozi Na Wataalamu Juu Ya Mgogoro Wa Ardhi Tarafa Ya Sale Na Loliondo 100

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1.1: Mgawanyo wa ardhi kwa kila tarafa katika Wilaya ya Ngorongoro 2
Jedwali 1.2:Orodha ya mikutano ya ukusanyaji wa tarafa ya Loliondo na Sale 9
Jedwali 1.3: Baadhi ya Viongozi wa kisiasa, wa kimila na watetezi wa haki za binadamu walioendelea kukamatwa, kuitwa vituo vya polisi na kuhojiwa wakati wa zoezi la kukusanya maoni ya wananchi (Machi-Aprili 2022). 12
Jedwali 2.1: Baadhi ya Vijiji Vilivyo Sajiliwa mwaka 1978 katika Tarafa za Loliondo na Sale 19
Jedwali 2.2:Vijiji vilipimwa na kuwa Hati Miliki za Ardhi 20
Jedwali 2.3:Mahusiano baina ya koo za Wamaasai na Wanyama pori 32
Jedwali 3.1:Mchakato wa kuchukuliwa Maeneo ya Wamasai Serengeti 35
Jedwali 3.2:Matukio ya majaribio ya kutaka kuchukua ardhi ya Vijiji 46
Jedwali 3.3:Idadi ya wananchi wa Loliondo waliokamatwa na kuteswa J ulai na Novemba 2017. 55
Jedwali 3.4:Idadi ya mifugo iliyokamatwa, kupigwa fini, kutaifishwa na kupigwa risasi 62
Jedwali 3.5:Baadhi ya Kampuni zilizoondoka kutokana na mgogoro wa OBC 63
Jedwali 4.1: Uwepo wa wawekezaji tofauti katika Tarafa za Loliondo na Sale 73

## ORODHA YA RAMANI

Ramani 1.1:Ramani ya Wilaya ya Ngorongoro 1
Ramani 1.2: Ramani ya Tarafa za Sale na Loliondo 3
Ramani 2.1:Matumizi ya Ardhi Kabla ya Mwaka 1958 16
Ramani 2.2: Matumizi ya Ardhi Baada ya 1958 17
Ramani 2.3: Matumizi ya sasa ya ardhi katika tarafa za Loliondo na Sale 22

Ramani 2.4:Ramani ya matumizi ya ardhi ya Kijiji cha Engaresero 2016-2026Chanzo: Kijiji cha Engaresero, 2016 **23**

Ramani 2.5: Ramani ya matumizi ya Ardhi ya Kijiji cha Ololosokwan 2008Chanzo: Kijiji cha Ololosokwan, 2008 **24**

Ramani 2.6:Usimamizi wa nyanda za malisho kijiji cha Ololosokwan kwa kutumia sheria Ndogo za Kijiji za 2000, kwa nyakati za kiangazi na masika **26**

Ramani 3.1:Ramani ya Tarafa za Loliondo na sale ikionyesha Vijiji vyenye Migogoro **38**

Ramani 3.2: Ramani ya mapendekezo ya matumizi Bora ya Ardhi ya Wilaya ya Ngorongoro 2010 kama ilivyondaliwa na Tume ya Mipango na Matumizi Bora ya Ardhi na Halmshauri ya Wilaya Ngorongoro **45**

Ramani 3.3:Ramani ya mapendekezo ya Kamati ya Ardhi Mseto Ngorongoro ikionyesha ardhi ya Vijiji vya Tarafa za Loliondo na Sale zliztopendekezwa kumegwa na kuwekwa chini ya NCA. **51**

Ramani 3.4:Ramani ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya iliyo kuwa iliyopendekezwa ikionyesha matumizi Kwa kanda ikiwemo eneo la Vijiji vya Loliondo vyenye Kilomita za mraba 1500. **52**

Ramani 4.1: Ramani inayoonyesha mito katika tarafa za Loliondo na Sale **70**

Ramani 4.2:Ramani inayoonyesha uoto wa asili katika Tarafa za Sale na Loliondo kwa nyakati tofauti **72**

## ORODHA YA GRAFU

Grafu 1. 1:Mgawanyo wa Ardhi katika Tarafa za Loliondo, Sale and Ngorongoro **2**

Grafu 1.2: Idadi ya Watu Katika Wilaya ya Ngorongoro **4**

Grafu 1.3: Idadi ya watu katika Tarafa ya Loliondo na Kata za Malambo na Piyaya tarafa ya Sale **4**

Grafu 1.4:Idadi ya watu kijinsia - Tarafa ya Loliondo na Sale **5**

Grafu 1.5:Idadi ya mifugo katika kata Nane za Tarafa ya Loliondo na Sale **5**

## ORODHA YA PICHA

Picha 1.1 Sehemu ya Wajumbe wa Kamati ya Wananchi kutoka Tarafa za Loliondo na Sale wakiwa katika Mapitio ya rasimu ya Kwanza ya Taarifa. **7**

Picha 1.2: Sehemu ya Wananchi kutoka tarafa ya Loliondo na Sale katika Kikao cha pamoja kujadili mgogoro wa Ardhi **8**

Picha 2.1: Lengo na Tamko la Saera ya Ardhi kuhusu Nyanda za Malisho kwa Wafugaji **21**
Picha 3.1: Mkataba wa Serikali na Mfalme wa Uarabuni (UAE) **41**
Picha 3.2: Majengo ya Kambi ya OBC katika eneo la Vijiji **42**
Picha 3.3: Ndege kubwa ya OBC ikipakua mizigo katika kiwanja chake cha ndege katika eneo la Lima Loliondo mwaka 2009. **43**
Picha 3.4: Picha kushoto alievaa suti ni Waziri wa Maliasili na Utalii (2017) Prof. Maghembe akiwa na waandishi wa habari Jackton Manyerere, na Matinyi, na Picha ya kulia ni Waziri wa Maliasili na Utalii (2014-2015) Ndg Lazaro Nyalandu na akimpokea Sheikh Mohamme **44**
Picha 3.5:Kielelezo cha barua ya Waziri Mkuu Mh. Pinda Juu ya msimamo wa Serikali kwa swala la Mgogoro wa Tarafa za Loliondo na sale tarehe 30/5/2013 **53**
Picha 3.6:Makazi ya wafugaji wa Loliondo yaliyochomwa moto wakati wa operesheni **56**
Picha 3.7:Parmoson Ololoso ( kushoto): wa Kijiji cha Olosokwan aliyepigwa risasi katika operesheni ya 2017 na maaskari waliokuwa wanafanya operesheni pamoja Ngoididio Rotiken (kulia) alipigwa risasi ya jicho na kikosi maalum cha polisi mwaka 2009 **57**
Picha 3.8:Mawakili wakiandamana baada ya wakili mwezao kukamatwa Loliondo akiwa katika majukumu yake ya uwakili (Wakili Shilinde Ngalula wa LHRC, akiwa anawatetea watu waliokamatwa Mahakama ya Wilaya, Ngorongoro.) **58**
Picha 3.9:Jeshi la polisi lilipokuwa linadhibiti maandamano ya wananchi baada ya maakazi yao kuchomwa moto **59**
Picha 3.10:Kichwa cha Habari cha Gazeti la Jamhuri la mwaka 2014 **60**
Picha 3.11:Makazi ya wenyeji wa Loliondo yakiungua moto na wenyeji wakijaribu kuokoa baadhi ya mali. **61**
Picha 3.12:Baadhi ya picha za mikutano ya wananchi wakipinga ardhi ya Vijiji vyao kumegwa kwa maslahi ya Kampuni ya OBC. **62**

**ORODHA YA VIELELEZO**

Kielelezo 3.1: Makubaliano ya MORU baina ya Viongozi wa mila (Malaigwanani) wa kimaasai 12 wa Loliondo na Ngorongoro na wakoloni 21st April, 1958 **36**

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ADDO** | Arusha Diocesan Development Office |
| **CCM** | Chama Cha Mapinduzi |
| **FEM-ACT** | Feminist Activist Coalition |
| **FZS** | FrankFurt Zoological Society |
| **GN** | Government Notice |
| **KIPOC** | Korongoro Integrated People's Oriented to Conservation |
| **KM** | Kilomita |
| **LGCA** | Loliondo Game Controlled Area |
| **NCA** | Ngorongoro Conservation Area |
| **NDC** | Ngorongoro District Council |
| **NGO** | Non-governmental Organisation |
| **NGONET** | Ngorongoro NGOs Network |
| **NLUPC** | National Land Use Planning Commission |
| **OBC** | Ortello Business Corporation |
| **PINGOS -FORUM** | Pastoralist Indigenous Non-Governmental Organization |
| **PM** | Prime Minister |
| **PWC** | Pastoral Women Council |
| **SENEPA** | Serengeti National Park |
| **TANAPA** | Tanzania National Parks |
| **TAWICO** | Tanzania Wildlife Corporation |
| **TAWIRI** | Tanzania Wildlife Research Institute |
| **THBUB** | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora |
| **THRDC** | Tanzania Human Rights Defenders Coalition |
| **UCRT** | Ujamaa Community Resources Team |



# SHUKRANI

Sisi wananchi wa Vijiji vya Tarafa za Sale na Loliondo katika eneo lenye mgogoro wa ardhi, tunapenda kutumia nafasi hii kuwashukuru watu na makundi yote yaliyochangia kupatikana kwa taarifa hii. Kwanza kabisa tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa kamati yetu ya Tarafa ya Sale na Loliondo kwa kujitolea kuwa sehemu ya kufanikisha mchakato huu. Kamati hii inayoundwa na viongozi wa kjamii, wasomi wa kijamii, wazee wa kimila na wamama wa kijamii imefanya kazi kubwa kufikisha repoti hii hapa ilipofika. Kwa unyenyekevu kabisa tunapenda kuwapongeza wataalam wetu wa kijamii kwa kujitolewa kuandika repoti hii bila malipo yoyote kwa kuwa wametambua kuwa na wao ni sehemu ya jamii.

Wakati huo huo tunapenda kutambua uongozi mzuri wa Mbunge wetu wa Ngorongoro Mh Emmanuel Shangai, pamoja na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ngorongoro Mh. Ndirango Olesenge kwa uratibu wao katika mchakato huu. Tunapenda pia kutambua mchango wa mawazo na mali wa wananchi wetu ambao wamekuwa tayari mara zote kutoa maoni na hata kuchanga fedha za kuwezesha wajumbe wa kamati hii kufanya kazi vizuri. Pia kwa kipekee kabisa tunapenda kuzitambua na kuzishukuru asasi zetu za kijamii kwa kuwa na sisi bega kwa bega wakati wote wa mchakato huu na kuhakikisha azma njema hii ya kutatua mgogoro huu kwa majadiliano inafikiwa kwa haraka. Michango yao ya kitalaamu, hali na mali imechangia kufikia malengo ya kamati kwa kiasi kikubwa. Pia tunashukuru kwa viongozi wote wa serikali waliokuwa tayari kufanya kazi na kamati hii.



# TAARIFA KWA UFUPI

## UTANGULIZI

Wilaya ya Ngorongoro ni mojawapo ya Wilaya sita za Mkoa wa Arusha. Wilaya hii ilianzishwa mwaka 1979, kabla ya hapo ilikuwa ni sehemu ya Wilaya ya Maasai. Kiutawala inaundwa na Tarafu Tatu ambazo ni Ngorongoro, Sale na Loliondo. Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro yapo Mjini Loliondo-Wasso katika Tarafa ya Loliondo. Wilaya inapakana na Nchi jirani ya Kenya kwa upande wa Kaskazini, Wilaya ya Serengeti kwa upande wa Magharibi, Wilaya ya Meatu kwa upande wa Kusini magharibi, Wilaya za Monduli na Longido kwa upande wa Mashariki na Wilaya ya Karatu kwa upande wa Kusini. Inakadiriwa kuwa na umbali wa kilomia takriban 400 kutoka Arusha makao makuu ya Mkoa hadi Loliondo, makao makuu ya Wilaya.

Kwa takribani miongo mitatu (3) sasa Ardhi ya Vijiji katika Tarafa za Loliondo na Sale imekuwa ikizungumziwa katika taarifa mbalimbali za Serikali, Asasi za Kiraia, na Vyombo vya Habari maarufu kama Mgogoro wa Loliondo. Katika nyakati zote hizi za mgogoro serikali pamoja na wananchi waishio katika vijiji vinavyoathirika hawajawahi kupata suluhu ya mgogoro huo. Kwa awamu nyingine hasa mwishoni mwa mwaka 2021 hadi sasa (Mei 2022) mgogoro huu umeibuka tena na wananchi kupitia viongozi wao wa serikali, mila na kupitia Mh. Mbunge wa Wilaya ya Ngorongoro Mh. Emmanuel Ole Shangai wameendeleza majadiliano na Ofisi ya Waziri Mkuu ili kutafuta namna bora ya kufikia muafaka wa mgogoro huo. Matokeo ya majadiliano yalifikiwa kuwa wananchi kutoka tarafa za Loliondo na Sale kuunda kamati yao ili kuratibu maoni ya wananchi na kuwasilisha serikalini. Malengo ya taarifa hii ni pamoja na (a) kubainisha mifumo ya wafugaji wa asili juu ya milki, usimamizi na matumizi ya ardhi katika tarafa za Loliondo na Sale, (b) kubainisha chanzo na historia ya mgogoro wa Ardhi katika tarafa za Loliondo na Sale, (c) kutoa mapendekezo ya namna ya kusuluhisha mgogoro huu na kuelimisha umma wa watanzania, viongozi wa Serikali na wadau wa uhifadhi, ardhi na maendeleo ya jamii kuhusiana na mgogoro wa tarafa za Loliondo na Sale.

Taarifa hii imegawanyika katika sura kuu Tano, Sura ya Kwanza inatoa maelezo kwa ufupi juu ya Wilaya ya Ngorogoro mahali ilipo, idadi ya watu, ukubwa wa Wilaya. Sura hii pia inatoa taarifa za awali kuhusu eneo la Tarafa za Loliondo na Sale hasa mahali zilipo; idadi ya watu, mifugo na mfumo wa

matumizi ya ardhi katika eneo la kilomita za mraba 1500. Sehemu hii pia inabainisha malengo ya taarifa, mbinu na mchakato wote uliopitiwa katika kuandaa taarifa hii zimeainishwa katika sura hii. Sura ya Pili inazungumzia taarifa muhimu juu ya hadhi ya ardhi kisheria ya eneo la ardhi ya vijiji katika Tarafa za Loliondo na Sale na hasa eneo la kilometa za mraba 1500 lenye mgogoro kwa zaidi ya miaka 30 sasa. Sura hii pia inafafanua zaidi mabadiliko ya kisheria yaliyotokea wakati wa utawala wa Kikoloni, baada ya Uhuru hadi sasa na jinsi mabadiliko hayo yalivyochangia migogoro ya ardhi au kupunguza migogoro hiyo. Vile vile sura hii inafafanua sheria mbalimbali ikiwemo sheria za ardhi, Wanyamapori, sheria za serikali za mitaa, sheria ya mipango ya matumizi ya Ardhi, pamoja na matamko ya viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa na serikali kabla na baada ya Uhuru. Sehemu hii pia inaonyesha mfumo wa asili wa usimamizi wa ardhi katika tarafa hizi kwa taratibu za mila za jamii yenyewe.

Sura ya Tatu inaangazia kwa kina kupitia fafanuzi mbalimbali juu ya historia ya mgogoro, chanzo chake, madhara pamoja na jitihada zilizochukuliwa katika kutatua au kuendeleza mgogoro ndani ya tarafa za Loliondo na Sale. Sura ya Nne inaeleza na kuchambua kwa kina hoja ambazo zimekuwa zikiwasilishwa na upande wa Serikali kwa nyakati na awamu tofauti za uongozi wa nchi juu ya eneo la kilomita za mraba 1500 ambalo ni eneo la Vijiji vya Tarafa za Loliondo na Sale. Inabainisha pia uchambuzi na hoja za wananchi. Sura ya Tano inatoa mapendekezo na maoni ya jamii juu ya jinsi gani mgogoro huu unavyoweza kushughulikiwa ili kufikia maridhiano baina ya serikali na wanavijiji. Mwisho kabisa sura hii inatoa hitimisho ya taarifa kwa kurejea na kutoa mwelekeo wa msingi juu ya taarifa.

**Mchakato wa Upatikanaji wa Taarifa Hii**

Taarifa hii imetokana na mchakato na maamuzi ya wananchi kupitia viongozi wao wa kisiasa na kimila chini uratibu wa Mbunge wa Wilaya ya Ngorongoro kutafuta nia ya kuendeleza majadialiano na serikali na mamlaka zake za hifadhi ili kutafuta muafaka wa kutatua mgogoro huu uliodumu zaidi ya miongo mitatu (3). Na ili kuwezesha ukusanyaji na uandishi wa taarifa ya wananchi kupitia kamati yao, jamii ilichagua kamati maalum kutoka katika Kata 8. Kamati hii iliyochaguliwa na wananchi inaongozwa na Mh. Mbunge wa Wilaya Ngorongoro na Mwenyekiti wa CCM Wilaya kwa lengo la kuandaa mapendekezo ya utatuzi wa mgogoro huu wa ardhi katika eneo la Kilomita za mraba 1500. Kamati hii inaundwa na wajumbe 35 kutoka katika kata zote 8 wakiwemo Madiwani, viongozi wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Ngorongoro, wenyeviti wa vijiji, viongozi wa mila, wawakilishi wa Wanawake, vijana na wataalamu wa jamii kwa lengo la kuratibu na kuandika mapendekezo ya wananchi.

Ili kuhakikisha kuwa taarifa na maoni ya wananchi yanakusanywa kwa upana na undani wake, Kamati ilitumia mbinu mbalimbali zikiwemo; a) Mikutano ya wananchi katika ngazi za vijiji na Kata, b) Mikutano jumuishi za Kata mbalimbali, c) Mikutano ya Wadau , d) Mikutano ya makundi mbalimbali kama viongozi wa mila, wanawake, madiwani, e) Kupitia nyaraka mbalimbali za serikali kabla na baada ya Uhuru , f) Kupitia machapisho mbalimbali ya kitaaluma, na vyombo vya Habari kuhusiana na eneo lenye mgogoro, na g) Kutembelea eneo lenye mgogoro kuthibitisha aina ya matumizi na kuona hali halisi.  Orodha ya wanakamati wa Tarafa ya Sale na Liliondo ipo mwishoni mwa taarifa hii.

**Wilaya ya Ngorongoro na tarafa za Loliondo na Sale**

Wilaya ya Ngorongoro ina eneo la kilometa za mraba zipatazo 14,036 ambapo Tarafa ya Ngorongoro ina jumla za kilomita za mraba 8,100, Tarafa ya Sale ina jumla za Km za Mraba 3,518 na tarafa ya Loliondo ina ukubwa wa kilomita za mraba 2,218. Eneo hili lenye mgogoro lina jumla ya watu takriban 70,000 wanaojihusisha kwa sehemu kubwa na shughuli ya ufugaji wa asili kama chanzo kikuu cha uchumi na ambao huchangia zaidi ya asilimia 50 ya mapato yote ya ndani ya Halmashauri.

Tarafa ya Loliondo na Sale kwa ujumla zina eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 5,744 ambayo kwa wilaya ya Ngorongoro pekee ni sawa na asilimia 41 ya eneo lote la wilaya. Kati ya km za mraba 5,744 za Sale na Loliondo, km za mraba 4,000 ndio zilikuwa na pori tengefu kwa mujibu wa sheria kabla ya mabadiliko ya 2009 ambayo ilifuta mapori tengefu ndani ya ardhi ya vijiji. Kati ya eneo lote la kilomita za mraba 5,744 eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,744 linajumuisha eneo lote la tarafa ya Sale isipokuwa kata za Malambo na Piyaya ambazo ni sehemu ya eneo la kilomita za mraba 4000 zinazojumuisha eneo lote la tarafa ya Loliondo. Eneo hili la kilomita za mraba 4000 ni eneo la ardhi ya vijiji na mji mdogo wa Loliondo na maeneo ya Sale.

Eneo lenye kilomita za mraba 1,500 ndani ya km za mraba 4000 ndio limekuwa na mgogoro wa ardhi kwa muda mrefu ikijumuisha kata mbili (2) za Malambo na Piyaya vya tarafa ya Sale, na kata sita (6) za tarafa ya Loliondo kata za Arash, Oloipiri, Maaloni, Oloirien, Soitsambu na Ololosokwan zenye jumla ya vijiji 23.

## HADHI YA ENEO LENYE MGOGORO KISHERIA

Matokeo ya majadiliano na jamii wakati wa ukusanyaji wa taarifa na nyaraka mbalimbali yanaonyesha kuwa kabla ya ujio wa wakoloni wa Kijerumani na badae Waingereza jamii ya kimasai ilikuwa inamiliki na kutumia ardhi

hii kwa taratibu za kimila chini ya usimamizi na uangalizi wa viongozi wa mila kwa niaba ya jamii. Ujio wa wakoloni ulileta utaratibu mwingine ambao ulikuwa chini ya sheria za kikoloni hasa wakati wa Wajerumani na baadae Waingereza walipokuja na sheria ya Ardhi namba 3 ya mwaka 1923 na kufuatiwa na sheria zingine ikiwemo za Uhifadhi wa Wanyama pori. Umiliki wa ardhi kimila ulitambuliwa pia na Sheria ya Ardhi ya 1923 na iliyofanyiwa marekebisho1928, ili kutambua zaidi haki za wenyeji.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya mwaka 1923 katika kifungu cha 9, ilitoa mamlaka kwa Mkurugenzi wa Huduma za Maendeleo ya Ardhi kutoa hati za kumiliki ardhi za Vijiji. Baada ya mabadiliko ya sheria za Ardhi za Tanzania hasa mwaka 1999, Sheria Mpya ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya mwaka 1999 illibainisha kuwa, kutakuwa na Vyeti vya ardhi vya Vijiji tofauti na hati za kumiliki ardhi zilizotolewa kwa Vijiji kwa mujibu wa Sheria ya ardhi ya mwaka 1923.Vilevile Sheria hizo mpya za ardhi zimeendelea kutambua hati hizo ambazo zilitolewa kwa Mujibu wa Sheria zaingine kabla ya kutungwa kwa Sheria hiyo.

Kipindi hiki itakumbukwa kutokana na jitihada za mageuzi makubwa ya upimaji wa Vijiji vya wafugaji katika Tarafa za Loliondo na Sale kwa kupitia viongozi wa Vijiji, Kata, Wilaya na mashirika ya kiraia ambapo vijiji mbalimbali vilipimwa na kupata Hati za kumiliki ardhi katika Vijiji vyao kama inavyoonekana katika Kiambatanisho namba 2. Mchakato wa upimaji na hatimaye kutolewa kwa hati za kumiliki ardhi hizi, ulisimamiwa na Halmashauri ya wilaya ya Ngorongoro kwa msaada wa mashirika ya KIPOC na ADDO. Jumla ya ardhi ya vijiji vyenye ukubwa wa Hekta 346,672 za tarafa ya Loliondo zilipimwa na kupatiwa hati za umiliki wa ardhi. Baadhi ya vijiji vilivyoweza kupata hati hizo ni pamoja na Arash, Loosoito/Maaloni, Olorien/ Magaidur, Oloipiri, Soitsambu na Ololosokwan, kwa mujibu wa sheria ya ardhi ya mwaka 1923. Jitihada zote hizi zinabainisha kuwa eneo la km za mraba 4000 za Loliondo na Sale ni ardhi halali za vijjiji zilizokuwa zinatumika pia kama pori tengefu.

Kifungu cha 7 (12) cha sheria ya Ardhi ya Vijiji inatambua hati zote za milki ya ardhi ya Vijiji vilivyotolewa kwa mujibu wa sheria zingine kabla ya kutungwa kwa sheria hiyo. Hivyo kwa mujibu wa sheria ya Ardhi ya Vijiji ya 1999, Vijiji vyote vya tarafa za Loliondo na Sale vilivyosajiliwa kwa Mujibu wa Sheria ya Serikali za mitaa [Mamlaka za wilaya] Na. 7 ya 1982 na kupata hati za kumiliki ardhi ni halali na vinaendelea kutambulika kisheria. Aidha ni dhahiri kuwa hatua ya Serikali ya kutaka kumega ardhi ya Vijiji kiasi cha kilomita za mraba 1,500 inavunja Ibara ya 24 ya katiba ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria za ardhi ambazo zinatoa haki ya msingi ya kumiliki mali ambapo ni pamoja na ardhi kama rasilimali kuu.

Pamoja na kutungwa kwa sheria mpya ya Ardhi, wakati huo wa utawala wa waingereza ni wakati huo pia zilitungwa sheria zinazo husiana na usimamizi, ulinzi wa wanayamapori na uhifadhi. Uwepo wa mapori ya wanyama katika eneo la Sale na Loliondo ulikuwa ni wa muda mrefu toka miaka ya wakoloni wa Kijerumani hadi wakoloni wa Kingereza. Ilipofika miaka ya 1930, Serikali ya kikoloni ya Waingereza waliona umuhimu wa kuanza kutunga sheria za kulinda maeneo ya wanyama pori hapa nchini na pia kuweka utaratibu wa kisheria wa kufanya shuguli za kiwindaji. Kwa miaka yote hiyo ya nyuma wakati wa ukoloni maeneo haya ya Loliondo na Sale yalikuwa katika maeneo ya wananchi yanayomilikiwa kisheria kama ilivyofafanuliwa hapo juu kwa lengo la kulinda na kuratibu shughuli za Wanyama pekee.

Himaya ya Wajerumani (German East Africa) ilianza kuweka mikakati ya kumiliki maeneo kuanzia mwaka 1885 hadi 19914 walipovamiwa na kuondolewa na Waingereza. Mfano mwanzoni mwa karne ya 20, Wajerumani walianzisha Sheria ya kusimamia Wanyamapori iitwayo Game Preservaion Ordinance ya mwaka 1908 hadi 1911.

Sheria mpya ya wanyamapori (New Game Ordinance ya 1948),ndiyo iliokuja na utaratibu wa kuanzisha Hifadhi ya Serengeti (Serengeti National Park). Hii ndiyo sheria ya kwanza iliyoanza kuleta maumivu makubwa hasa kwa ardhi za Wamasai waliokuwa wanaishi Serengeti, Ngorongoro na Loliondo. Mwaka 1959 Kutokana na sheria hii Wamasai wakaondolewa maeneo ya Serengeti ya Mwaka 1959 na kuamishiwa maeneo ya Ngorongoro na Loliondo na kuungana na ndugu zao wengine. Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ya 1959 ilitungwa na watawala kwa kikoloni ili kuhifadhi eneo la Ngorongoro na pia kuwalinda na kuwaendeleza jamii ya wamasai walikuwepo na waliohamishiwa eneo la Ngorongoro kupisha uanzishwaji wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Sheria ya Uhifadhi wa Wanyama Pori ya mwaka 1974, ilianzisha mapori tengefu ambapo Loliondo na Sale ilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 269 la 1974. Kabla ya sheria hii ya wanyamapori kutungwa baada ya uhuru, kulikuwa na sheria ya Ukoloni iliyoitwa Fauna Game Ordinance iliyoanzisha pori la akiba la Loliondo katika ardhi ya vijiji ambayo ilikuwa ikitumika kwa taratibu za mila na tamaduni zao kama ilivyokuwa nchi nzima kabla ya ukoloni ambapo haikuwa na madhara katika milki ya ardhi ya Vijiji kwa kuwa ilitumika kulinda na kuratibu shughuli za wanayamapori. Baada ya miaka kadhaa baadaye baada ya uhuru, mwaka 1974, Sheria hiyo ikafutwa baada ya kutungwa sheria mpya tajwa hapo juu ya wanayama pori. Sheria hii pia ilitangaza maeneo ya mapori tengefu katika maeneo ya Vijiji na haikuondoa haki ya milki ya ardhi ya wananchi katika ardhi ya Vijiji.

Mwaka 2009, Sheria mpya ya wanyamapori ilitungwa ambapo pia ilifuta Sheria ya Uhifadhi wa Wanyama Pori ya 1974. Mabadiliko ya Sheria ya Wanyamapori yalibadili hadhi ya mapori tengefu na kuondoa shughuli zote za kibinadamu kama ilivyokuwa awali. Sheria hii kwa kutambua kuwa maeneo mengi yaliyokuwa na mapori tengefu ni ardhi halali za vijiji iliweka utaratibu katika kifungu cha 16 (4) hadi 16 (5) kwa Waziri mwenye dhamana (Maliasili na Utalii) kufanya mapitio upya na kuondoa mapori tengefu katika ardhi za Vijiji ndani yam waka moja baada ya Sheria hiyo kuanza kutumika (" For the purpose of sub-section 4 , The Minister shall ensure that no land falling under the village land is included under the game controlled areas' Section 16).

Tafsiri yake ni kuwa, kwa kutambua kuwa maeneo mengi karibu asilimia 60 ya GCA hapa nchini yalikuwa katika ardhi ya vijiji, Bunge ambalo ni muhimili wa kutunga Sheria liliona muhimu wa kuondoa mapori tengefu katika maeneo ambayo ni ardhi za vijiji kama ilivyokuwa kilometa za Mraba 4000 za Loliondo GCA. Bahati mbaya zoezi hili kwa upande wa Loliondo halikufanyika kama sheria ilivyoagiza, badala yake kumekuwemo na maneno mengi kuwa bado Loliondo nzima ni GCA kinyume na utaratibu wa sasa wa kisheria ambao hauruhusu GCA kuchangamana na shughuli za kibadamu. Matokeo yake ni kwamba kwa mujibu wa sheria ya Wanyama Pori ya sasa Loliondo hakuna tena pori tengefu inayotambulika kisheria. Kwa uchambuzi huu ni wazi kuwa eneo lote la kilometa za mraba 4000 za Loliondo na Sale ni ardhi halali ya vijiji.

## HISTORIA NA MADHARA YA MGOGORO

### Historia na Chanzo cha Mgogoro wa Ardhi Tarafa ya Loliondo na Sale

Taarifa na kumbukumbu zinaonyesha kuwa migogoro katika Tarafa za Loliondo na Sale zilianza kabla ya Uhuru wa Tanganyika, na imekuwa ikichukua sura tofauti kadiri muda unavyo kwenda. Kwa mantiki hiyo, uchambuzi wa matukio, sura ya migogoro ya ardhi katika Tarafa hizi zinaweza kupangwa katika vipindi tofauti vya kihistoria. Migongano hii kwa kiasi kikubwa imekuwa baina ya Wenyeji-Wafugaji wa Kimaasai na Wizara ya maliasili na Utalii kwa nyakati tofauti. Aidha, sababu za migogoro imekuwa ni mgongano wa maslahi ya maisha kwa wenyeji, na ya kibiashara/uhifadhi kwa upande wa watawala na wawekezaji. Kwa mujibu wa taarifa mbalimbali, mgogoro huu umegawanyika katika sehemu kuu tatu, ambazo ni kipindi cha utawala wa wakoloni, baada ya uhuru na baada ya ujio wa kampuni ya kiwindaji ya OBC mwaka 1992.



- **Kuondolewa kwa wafugaji wa Jamii ya Kimasai kupisha uanzishwaji wa Hifadhi ya Serengeti 1958**

  Mgogoro huu wa tarafa za Loliondo na Sale ulianza miaka 1950 baada ya serikali ya kikoloni kuwaondoa wananchi wa jamii ya wamasai waliokuwa wakiishi Serengeti ili kupisha uanzishaji wa Hifadhi ya Serengeti. Mwaka 1958 makubaliano yalifikiwa baada ya mazungumzo ya miaka zaidi ya 8 kwa Jamii ya wamasai kushurutishwa kukubaliana na kuridhia mipaka na maslahi mengine kupitia "Serengeti Compensation Scheme". Mwaka mmoja baada ya makubaliano kufikiwa Hifadhi ya Serengeti ilianzsihwa rasmi mwaka 1959, sambamba na Hifadhi ya Ngorongoro (1959) ambako serikali ya kikoloni ilikubali kufanya majaribio ya kuwa na hifadhi yenye matumizi mseto ya ardhi (wanyamapori, shughuli za binadamu, na utalii).

  Katika makubaliano ambyo hadi sasa hatuna uhakika na uhalali wake, kupitia mpango wa Mfumo wa Fidia ya Serengeti, serikali ya kikoloni ilitoa ahadi lukuki kwa wafugaji endapo watakubali kuhama kwenda maeneo ya Loliondo na Nyanda za juu za Ngorongoro. Kwanza, tulihaidiwa kupewa huduma za mifugo kama majosho, maji, na huduma zingine za kijamii. Pili, tulihaidiwa kuwa huko tuendako upande wa mashariki mwa Serengeti (Loliondo) endapo patatokea mgogoro baina ya Wamasai na shughuuli za uhifadhi, haki zetu zitapewa kipaumbele zaidi. Baada ya sisi kuhamishwa baadhi ya ahadi hizo hazikutekelezwa na Serikali hiyo ya Kikoloni lakini na zingine kwa sasa haziheshimiwi na serikali ya sasa.

  Kutokuheshimiwa na kutotambuliwa kwa makubaliano haya ndiyo yamepelekea kuendelea kwa mgogoro huu wa ardhi baina ya jamii ya wamasai na Wizara ya Maliasili na Utalii na Kampani ya OBC kwa upande mwingine. Hali hii imechangia jamii yetu ya Kimasai kuendelea kufukuzwa katika maeneo yao ya asili kwa lengo la uwekezaji wa uwindaji.

- **Mgongano wa Sheria za ardhi, Serikali za Mitaa na Sheria za wanyamapori**

  Mgongano kati ya Sheria za ardhi, Serikali za Mitaa na sheria za uhifadhi wa wanyamapori juu ya matumizi ya ardhi. Baada ya uhuru serikali ya Tanzania iliendeleza sera za kikoloni ambapo miaka kadhaa baadae yaani mwaka 1968 iliongeza mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti

kupitia Tangazo la Serikali (GN. 235/1968) na katika kifungu cha tano ikatamka mipaka na kuionyesha kwenye ramani Na. 14151 mipaka mipya ya Hifadhi ya Taifa Serengeti.

Mwaka 1974 serikali ilitunga sheria ya Uhifadhi wa Wanyama Pori ya mwaka 1974 na kuanzisha mapori tengefu ambapo Loliondo na Sale yalitangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 269 la 1974. Hata hivyo Sheria ya uhifadhi wa wanyama pori ya wakati huo haikuwa na mgogoro na shughuli za kibinadamu katika maeneo ya Vijiji na ndiyo maana ilikuwa rahisi kutangaza mapori tengefu katika ardhi za vijiji ambavyo viliandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria zingine za nchi.

Katikati ya mgogoro huu serikali ilitunga Sheria ya uhifadhi wa Wanyama pori ya 2009, ambayo ilikataza shughuli za kibinadamu ndani ya mapori tengefu. Mwingiliano, utata na mgogoro wa kisheria iliongezeka baada ya Serikali kutaka kutenga eneo halali la Vijiji lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,500 kama sehemu ya utekelezaji wa sheria hiyo ambayo majaribio ya utekelezaji yaliaza Katika Tarafa za Loliondo na Sale pekee nchini kabla ya kutangazwa kwa tarehe ya kuanza kutumika. Hata hivyo jaribio hili lilionekana kuwa kinyume hata na sheria yenyewe ya Wanyama Pori ya 2009, iliyoagiza mabadiliko yoyote yafanyike ndani ya mwaka mmoja baada ya sheria hiyo kuanza kutumika kama ilivyofafanuliwa katika sura ya tatu.

- **Ujio wa Kampuni ya Ortello Business Corporation**

Mwaka 1992, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia ofisi yya Mkuu wa Wilaya Ngorongoro, Mhe Mbunge na mwenyekiti wa Halmashauri ilisaini Mkataba wa uwindaji na Mhe Brigadia Mohamed Abdulahim Al-Ali ndani ya ardhi ya vijiji vya Tarafa za Loliondo na Sale bila kupatikana ridhaa ya vijiji (rejea mkataba ulioingiwa katika makundi tajwa hapo chini). Baadae shughuli zote za uwindaji kwa niaba ya Mfalme huyu zilianza kutekelezwa na kusimamiwa na kampuni iliyoanzishwa kwa malengo haya, ambayo ni Ortello Business Corporation (OBC), katika eneo la Vijiji vya Tarafa za loliondo na Sale lenye ukubwa wa kilometa za mraba 4000.

Kwa sababu ya kukosekana kwa ridhaa ya wananchi kupitia mamlaka za vijiji, serikali ilivunja sheria za mikataba kwa kuchukuwa nafasi ya vijiji na kusaini mkataba kwa niaba yao bila ridhaa ya vijiji. Tukio hilo linakuwa la pili katika mtiririko wa kuchukua nafasi ya jamii na au kufinya nafasi ya ushiriki wa jamii katika kuamua mustakabali wa usalama wa ardhi yetu.

Hali hii ilizua taharuki kubwa iliyojulikana kwa jina la 'Loliondo Gate Scandal'. Kampeni hii ilivuka mipaka ya Tanzania na kuhusisha mitandao, vyombo vya habari na watetezi wa haki za binadamu duniani. Wakati huo, mgogoro huu maarufu wa Loliondo ulihusu jamii kudai nafasi ya ushiriki katika maamuzi ya mpangilio na matumizi ya ardhi yao.

Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii ilisimama kumtetea Mfalme kwa kisingizio kwamba ni mwekezaji mwenye faida kwa nchi yetu na hadhi ya kidipomasia. Kupitia mapishano haya kwa miaka yote, mgogoro huu umejengwa na kubebwa na dhana ya uhifadhi kwa upande wa serikali na mwekezaji, na usalama wa ardhi na malisho kwa upande wa jamii.

**Mikakati na hatua za OBC kutengewa ardhi ya vijiji**

Mwaka moja tu baada ya OBC kuanza kazi, Rasimu ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi Wilaya ya Ngorongoro (Ngorongoro District Land Use Framework Plan (1993 – 2008) ilitayarishwa kwa msaada wa OBC na kuanisha eneo (linalokadiriwa sasa kuwa ni km za mraba 1500) kuwa eneo linalopaswa kutumika kwa madhumuni ya Uhifadhi wa wanyama pori na utalii. Ni muhimu kutambua kuwa hata mpango huu wa matumizi ya ardhi, 1993-2008, haukuandaliwa katika mazingira ya ushiriki wa wananchi bali kwa msukumo wa kampuni ya OBC. Na kwa sababu hiyo, mpango huu wa kwanza wa kutaka kuchukua ardhi ya vijiji kupitia mpango wa matumizi bora ya ardhi ulikwama.

Mwaka 1996, Kampuni ya OBC ilianzisha hatua za kuweka miundombinu ya kufanikisha shughuli zake zikiwepo, ujenzi wa barabara, kempu na uwanja wa ndege bila ushirikishwaji wa wananchi. Ujenzi wa miundombinu hizi, ziliibua tena hasira kwa wananchi. Hata hivyo, taratibu za kimazingira hazikuzingatiwa hasa baada ya kempu ya kudumu kujengwa katika chanzo cha maji ya mto Olasae.

Mgogoro wa Loliondo- katika Tarafa za Loliondo na Sale umekuwa ni mgogoro mkubwa na wenye kubadilisha sura na mikakati kwa nyakati tofauti. Kampuni ya OBC kwa kushirikiana na serikali ilifadhili uundwaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya Wilaya ya mwaka 2010-2030, na kwa kutumia ushawishi wake wa fedha, rasimu hiyo ilibainisha eneo la km za mraba 1500 kama eneo la kutengwa kwa ajili ya uhifadhi/uwindaji. Hapa ndipo namba hizi maarufu 1500 ziliendelea kujitokeza. Pamoja na kwamba huwezi kutengeneza mpango wa matumizi bora ya Wilaya bila kukamilisha

mipango ya Vijiji, OBC ilishawishi Serikali kuendelea na Mpango huo ambayo ilikataliwa na baraza la madiwani Wilaya kwa mantiki ya kutokuwa na ushirikishwaji

**Majaribio ya kuwaondoa Wananchi katika Ardhi ya Vijiji**

Baada ya kushindikana kwa taratibu zingine za kisheria na kisera kuchukua eneo la km za mraba 1500, kampuni ya OBC na wandani wake wakabadilisha mbinu na kuanza kutumia nguvu za dola kutaka kutuondoa katika ardhi yetu. Nguvu hizi zimepelekea ukikuwaji mkubwa wa haki za binadamu kama inavyojitokeza katika sehemu mbalimbali za taarifa hapo chini. Tangu Kampuni ya OBC kuanza kufanya shughuli za uwindaji katika ardhi ya vijiji matukio mbalimbali yafuatayo katika jedwali husika hapo chini.

- **Mapendekezo ya Kamati ya Mapitio ya Matumizi Mseto ya Ardhi ya Ngorongoro**

  Kamati ilipendekeza kumegwa ardhi ya Vijiji kwa upande wa Loliondo yenye ukubwa wa kilomita za mraba 1500. Ikumbukwe kuwa ardhi hii ya Vijiji imekuwa na mgogoro kati ya Wizara ya maliasili na Utalii, wananchi pamoja na kampuni ya uwindaji ya OBC kwa takribani miaka 30 bila suluhu. Mapendekezo hayo ya kamati yanalenga kuchochea mgogoro uliokuwepo na si kutatua kwa kuwa Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro ilishindwa kwa muda mrefu kutatua migogoro kati yake na jamii inayoishi ndani ya mamlaka.

  Kwa upande wa Ziwa Natron ambapo inajumuisha Vijiji vya Kata za Engaresero na Pinyinyi, kamati ilipendekeza kumegwa ardhi ya Vijiji yenye ukubwa wa kilomita za mraba 2,804.14, ambapo itagusa pia maeneo ya Monduli na Longido kwa lengo hilo hilo la kuongeza eneo la NCA. Eneo hili pia ni ardhi halali ya Vijiji vilivyopimwa, kupata vyeti vya ardhi vya Vijiji (CVLs) na kufanya mipango ya matumizi ya ardhi ambapo ardhi yote imepangiwa matumizi. Vilevile katika maeneo ya makazi watu moja moja kwa kiasi kikubwa wamemilikishwa ardhi kwa taratibu za Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya 1999. Hivyo eneo hili kuingizwa kwenye mipaka ya Mamlaka ya Hifadhi ya ngorongoro ni kuvunja sheria za ardhi na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ibara ya 24.

**Madhara Yatokanayo na Jitihada za Kuchukua Ardhi ya Vijiji (sq km 1500) kwa jamii**

**a) Ukiukwaji wa Haki za Binadamu**

Katika sakata hili la kutuondoa kwa nguvu katika maeneo ya Vijiji vyetu kwa nyakati tofauti (2009, 2013, 2014 na 2017) kumesababisha ukiukwaji mkubwa wa haki zetu. Aidha, ilitokea vifo vingi vya mifugo kwa kukosa malisho, maji na mengine kupotea. Ukiukwaji wa haki za binadamu katika eneo hili limeandikwa kwa wingi kwa miaka 30 sasa na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi kama inavyoonekana katika orodha ya marejeo ya taarifa hii. Kwa kuonyesha upana wa tatizo operesheni ya mwaka 2017, pekee inaonyesha watu 138 waliweza pata changamoto mbalimbali kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini

- **Kuchomwa kwa Makazi na Mali za Wananchi**

  Katika matukio mengi yaliyokiuka haki za binadamu, uchomaji wa makazi na mali za wananchi ni moja ya matukio makubwa yaliyofanywa vyombo vya dola katika maeneo yetu. Makazi katika Maisha yetu ya kimila ni zaidi ya tafsiri ndogo inayofahamika kuwa makazi ni nyumba za kisasa pekee. Makazi katika jamii yetu hujumuisha hadi maeneo ya kuhifadhia mifugo, ndama na mazingira yanayozunguka na kupelekea kuharibu mfumo wa maisha yetu. Imekuwa vigumu kupata takwimu za miaka yote ya mgogoro lakini takwimu za Mwaka 2017 zinaonyesha kati ya maboma 4,698 maboma 1,190 zilizochomwa Moto. Kuchomwa kwa maboma haya kumepelekea robo ya wananchi wote wanaoishi katika eneo hili kuadhirika pamoja na mali zao ambazo nyingi zinathamani za kimila.

- **Kupigwa na Kuteswa**

  Operesheni zote nne (2009,2013,2014 na 2017) zimepelekea wananchi kupigwa, kuteswa na wengine kuwa vilema kutokana na matumizi ya silaha za moto. Ni muhimu kufahamika kuwa wakati wote wa manyanyaso haya kama wananchi hatukuwahi kufanya jitahada zozote za kujitetea kwa njia za kupambana au kuchukua sheria mkononi. Mifano ya watu waliopata changamoto hizi kati ya wengine ni pamoja na Ngodidio Rotiken wa Kijiji cha Kirtalo 2009, na Parmoson Ololoso wa Ololosokwan, 2017. Pamoja na kwamba serikali inatumia nguvu kubwa kuwaondoa wananchi katika eneo lao la vijiji wamekuwa wakitumia risasi za moto kinyume na sheria.

- **Vitisho, Kukamatwa na Kubambikizwa Kesi**

  Katika operesheni zote au jitiahda zote za kutaka kutuondoa katika maeneo yetu, tumeshuhudia wenzetu wengi wakikamatwa na polisi na kubambikizwa kesi. Wananchi wenzetu wamekuwa wakikamatwa na kupelekwa katika vituo vya polisi na wakati mwingine katika mahakama zilizoko nje ya Wilaya kama kule Mugumu Wilaya ya Serengeti. Kwa operesheni zote za miaka yote mitatu takriban zaidi ya watu 200 walikamatwa na kupelekwa katika vituo vya polisi na wengine kushtakiwa Mahakamani. Kwa mfano kwa nusu ya mwaka 2022 pekee zaidi ya watu 20 wameshakamatwa na wengine kutakiwa kurepoti mara kwa mara katika vituo vya polisi.

  Matukio haya ya vitisho, kamatakamata na kubambikziwa kesi yamekumba zaidi wananchi, viongozi wao wa kisiasa, viongozi wa kimila, waandishi wa habari, mawakili na watetezi wa haki za binadamu. Baadhi ya watetezi na viongozi wa wananchi wamefikishwa katika vituo vya polisi na wengine kutishiwa, kuhojiwa au kufunguliwa kesi za uchochezi. Lengo la vitisho kwa watetezi ni kutaka kuwanyamazisha wasidai au kushiriki katika kutafuta suluhu ya mgogoro huu wa ardhi hasa kwa upande wa wananchi.

  Vitisho hivyo vya wanaharakati, waandishi wa habari na viongozi vimeleta tishio na taharuki kwa wananchi na kutukosesha uhuru wa kufanya majukumu yetu na kujadili mambo yanayohusu utetezi ambayo ni haki yetu kikatiba.

- **Wananchi wa Tanzania kuitwa Wahamiaji kutoka Mataifa ya Jirani**

  Kwa zaidi ya miongo miwili vyombo habari na baadhi ya viongozi wa Serikali kwa nyakati tofauti vimeendelea kuripoti kuwa asilimia kubwa ya watanzania waishio katika tarafa hizi ni wahamiaji kutoka nchi mbalimbali zikiwemo Kenya na Sudan ili kuwatishia katika harakati za kudai haki zao za ardhi. Mfano Gazeti la Jamhuri lilikuwa likitumika kuandika matukio haya ya kusema watanzania wa Loilondo ni wakenya ili kulinda maslahi ya mwekezaji wa OBC.Kwa miaka mingi sasa OBC pamoja na Wizara ya Maliasili na utalii wamekuwa wakitumia baadhi ya vyombo vya habari katika kufanya propaganda za kupotosha taarifa za ukweli kuhusu loliondo, ambapo imepelekea watu wengi kukamatwa na kusababisha kuchochea mgogoro zaidi. Zaidi ya asimilia 70% ya watu wa loliondo wametuhumiwa kuwa ni wakenya nasio raia wa Tanzania.

- **Madhara ya Kiuchumi kwa Wananchi**

  Kila jamii ya kitanzania inafahamika inategemea shughuli zipi katika kujiwezesha kiuchumi ambayo kwa sisi wafugaji sughuli kuu ya kiuchumi ni ufugaji. Eneo hili la Vijiji lenye mgogoro linategemewa kwa asilimia 90 kwa malisho ya mifugo katika Vijiji vyote vya Tarafa za Loliondo na Sale hasa katika Kata Nane zenye Vijiji zaidi 23 na mifugo takriban 973,745 ziliondolewa kwa nyakati tofauti za operesheni katika eneo la mgogoro. Kama inavyofahamika jamii ya kiamasai kuwa kitega uchumi yao ni mifugo hii ni dhairi kuwa Operesheni hizo zilisababisha anguko kubwa la kiuchumi katika jamii yetu kwani ufugaji ndiyo shughuli kuu ya kiuchumi. Operation zote zimekuwa zikitekelezwa nyakati ngumu za kiangazi kitu ambacho inatupelekea tuamini kuwa nia yake ni kutufisili kiuchumi.

- **Ukamataji wa Mifugo**

  Operesheni hizo pia ziliambatana na ukamataji wa mifugo nje ya eneo la Hifadhi ya Serengeti kwa kuwa kulikuwa ushirikiano wa maaskari wa SENAPA na Kampuni ya OBC ambayo ilikuwa inafanya hujuma na uchochezi katika mgogoro. Mwaka 2017, mifugo 290 zilikamatwa pamoja na watu 6 na kufunguliwa mashtaka katika Mahakama ya Wilaya ya Serengeti iliyoko Mugumu, kwa kesi ya jinai Na. 187, ambapo baada ya wananchi kutoridhika na maamuzi walikata rufaa kwenda mahakama kuu kanda ya Mwanza, ambapo walifungua shauri la jinai kati ya Noonkirimban Seret Sironga v. Republic.  Tarehe 11/01/ 2018 Mahakama litoa hukumu ya ushindi kwa wananchi na Hifadhi ya Sengeti iliamuriwa kurudisha mifugo ya wananchi iliyokuwa imetaifishwa kwa wamiliki halali.

- **Wananchi kukosa Mapato Kutokana na Mgogoro wa Kampuni ya OBC**

  Kabla ya mgogoro huu uliosababishwa na kampuni ya OBC kutokea katika eneo la tarafa za Loliondo na Sale, vijiji vilikuwa vikijishughulisha na biashara ya utalii wa picha na kupata mapato. Kutokana na mgogoro huu makampuni hayo ya kitalii yaliondoka na hivyo kuathiri fursa na huduma za kijamii kama elimu, afya na ajira zilizokuwa zinatolewa kutokana na manufaa ya uwepo wa shughuli hiyo ya kitalii. Takribani makampuni 5 ziliondoka katika eneo la vijiji kwa sababu ya kampuni ya OBC na kusababisha hasara kubwa kwa vijiji kwa kukosa mapato, zaidi ya wanafunzi waliokatiza masoma na miradi mingi ya afya, maji kusimama na kusababisha wananchi kuchangishwa tena kwa ajili ya kumalizia.

Pamoja na rasilimali za vijiji kuendelea kuvunwa na kampuni ya uwindaji ya OBC, vijiji kutoka tarafa hizi hazikunufaika na uwepo wa kampuni hii ya uwindaji. Baadhi ya kampuni ambazo zilisitisha shughuli zao kutokana mgogoro huu ni zaidi tano (5) kama zinavyoonekana katika jedwali hapo chini

## HOJA ZA SERIKALI NA MAONI YETU

Tangu mgogoro huu wa Loliondo uibuke miaka ya tisini kumekuwa na hoja hasa kwa upande wa serikali juu ya sababu za eneo hili la vijiji kumegwa. Hoja hizo zimekuwa zikitolewa ili kuhalalisha sababu ya kumega eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 1500 toka ardhi ya vjiji na hivyo mgogoro kuchukua sura tofauti huku serikali ikitoa sababu zake na wananchi wenyeji nao wakitoa za kwao.

Baadhi ya hoja za Serikali ambazo imekuwa ikizitolewa kwa lengo la kutaka kumega eneo la km za mraba 1500 ni kama ifuatavyo; Mosi, eneo hilo ni eneo la ushoroba na mapitio ya Wanyama, Pili, eneo hilo linatumika zaidi na Wanyama kama eneo la mazalia, Tatu, ni eneo la vyanzo vya maji vya ikolojia ya serenegeti, eneo hilo ni la wazi na sio ardhi ya vijiji, Tano, kutunza mazingira na ekolojia ya Serengeti-mara na Sita, eneo hilo linamegwa kwa ajili ya wawekezaji wa utalii na uwindaji.

Baada ya vikao mbalimbali vya wananchi na kupitia hoja moja baada ya nyingine, wanavijiji kupitia mikutano yao na uwakilishi wao mbalimbali wamekuwa na hoja zifuatazo zinazolenga kujibu hoja za serikali;

- Jamii inaona kuwa uwepo wa jamii na mifugo haina madhara kwa mzunguko wa Wanyama kwa sababu zifuatazo: Ni muhimu kujua kwamba eneo hili kwa kawaida lina matumizi mseto kati ya binadamu, mifugo na wanyama pori kabla na baada ya uhuru. Mfumo huu ni jumuishi, shirikishi na rafiki kati ya jamii na uhifadhi. Kwa muda wote mifugo, binadamu na wanyama pori wameishi pamoja bila madhara kwa kuwa maslahi ya pande zote yanazingatiwa na kuheshimiwa kwa taratibu za mila na desturi za jamii husika kama ilivyofafanuliwa katika sura ya pili ya taarifa hii, Kwa kipindi cha kuhama kwa nyumbu wafugaji huondoa mifugo yao ili kupisha wanyama kwani wanaweza kusababisha madhara ya magonjwa na wakati mwingine kuondoka na mifugo na kupotea kwa kuwa wanahama kwa makundi makubwa. Hoja ya kutenga km za mraba 1500 kwa ajili ya mapition ya wanyama haijajitosheleza kwa kuwa mtawanyiko wa wanyama upo maeneo mengi ya wilaya.

- Ifahamike kuwa katika hili, wanyamapori ambao huzaa kwa makundi makubwa na kwa wakati mmoja ni nyumbu, pundamilia na swala. Wakati wa kuzaliana kwa nyumbu wafugaji wanahama na mifugo yao yote kwa muda wa miezi zaidi ya 5 (Disemba hadi Aprili) ili kuruhusu nyumbu wazae na ndama kupoteza manyoya. Hii ni kwa sababu manyoya, kondo na utando (inkipa kwa Kimasai) ya nyumbu husababisha homa kwa mifugo ijulikanayo kwa lugha ya kiingereza kama Malignant Catarrhal Fever (MCF) isiyo na tiba na kupelekea vifo vingi kwa mifugo.

- Baada ya mikutano na majadiliano mengi ya wananchi kuhusu hoja hii ya hadhi ya ardhi yao kisheria, na kwa kupitia wanasheria wa kijami, msimamo wa sasa wa wananchi wa Loliondo ni kuwa kwa sasa Loliondo hakuna tena Pori Tengefu baada ya Mabadiliko ya Sheria ya Mwaka ya 2009. Wananchi wanaamini eneo lote la km za mraba 4000 kwa sasa hazina tena hadhi ya pori tengefu kama Sheria ya 2009 ilivyoagiza kuwa hakutakuwa tena na ardhi ya Kijiji itakayokuwa na mapori tengefu. Sheria iliagiza kuondelewa kwa mapori tengefu katika maeneo yote yenye ardhi za vijiji. Soma zaidi sura ya pili ya taarifa hii kuelewa uchambuzi wa kijamii kuhusu uhalali wa ardhi yenye mgogoro kwa sasa.

- Hoja zetu zingine kuhusiana na hoja hii kama ifuatavyo; Ni muhimu serikali na jamii ya watanzania kuelewa kuwa kihistoria eneo hili halikuwahi kuwa wazi tangu enzi za mababu, wakati wa Ukoloni, baada ya Uhuru hadi sasa kama ilivyoonyeshwa katika Sura ya pili ya taarifa hii.

## MAPENDEKEZO YA WANANCHI

1. Serikali itambue kuwa eneo hili lenye kilomita za mraba 1500 katika Tarafa za Loliondo na Sale, ni eneo halali la Vijiji kwa mujibu wa sheria za nchi kama ilivyo chambuliwa katika Sura ya pili ya taarifa hii.
2. Sisi wananchi wa Vijiji Vya Tarafa za Sale na Loliondo tupo tayari kujadiliana na Serikali ili kutafuta suluhu ya kudumu kuhusu mgogoro huu ambao umedumu kwa takribani miaka 30.
3. Kimsingi, chanzo kikuu cha mgogoro huu kati ya wananchi na Wizara ya Maliasili na Utalii kimesababishwa na kuchochewa na Kampuni ya OBC, hivyo ili tuweze kuishi kwa amani katika Vijiji vyetu na kuendelea kuwa na mahusiano mazuri na Serikali yetu, kampuni hii

iondolewe katika eneo hili la Tarafa za Loliondo na Sale ili tupate nafasi huru ya kujadili swala la uhifadhi na maendeleo ya wananchi kwa kushirikiana na Serikali yetu.

4. Kufanya mapitio ya mipango ya matumizi ya ardhi ya Vijiji ili kukidhi mahitaji ya sasa na baadae ya kijamii, kiuchumi, kimazingira na kiutawala kwa Mujibu wa Sheria za Mipango ya Matumizi ya Ardhi Na. 6 ya 2007 na Sheria ya ardhi ya Vijiji Na.5 ya 1999.

5. Wizara ya Maliasili na Utalii isitishe azma ya kumega sehemu ya ardhi ya vijiji kwa matumizi ya uhifadhi na uwindaji kwani eneo hili ni ardhi halali ya Vijiji husika. Serikali itambua na kuendeleza uhifadhi wa kijamii kwa malengo ya kulinda rasilimali asili pamoja na haki za ardhi wafugaji.

6. Tunapendekeza baada ya kufanyika kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa kila kijiji, Wananchi waunde Kamati Jumuishi ya vijiji vyenye mgogoro ili kuratibu shughuli zinazofanyika katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na shughuli za malisho ya mifugo, uhifadhi wa wanyamapori, utalii, utunzaji wa mazingira, ibada za kimila na utunzaji wa vyanzo vya maji.

7. Serikali ikatae pendekezo la kumegwa kwa eneo la ardhi ya Vijiji vya Loliondo na Sale lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1500 na eneo la Ziwa Natron inayojumuisha Kata za Pinyinyi na Engaresero kwa lengo la kuingizwa kwenye eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCA) kama ilivyopendekezwa na Kamati ya wahifadhi ya matumizi mseto ya ardhi yaani Multiple Land Use Model (MLUM) ya 2019.

8. Serikali itambue kwamba eneo hili ni muhimu kiuchumi kwa wafugaji wa Vijiji vya Tarafa za Loliondo na Sale ambalo linategemewa na watu zaidi ya 66,000, kwani kupoteza ardhi hiyo ni kuwarudisha wananchi katika umaskini na ufukara wa kutisha.

9. Serikali itambue kuwa eneo hili sio wazi bali ni nyanda za malisho ya mifugo. Wananchi wa eneo hili, wanategemea kwa zaidi ya asilimia 90 kwa shughuli za ufugaji asili kama chanzo kikuu cha mapato na chakula.

10. Tunashauri Serikali izingatie shauri linalohusu mgogoro huu ambalo lipo katika Mahakama ya haki ya Afrika Mashariki.

11. Tunaisihi Wizara ya Habari na Mamlaka ya Mawasiliano nchini kupiga marufuku vyombo vya habari visivyo fuata maadili ya uandishi ambavyo vinatoa taarifa za uongo, upotoshaji na uchonganishi kati

ya serikali na wananchi wa Tarafa za Loliondo na sale.

12. Tunashauri Serikali itambue haki za mashirika na watetezi wa kijamii na haki za binadamu ambao wamekuwa wakisumbuliwa mara kwa mara wanapojaribu kusaidia serikali na jamii kutatua changamoto hizi.

13. Tunahimiza Serikali ipige marufuku kamata kamata ya viongozi wa kijamii inayoendelea kwa sasa katika Tarafa za Sale na Loliondo. Kitendo hichi kinaendelea kuzua taharuki miongoni mwa jamii na pia kufifisha jitihada za pamoja za kutatua changamoto hizi.

14. Tunapendekeza kuundwa kwa Tume Huru ya kuchunguza ukiukwaji wa haki za binadamu na haki za wafugaji zilizofanyika kwa kipindi cha miaka 30 iliyopita katika eneo lenye mgogoro.

15. 16. Tunapendekeza kuwa kuanzia sasa swala la mgogoro wa Loliondo na Sale uwe unakwenda kwa njia ya mazungumzo kupitia kamati hii ya jamii pamoja na serikali ili kupunguza mvutano isiyokuwa ya lazima. Kamati hii itasaidia kuondoa mwanya wa watu wasiohusika na mgogoro huu na wanaotoka nje ya Wilaya ya Ngorongoro kutumika katika majadiliono ya kutatua mgogoro huu.

16. Kwa kuzingatia kuwa nchi ipo katika uchumi wa kati, serikali iboreshe na kufungua fursa mbali mbali za kibiashara kwa kuboresha miundo mbinu hasa masoko, Kiwanda cha kuchakata mazao ya mifugo, elimu za ufugaji wenye tija, mtandao wa barabara za lami nk. Hatua hii itatoa fursa kwa wananchi kupata fursa za kimaendeleo kwa haraka na kuchangia pato la taifa pamoja na kupunguza migogoro ya rasilimali.

17. Serikali ifanye jitihada za haraka kuwekeza katika Elimu ili kuendeleza watoto wa jamii hii. Hii ni Pamoja na serikali kujenga shule za Msingi katika kila kitongoji kilichopo Zaidi ya kilomita 7 kutoka kitovu cha Kijiji.



# SURA YA KWANZA

# TAARIFA ZA AWALI

## 1.0 UTANGULIZI

Sura hii ya kwanza inatoa taarifa za awali zinazoelezea eneo la Wilaya, Muundo wa Wilaya, matumizi ya Ardhi katika Tarafa za Sale na Loliondo, malengo ya taarifa hii, njia za ukusanyaji taarifa, idadi ya watu na mifugo katika eneo hili.

### 1.1. Mahali ilipo Wilaya ya Ngorongoro

Halmashauri ya Wilaya Ngorongoro ni mojawapo kati ya Halmashauri za Wilaya sita na Jiji moja zilizopo katika Mkoa wa Arusha Nchini Tanzania. Wilaya hii inapakana na Nchi jirani ya Kenya kwa upande wa Kaskazini, Wilaya ya Serengeti kwa upande wa Magharibi, Wilaya ya Meatu kwa upande wa Kusini magharibi, Wilaya za Monduli na Longido kwa upande wa Mashariki na Wilaya ya Karatu kwa upande wa Kusini.Makao Makuu ya Wilaya yapo Loliondo -Wasso umbali wa takriban kilomita 400 kutoka Makao Makuu ya Mkoa. Wilaya hii ilianzishwa mwaka 1979 ikiwa na Tarafa tatu za Loliondo, Sale na Ngorongoro.




***Ramani 1.1:*** *Ramani ya Wilaya ya Ngorongoro*


Wilaya ya Ngorongoro ina eneo la kilomita za mraba zipatazo 14,036 ambalo lipo katika nyuzi 30030’ kusini mwa Ikweta na 35042’ Mashariki mwa Greenwich na urefu wa mita 1,009 hadi 3,645 kutoka usawa wa bahari[1].

***Jedwali 1.1:*** *Mgawanyo wa ardhi kwa kila tarafa katika Wilaya ya Ngorongoro*

| | Tarafa | (km²) | Asilimia |
|---|---|---|---|
| | Tarafa ya Ngorongoro | 8,300 | 59.13 |
| | Tarafa ya Sale | 3,518 | 25.06 |
| | Tarafa ya Loliondo | 2,218 | 15.80 |
| **Jumla** | | **14,036** | **100** |

### 1.2 Ukubwa wa Tarafa ya Sale na Loliondo

Tarafa ya Loliondo na Sale kwa ujumla zina eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 5,744 ambayo kwa wilaya ya Ngorongoro ni sawa na 41% ya eneo lote la wilaya. Kati ya eneo lote la kilomita za mraba 5,744 eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,744 linajumuisha eneo lote la tarafa ya Sale isipokuwa kata za Malambo na Piyaya ambazo ni sehemu ya eneo la kilomita za mraba 4000 zinazojumuisha eneo lote la tarafa ya Loliondo. Eneo hili la kilomita za mraba 4000 ni eneo la ardhi ya vijiji na mji mdogo wa Loliondo na maeneo ya Sale. Mchanganuo huu wa ukubwa wa Tarafa za Sale na Loliondo umefafanuliwa katika Grafu ifuatalo;





***Grafu 1.1:*** *Mgawanyo wa Ardhi katika Tarafa za Loliondo, Sale and Ngorongoro*

Eneo hili ndilo lenye kilomita za mraba 1500 ambalo limekuwa na mgogoro

1 https://ngorongorodc.go.tz/historia, imerejewa tarehe 30 April, 2022


wa ardhi kwa muda mrefu ikijumuisha kata mbili (2) za Malambo na Piyaya vya Tarafa ya Sale, na kata sita (6) za tarafa ya Loliondo kata za Arash, Oloipiri, Maaloni, Oloirien, Soitsambu na Ololosokwan zenye jumla ya vijiji 23. Ieleweke kwamba mgogoro huu wa ardhi ya Vijiji inatokana na mgongano wa maslahi ya matumizi mbalimbali ya ardhi katika eneo la ardhi za Vijiji baina ya wananchi, mwekezaji (OBC) na Serikali. Mgogoro huu umedumu kwa zaidi ya miaka 30 ambapo kwa miaka ya hivi karibuni imechukuwa sura mpya baada ya serikali kuanza mchakato wa kumega ardhi hiyo ya Vijiji bila ridhaa ya wananchi na kuzua taharuki kubwa kila kona katika tarafa hizo.




***Ramani 1.2:*** *Ramani ya Tarafa za Sale na Loliondo*

*Chanzo: Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Wilaya ya Ngorongoro, 1994*


Idadi ya Watu: Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, Wilaya ya Ngorongoro ilikuwa na idadi ya watu 174,278 Wanaume wakiwa ni 82,610 na Wanawake ni 91,668 ambapo wastani wa ukubwa wa kaya ni 4.8 na ongezeko la watu katika Mkoa wa Arusha ikiwa ni asilimia 2.93.





***Grafu 1.2:*** *Idadi ya Watu Katika Wilaya ya Ngorongoro*


Eneo la Vijiji la kilomita za mraba 1500, katika tarafa ya Loliondo na kata mbili za tarafa ya Sale ya Piyaya na Malambo hujumuisha vijiji vipatavyo 23, wanaotegemea eneo hili, kwa maisha ya wafugaji na mifugo yao. Mbali na umuhimu wa malisho ya mifugo, eneo hili la kilomita za mraba 1500, hutumika na wamaasai kwa ajili ya shughuli za tamaduni hasa matambiko; kuabudia na maeneo yenye miti kwa ajili ya tiba za asili.

***Grafu 1.3:*** *Idadi ya watu katika Tarafa ya Loliondo na Kata za Malambo na Piyaya tarafa ya Sale*




Idadi ya watu katika Tarafa ya Loliondo na Kata mbili za Tarafa ya Sale (Malambo na Piyaya) ambazo zipo kwenye mgogoro zina jumla ya wakazi 66,496 kama inavyoonyeshwa katika grafu na mbili hapo juu.







| | Oloirien | Arash | Maaloni | Soitsambu | Oloipiri | Ololosokwan | Piyaya | Malambo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 5253 | 4161 | 2246 | 6062 | 2255 | 2658 | 2723 | 5445 |
| Wanawake | 5381 | 4630 | 2634 | 6221 | 2357 | 3693 | 3222 | 6555 |
| Idadi ya watu | 10,634 | 8,791 | 4,880 | 12,283 | 4,612 | 7,351 | 5,945 | 12,000 |


***Grafu 1.4:*** *Idadi ya watu kijinsia - Tarafa ya Loliondo na Sale*

### 1.3 Idadi ya Mifugo

Tarafa za Sale na Loliondo katika kata Nane zenye mgogoro zina jumla ya mifugo 973,745. Mifugo hii ni pamoja na kondoo, mbwa, mbuzi, nguruwe, kuku, punda, bata na ng'ombe.




***Grafu 1.5:*** *Idadi ya mifugo katika kata Nane za Tarafa ya Loliondo na Sale*



### 1.5 Malengo ya Taarifa

Taarifa hii ya Wananchi kutoka Tarafa za Sale na Loliondo ina dhamira ya dhati ya kutafuta fursa ya kutafuta suluhu ya kudumu ya mgogoro huu wa ardhi katika maeneo Vijiji yetu. Malengo mahusisi ni kama yafuatayo;

a) Kubainisha mifumo ya wafugaji wa asili juu ya milki, usimamizi na matumizi ya ardhi katika tarafa za Loliondo na Sale.
b) Kuchambua hadhi ya ardhi (Legal Status) ya vijiji katika kata Nane za Taraza za Sale na Loliondo.
c) Kubainisha chanzo na historia ya mgogoro wa Ardhi katika tarafa za Loliondo na Sale
d) Kuelimisha umma wa watanzania, viongozi wa Serikali na wadau wa uhifadhi, ardhi na maendeleo ya jamii kuhusiana na mgogoro wa tarafa za Loliondo na Sale ili kuweka rekodi ya taarifa sahihi na kuondoa upotoshwaji mkubwa unaofanywa na baadhi ya watu.
e) Kuchambua hoja za serikali kuhusu ardhi ya Vijiji vyenye mgogoro na kutoa maoni ya wananchi juu hali halisi ya hoja zeneyewe
f) Kutoa mapendekezo ya namna ya kusuluhisha mgogoro huo.

### 1.6 Muundo wa Taarifa

Taarifa hii imegawanyika katika sura kuu Tano, Sura ya kwanza inatoa maelezo kwa ufupi juu ya Wilaya ya Ngorogoro mahali ilipo, idadi ya watu, ukubwa wa wilaya. Katika sura hii pia taarifa za awali kuhusu eneo la Tarafa za Loliondo na Sale hasa mahali zilipo; idadi ya watu, mifugo na mfumo wa matumizi ya ardhi katika eneo la kilomita za mraba 1500. Malengo ya taarifa, mbinu na mchakato wote uliopitiwa katika kuandaa taarifa hii zimeainishwa katika sura hii.

Sura ya pili inazungumzia taarifa muhimu juu ya hadhi ya ardhi kisheria ya eneo la ardhi ya vijiji katika Tarafa za Loliondo na sale na hasa eneo lenye kilometa za mraba 1500 zenye mgogoro wa miaka 30 sasa. Pia sura hii itafafanua zaidi mabadiliko ya kisheria toka enzi kabla, wakati wa wakoloni hadi sasa na jinsi mabadiliko hayo yalivyochangia migogoro ya ardhi au kupunguza migogoro hiyo. Vile vile sura hii inafafanua sheria mbalimbali zikiwemo sheria za ardhi, Wanyamapori, sheria za serikali za mitaa, sheria ya mipango ya matumizi ya Ardhi, na pia matamko ya viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa na serikali kabla na baada ya uhuru. Sehemu hii pia inaonyesha mfumo wa asili wa usimamizi wa ardhi katika tarafa hizi kwa taratibu za mila za jamii yenyewe. Sura ya Tatu inaangazia kwa kina kupitia

fafanuzi mbalimbali juu ya historia ya mgogoro, chanzo chake, madhara yatokanayo pamoja na jitihada zilizochukuliwa katika kutatua mgogoro ndani tarafa za Loliondo na Sale. Sura ya Nne inaeleza na kuchambua kwa kina hoja ambazo zimekuwa zikiwasilishwa na upande wa Serikali juu ya eneo la Vijiji vya Tarafa za Loliondo na Sale lenye kilomita za mraba 1500 kwa nyakati na awamu tofauti za uongozi wa nchi. Sura ya Tano inatoa mapendekezo na maoni ya jamii juu ya jinsi gani mgogoro huu unavyoweza kushughulikiwa ili kufikia maridhiano baina ya serikali na wanavijiji. Mwisho kabisa sura hii inatoa hitimisho ya taarifa kwa kurejea na kutoa mwelekeo wa msingi juu ya taarifa.

### 1.7 Mchakato wa Upatikanaji wa Taarifa

Sehemu hii inaonyesha mbinu zilizotumika katika kukusanya, kuchakata na kuandaa taarifa kupitia Kamati maalumu ya jamii kutoka katika kata 8 iliyoundwa na wananchi kwa kuongozwa na Mh. Mbunge wa Wilaya Ngorongoro na Mwenyekiti wa CCM Wilaya kwa lengo la kuandaa mapendekezo ya utatuzi wa mgogoro huu wa ardhi katika eneo la Kilomita za mraba 1500. Kamati hii imeundwa na wajumbe zaidi ya 40[2] kutoka katika kata zote 8 wakiwemo Madiwani, viongozi wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Ngorongoro, wenyeviti wa vijiji, viongozi wa mila, wawakilishi wa Wanawake, vijana na wataalamu wa jamii kwa lengo la kuratibu mapendekezo ya wananchi.




***Picha 1.1***
*Sehemu ya Wajumbe wa Kamati ya Wananchi kutoka Tarafa za Loliondo na Sale wakiwa katika Mapitio ya rasimu ya Kwanza ya Taarifa.*

2 Kiambatanishi cha Wajumbe wa Kamati

Ili kuhakikisha kuwa taarifa na maoni ya wananchi yanakusanywa kwa upana na undani wake Kamati ilitumia mbinu mbalimbali zikiwemo;

a) Mikutano ya wananchi katika ngazi za vijiji na Kata
b) Mikutano jumuishi ya Kata mbalimbali



***Picha 1.2:*** *Sehemu ya Wananchi kutoka tarafa ya Loliondo na Sale katika Kikao cha pamoja kujadili mgogoro wa Ardhi*

c) Mikutano ya Wadau
d) Mikutano ya makundi mbalimbali kama viongozi mila, wanawake, madiwani
e) Kupitia nyaraka mbalimbali za serikali kabla na baada ya Uhuru
f) Kupitia machapisho mbalimbali kuhusiana na eneo lenye mgogoro
g) Kutembelea eneo lenye mgogoro kuthibitisha aina ya matumizi na kuona hali halisi.

**Jedwali 1. 2: Orodha ya mikutano ya ukusanyaji wa tarafa ya Loliondo na Sale**

| Na | Eneo | Tarehe | Aina ya Mkutano | Idadi ya watu |
|---|---|---|---|---|
| | Kijiji cha Ormanie | 29 March, 2022<br>2 Aprili, 2022 | kupitia maresho toka kamati ya mapendekezo ya Arusha | 545<br>707 |
| | Kijiji Piyaya | 15 Feb,2022<br>7 Aprili, 2022<br>19 Aprili, 2022 | Majadiliano ya mgogoro wa ardhi (1500 sqkm)<br>Kupokea mrejesho wa kikao cha Arusha Ms TCDC,<br>Kikao cha kujumuisha mapendekezo ya jamii | 295 |
| | Kijiji cha Arash | 15 Januari, 2022,<br>5 Februari, 2022<br>26 Februari, 2022<br>5 Marchi, 2022<br>19 Marchi, 2022 | Majadiliano na kutoa mapendekezo juu ya mapendekezo ya mgogoro wa km 1500 | 1516 |
| MS-TCDC-Arusha | | 3-4 Aprili, 2022 | Mapitio ya rasimu ya Kwanza ya Taarifa | 60 |
| | Lush Garden -Arusha | 24 Aprili, 2022 | Mapitio ya Rasimu ya pili ya Taarifa | 65 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kijiji cha Ormanie | 28 Aprili, 2022 | Mkutano Mkuu kuwasilisha na kupitia rasimu ya pili ya taarifa | 258 |
| | Malambo | Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 745 |
| | Madukani | Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 328 |
| | Kirtalo | Machi-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 373 |
| | Ololosokwan | March-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 652 |
| | Oloipiri | Machi-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 379 |
| | Maaloni | March-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 415 |
| | Mbuken | Machi-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 314 |



| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Loosoito | March-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 296 |
| | Olalaa | Machi-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 225 |
| | Engobereti | March-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 271 |
| | Oloiswashi | Machi-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 259 |
| | **Jumla** | | | **7,703** |

Baada ya Kikao cha tarehe 3-4 March Mjini Arusha, wawakilishi wa kamati toka Tarafa ya Loliondo, Sale na Ngorongoro walikwenda Dodoma na kuonana na Waziri Mkuu na kumpa taarifa ya mchakato wa kamati. Wawakilishi hawa walikuwa kumi na waliweza kueleza malengo ya taarifa hii inayoandaliwa na kamati.

### 1.8 Vikwazo katika ukusanyaji wa Taarifa

Katika ukusanyaji wa Taarifa hii kumekuwepo pia na vikawazo vilivyofanya maoni kuwa mgumu kupatikana. Baadhi ya changamoto zilizokwamisha ukusanyaji wa taarifa na uandishi wa taarifa hii ni pamoja;

(a) Viongozi wa kisiasa, wa kimila na watetezi wa haki za binadamu kukamatwa, kuitwa vituo vya polisi na kuhojiwa wakati zoezi hili la uandishi wa ripoti likiendelea.

**Jedwali 1.3: Baadhi ya Viongozi wa kisiasa, wa kimila na watetezi wa haki za binadamu walioendelea kukamatwa, kuitwa vituo vya polisi na kuhojiwa wakati wa zoezi la kukusanya maoni ya wananchi (Machi-Aprili 2022).**

| Na | Kiongozi | Kata/Kijiji | Cheo | Tarehe ya kukama-twa | Alikope-lekwa | Hali ya Shauri |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Joel Clemence | Malambo | Diwani | | Loliondo na Arusha | Bado anaendelea kuripoti kituo cha Polisi |
| | Motiko Risando | Malambo | Mwenyekiti wa Kijiji | | Loliondo | Bado anaendelea kuwasili kituo cha Polisi |
| | Simon Ndari | Malambo | Laigwanani | | Loliondo | Bado anaendelea kuripoti kituo cha Polisi |
| | John Kulinja | Malambo | Laigwanani | | Loliondo | Bado anaendelea kuripoti kituo cha Polisi |
| | Simon Ole Nairiamu | Piyaya | Diwani | | Loliondo | Bado anaendelea kuripoti kituo cha Polisi |
| | Moloimet Saing'eu | Ololosokwan | Diwani | | Loliondo | Bado anaendelea kuripoti kituo cha Polisi |
| | Ndirango Olesenge | Loliondo/ Orgosorok | Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ngorongoro | | | Bado anaendelea kuripoti kituo cha Polisi |
| | Mathew Siloma | Arash | Diwani | | Loliondo-Arusha | Bado anaendelea kuripoti kituo cha Polisi |
| | Mbeka Rago | Maaloni | Diwani | | Loliondo | Bado anaendelea kuripoti kituo cha Polisi |

b) Kukosekana kwa barua rasmi kutoka kwa Waziri Mkuu/Serikali ya kutambua mchakato huu wa kuandaa taarifa ya mapendekezo. Kazi hii imefanyika kwa mazungumzo ya mdomo zaidi kati ya Waziri Mkuu , Mbunge na viongozi wa kamati hii ya mapendekezo .

(c) Vyombo vya habari kuendelea kupotosha mchakato huu na kuchangia kukosekana kwa taarifa halisi

(d) Muda mchache wa kukusanya taarifa

(e) Ukubwa wa mikutano ya jamii wakati wa kutoa maoni umechangia pia kushindwa kuweka kumbukumbu nzuri za mikutano hasa mahudhurio

(f) Ufinyu wa rasilimali fedha wakati wa ukusanyaji, uandishi na uhakiki wa taarifa hii

## SURA YA PILI

# HADHI YA ARDHI YA VIJIJI VYA TARAFA ZA SALE NA LOLIONDO KISHERIA

## 2.0 UTANGULIZI

Sura hii imejikita zaidi katika kuelezea hadhi ya kisheria (Legal Status) ya eneo la ardhi ya vijiji katika Tarafa za Loliondo na Sale hasa eneo lenye kilometa za mraba 4000 zenye mgogoro wa miaka 30 sasa. Itafafanua zaidi mabadiliko ya kisheria toka enzi za wakoloni hadi sasa na jinsi mabadiliko hayo yalivyochangia migogoro ya ardhi au kupunguza migogoro hiyo. Vile vile sura hii inafafanua sheria mbalimbali zikiwemo sheria za ardhi, Wanyamapori, sheria za serikali za mitaa, na sheria ya mipango ya matumizi ya Ardhi, na pia matamko ya viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa na serikali kabla na baada ya uhuru.  Sehemu hii pia inaonyesha mfumo wa asili wa usimamizi wa ardhi katika tarafa hizi kwa taratibu za mila za jamii yenyewe.

### 2.1 Historia ya Utawala na Usimamizi wa Ardhi

Eneo hili linachambua historia ya umiliki wa ardhi kwa jamii za kimasai hasa eneo la Loliondo na Sale kabla ya ujio wa wakoloni, wakati wa wakoloni na baada ya uhuru.

### 2.1.1 Utawala wa Ardhi kabla ya Wakoloni

Mfumo wa umilikaji wa ardhi kabla ya utawala wa kikoloni ulikuwa ni wa kimila. Ardhi yote ilikuwa "ikimilikiwa" kimila na koo na makabila mbalimbali kwa taratibu za koo na makabila husika. Hapa msisitizo unawekwa kwenye aina ya umiliki yaani kimila na kwa taratibu za koo husika. Dhana ya "kumiliki" ardhi kwa wakati huo ilikuwa ni MATUMIZI, yaani mtu alipata/aligawiwa ardhi ili aitumie kwa matumizi mbalimbali ya ardhi kama ufugaji na kilimo na wala si kwa nia au sababu nyingine Wananchi (wamiliki) walikuwa na sauti ya mwisho katika ardhi yao, waliweza kumiliki, kutumia na kugawa ardhi

kadri walivyoona inafaa. Viongozi wa mila na jadi ndio walikuwa waangalizi na wasimamizi wa ardhi ya familia na ukoo na ndio walikuwa uwasilishaji wa migogoro pale ilipojitokeza. Maandiko mengi yanaonyesha kuwa kwa muda mrefu toka kabla na enzi za Wakoloni wa Kijerumani wafugaji wa kimasai wamekuwepo katika maeneo ya Loliondo na Sale na wakitumia rasilimali ardhi kwa sheria za kimila (Deemed Customary Rights of Occupancy).


### 2.1.2 Usimamizi wa Ardhi wakati wa Utawala wa Wajerumani 1886-1918

Baada ya Mkutano wa Berlin nchini Ujerumani uliofanyika mwaka 1884 ambayo agenda yake kubwa ilikuwa ni wakoloni kugawana makoloni ya Bara la Africa na kuondoa migogoro baina yao juu ya utawala wa bara hili, Ujeremani ilikabidhiwa Tanganyika kuwa koloni lake kati ya makoloni mengine aliyokuwa nayo. Na kabla ya wakoloni wa Kijerumani ardhi yote ya Tanganyika ilikuwa inasimamiwa na sheria za kimila kwa mujibu wa taratibu za kila kabila na hivyo Wajerumani baada ya kuingia Tanganyika waliweka ardhi yote chini ya utaratibu wao. Kwa upande wao alianzisha utaratibu wao wa kumiliki maeneo yenye rutuba kwa ajili ya kuanzisha mashamba makubwa (Plantations).

Wajerumani walitunga sheria iliyomilikisha himaya ya Kijerumani ardhi ya Watanzania (Imperial Decree" Regarding Creation, Acquisition, Conveyance of Crown Land in 1895). Sheria hii iliwapa nguvu wajerumani ya kumiliki na kutumia ardhi yote ya watanganyika. Sheria hii ilifanya ardhi ya Tanganyika kuwa chini ya himaya ya Kijerumani (German Crown Empire) na yoyote aliyetaka ardhi ni sharti apewe na governor wa kijerumani. Wafugaji hawakuwa wakifanya shughuli za kilimo na badala yake walijikita kwenye shughuli za ufugaji ambayo haikuwa na madhara ya uharibifu wa ardhi.

### 2.1.3 Usimamizi wa Ardhi wakati wa Utawala wa Waingereza 1919-1961

Utawala wa Kijerumani ulianguka baada ya vita kuu ya kwanza ya Dunia 1918. Makoloni yote yaliyokuwa chini ya Wajerumani yaligawanywa kwa wakoloni wengine haswa walioshinda vita husika. Tanganyika kama baadhi ya makoloni mengine ilikabidhiwa kwa Waingereza na Umoja wa Mataifa. Mwaka 1923, utawala wa waingereza baada ya kuingia na kujiimarisha ulipitisha Sheria ya Ardhi, 1923. Sheria hii ilianzisha utaratibu wa kumilikisha ardhi (rights of occupancy). Lakini baadae ili kulinda haki za watanganyika na wazawa kumiliki ardhi kimila, mwaka 1928 dhana ya umiliki ardhi ilipanuliwa na kutambua milki ya ardhi kimila kuwa sehemu ya sheria za ardhi. Kwa maana hiyo maeneo yote ya Sale na Loliondo hadi Ngorongoro yalikuwa yanamilikiwa kihalali kwa taratibu za kimila.




***Ramani 2.1:*** *Matumizi ya Ardhi Kabla ya Mwaka 1958*


Pamoja na kutungwa kwa sheria mpya ya Ardhi wakati huo wa utawala wa waingereza ni wakati huo pia zilitungwa sheria zinazo husiana na usimamizi, ulinzi wa wanyama pori na uhifadhi:[3]. Baadhi ya sheria za uhifadhi zilizotungwa wakati wa Uingereza zimefafanuliwa katika sura zinazofuata. Ingawa wakoloni walitunga sheria mbalimbali za uhifadhi wa wanyamapori ikiwa ni pamoja na sheria ya mwaka 1948, iliyo anzisha Hifadhi ya Serengeti. Sheria hii ndiyo iliyokuwa na madhara makubwa kwa jamii ya wafugaji toka Tarafa ya Loliondo na Ngorongoro. Sheria hii iliwaondoa wafugaji kutoka Serengeti na kusababisha wafugaji hao kuhamia na kuungana na wafugaji wenzao katika maeneo ya Ngorongoro na Loliondo mwaka 1959. Sheria zingine zilizoanzishwa kipindi hicho zililenga kusimamia uhifadhi wa wanyama pori na sio za milki ya ardhi.

3 Neumann, RP 2000, 'Land, justice, and the politics of conservation in Tanzania', in Zerner C (ed), People, plants, and justice: the politics of nature conservation, Columbia University Press, New York, pp. 117–143., Neumann, RP 1998, Imposing wilderness: struggles over livelihood and nature preservation in Africa, University of California Press, Berkeley and Los Angeles, Neumann, RP 1995a, 'Ways of seeing Africa: colonial recasting of African society and landscape in Serengeti National Park', Ecumene, vol. 2, pp. 149169. And Neumann, RP 1995b, 'Local challenges to global agendas: conservation, economic liberalization and the pastoralists rights movement in Tanzania', Antipode, vol. 27, no. 4, pp. 363382.

### 2.1.4 Utawala na Usimamizi wa Ardhi baada ya Uhuru 1961-1989

Baada ya kupata uhuru, sheria ya Ardhi ya 1923, ilifanyiwa marekebisho ili kukidhi matakwa ya wakati wa Serikali ya Tanganyika huru. Moja ya marekebisho yaliyofanywa ni kuondoa neno Gavana kwenye sheria hiyo ya kikoloni na kuandika neno RAIS. Mara baada ya kupata uhuru, serikali ya Tanganyika ilibadili mfumo wa umiliki wa ardhi kutoka milki wa moja kwa moja usio na ukomo (Freeholds) kwenda umiliki wa ardhi kwa vipindi maaulum (Leaseholds) vya 33, 66 na 99. Ardhi yote ikawa ardhi ya umma chini Rais, na Rais akapewa mamlaka/dhamana ya kusimamia ardhi yote kwa niaba ya watanzania.

Pamoja na kwamba hakukuwa na mabadiliko makubwa katika sheria ya ardhi, baada ya Uhuru, ila kulikuwa na mabadiliko katika dhana ya utwaaji wa ardhi ambapo sheria ya utwaaji wa Ardhi[4] ilitungwa ili kutoa mamlaka kwa Rais kuweza kurudisha ardhi iliyokuwa chini au mikononi mwa watu binafsi kuwa chini ya umma au kubadilisha matumizi ya ardhi. Mabadiliko haya yalienda sambamba na Azimio la Arusha[5] na hivyo mabadiliko ya sheria hii ilikuwa moja ya nyenzo ya utekelezaji wa Azimio la Arusha. Wakati huo hakuna mabadiliko yoyote ya sheria ya ardhi, hivyo ardhi yote ya mila ilibakia kuwa mikononi mwa jamii, hivyo kwa upande wa Ardhi za Tarafa ya Loliondo na Sale umilikaji na matumizi ya ardhi yaliendelea kuwa chini ya wananchi wenyeji ambapo kwa upande wa tarafa hizi ni wafugaji.




**Ramani 2.2:** *Matumizi ya Ardhi Baada ya 1958*

4 Na. 47 ya 1967
5 Tarehe 5 mwezi wa 2 mwaka, 1967

Wakati wote wa Azimio la Arusha la 1967 na baada ya hapo serikali iliendelea na jitihada mbalimbali hasa katika ujenzi wa uchumi na kuwaleta watu pamoja kwa kile kilichokuwa kinatajwa kuwa ni kurahisisha maendeleo. Na hadi kufikia miaka ya 1970 serikali ilikuja na Sera ya Ujamaa na Kujitegemea. Lengo kuu la Azimio la Arusha pamoja na malengo mengine ilikuwa na lengo la kurudisha misingi ya uzalishaji mali mikononi mwa umma.

Ni muhimu kusisitiza pia kwamba kipindi hiki ndicho kilichokuwa na nyakati za utwaaji wa ardhi za Wafugaji hasa kwa maeneo ya Hanang (1970-1990) na Loliondo - (Breweries Ltd  - 1984) ambapo maeneo makubwa ya nyanda za malisho yaliweza kutwaliwa na kuwa sehemu ya mashamba ya serikali na ranchi za taifa maarufu kama NAFCO na NARCO na kupelekea kufunguliwa kwa kesi nyingi za kupinga utwaaji huo wa ardhi ya wafugali kama vile Mulbadaw Village Council and 67 Others vs. NAFCO[6], Yoke Gwaku and 5 Others vs. Gawal Farms Limited and NAFCO[7] na Isata Ndekerei & 14 others vs. Tanzania Breweries Limited Farms[8], kwa upande wa Loliondo.

Pamoja na kwamba uanzishwaji wa mashamba haya yalikuwa kwa ajili ya serikali, lakini baadaye yalikuja kubinafsishwa/kuuzwa kwa makampuni binafsi kwa mfano shamba la Sukenya Na. 373 lenye ekari 12,617 iliuzwa kwa kampuni tanzu ya Thomson Safari inayojulikana kama Tanzania Conservation Limited (TCL) mwaka 2006 na kupelekea wananchi wa Vijiji Vitatu vya (Mondorosi, Sukenya and Soit Sambu) kufungua kesi ya ardhi Na. 26 ya 2013[9] kwa ajili ya kudai ardhi hiyo ya Vijiji.

Vile vile Kijiji cha Ololosokwan kilifungua kesi ya Ololosokwan Village Council vs. Tanzania Cattle Products and Conscorp Tanzania Limited[10], juu ya ardhi ya Kijiji yenye ukubwa wa hekari 25,000. Pande zote ziliamua kufanya makubaliano ya usuluhishi wa mgogoro nje ya Mahakama na kupelekea baadaye kusaini makubaliano ya uwekezaji katika eneo hilo[11]. Katika jitihada na harakati hizo za ulinzi wa ardhi ya wananchi, Kijiji cha Ololosokwan mwaka 2011 kilifungua kesi upya ya Ololosokwan Village Council vs. Tanzania Cattle Products and Andbeyond Tanzania Ltd,[12] baada ya kugundua kuwa kampuni ya Tanzania Cattle products ambayo iliridhiwa na Andbeyond ilipata hati ya kumiliki ardhi Na.9990 kwa njia ya udanganyifu, ambapo 2012, walikubali kumaliza mgogoro nje ya mahakama na kurudisha (surrender) hati hiyo.

6 (1984) T.L.R. p. 15-27 HC-Arusha
7 Civil Case No. 52 of 1988 HC-Arusha (unreported)
8 Magistrate Court of Arusha Case No. 74 of 1987
9 Mondorosi Village Council, Sukenya Village Council and Soit Sambu village Council Vs. Tanzania breweries LTD, Tanzania Conservation LTD, Ngorongoro District Council, The Commissioner for Lands and Attorney general (HC-Arusha) Land Case No. 26 of 2013
10 Civil Case No. 31 of 1994.
11 Tarehe 26/10/1999, Agreement between Ololosokwan Village Council and Conscorp Tanzania Limited (CC Africa), see Annex 2
12 Land Case No. 15 of 2011 (HC-Arusha)

### 2.1.5 Uanzishwaji wa Wilaya Ngorongoro na Usajili wa Vijiji

Baada ya Uhuru serikali iliendeleza mfumo wa utawala ambapo wilaya na Vijiji viliendelea kuwa sehemu ya utawala wa Serikali za Mitaa ambapo eneo la wilaya Ngorongoro ilikuwa chini ya utawala wa Wilaya ya Maasai. Wilaya ya Maasai ilijumuisha Wilaya za sasa za Kiteto, Simanjiro, Monduli, Longido na Ngorongoro na makao makuu ya wilaya ikiwa ni Monduli. Baadaye mwaka 1979, Wilaya mpya ya Ngorongoro ilianzishwa ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

Ikumbukwe kwamba kabla ya uanzishwaji wa Wilaya Ngorongoro, wananchi katika tarafa za Loliondo na Sale walikuwa wakiishi na kumiliki ardhi katika vijiji vyao vilivyosajiliwa ndani ya iliyokuwa Wilaya ya Maasai. Baadhi ya vijiji katika tarafa vilisajiliwa kabla ya kuanzishwa kwa Wilaya mpya ya Ngorongoro ni kama zinavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini na kiambatanisho namba 1[13] na 2.

**Jedwali 2. 1:Baadhi ya Vijiji Vilivyo Sajiliwa mwaka 1978 katika Tarafa za Loliondo na Sale**

| Na | Jina la Kijiji | Tarehe ya Kuandikishwa | Namba ya Hati ya Usajili |
|---|---|---|---|
| 1 | Malambo | 28 Februari, 1978 | AR.KIJ.372 |
| 2 | Piyaya | 15 Aprili, 1978 | AR.KIJ.431 |
| 3 | Arash | 8 Septemba, 1978 | AR.KIJ.405 |
| 4 | Oloosoito/Maaloni | 8 Septemba, 1978 | AR.KIJ.406 |
| 5 | Oloirien/Magaiduru | 8 Septemba, 1978 | AR.KIJ.407 |
| 6 | Soitsambu | 8 Septemba, 1978 | AR.KIJ.402 |
| 7 | Ololosokwan | 15 Aprili, 1978 | AR.KIJ.403 |

### 2.1.6 Utawala na Usimamizi wa Ardhi Kuanzia Mwaka 1990- 2022

Sehemu hii n inaachambua na kufafanua umiliki wa ardhi za kifugaji mara baada ya kuingia katika mfumo wa soko huria na pia wakati Tanzania ilipoanza kufanya mabadiliko au maboresho ya sheria za ardhi hapa Tanzania. Eneo hili linachambua umiliki wa ardhi ya vijiji na ardhi za vijiji kwa taratibu za kimila lakini chini ya sheria na sera mpya za ardhi.

13 Kiambatanisho Na. 1

### 2.1.6.1 Upimaji wa Vijiji na Kupata Hati/Vyeti vya kumiliki Ardhi

Kipindi hiki itakumbukwa kuwa kulikuwa na jitihada za mageuzi makubwa ya upimaji wa Vijiji vya wafugaji katika Tarafa za Loliondo na Sale kwa kupitia viongozi wa Vijiji, Kata, wilaya na mashirika ya kiraia ambapo vijiji mbalimbali vilipimwa na kupata Hati za kumiliki ardhi katika Vijiji vyao. Mchakato huu ulisimamiwa na Halmashauri ya wilaya ya Ngorongoro kwa msaada wa mashirika ya KIPOC na ADDO. Jumla ya ardhi ya vijiji vyenye ukubwa wa Hekta 346,672 za tarafa ya Loliondo vilipimwa na kupatiwa hati za umiliki wa ardhi, baadhi ya vijiji ni pamoja na Arash, Loosoito/Maaloni, Olorien/ Magaidur, Oloipiri, Soitsambu na Ololosokwan, kwa mujibu wa sheria ya ardhi ya mwaka 1923.[14]

**Jedwali 2. 2:Vijiji vilipimwa na kuwa Hati Miliki za Ardhi**

| NA. | JINA LA KIJIJI | NAMBA HATI | TAREHE | NAMBA YA CHETI | TAREHE | UKUBWA WA ARDHI (HEKTA) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Arash | 7264 | 13.10.1990 | | | 66,800 |
| 2 | Oloosoito/ Maaloni | 7259 | 13.10.1990 | | | 77,860 |
| 3 | Oloirien/ Magaiduru | | 13.10.1990 | | | 30,340 |
| 4 | Oloipiri | 7182 | 13.10.1990 | | | 47,100 |
| 5 | Soitsambu | 7275 | 13.10.1990 | | | 73,342 |
| 6 | Ololosokwan | 7262 | 13.10.1990 | 1NGR | 26.01.2006 | 51,230 |
| | Jumla ya Hekta | | | | | 346,672 |

### 2.1.6.2 Tume ya Rais ya Uchunguzi wa Masuala ya Ardhi -1991


Kutokana na migogoro mingi iliyoibuka katika nchi yetu kuanzia miaka 1970s-1990s Rais wa wakati huo Mh. Alli Hassan Mwinyi, mwaka 1991 aliunda tume iliyongozwa na Prof Issa Shivji ili kuchunguza vyanzo vya migogoro ya ardhi[15]. Tume ilizinguka nchi nzima kukusanya maoni ya wananchi na hatimaye kuandika taarifa na kuwasilisha mapendekezo kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ifahamike kuwa kabla ya tume hiyo sheria ya ardhi iliyokuwa inatumika ni ya Kikoloni ya mwaka 1923 na hivyo mapendekezo ya taarifa ya tume ni pamoja na kutunga Sheria mpya za Ardhi ambazo zinatokana na maoni ya watanzania ili kukidhi matakwa na maslahi ya wananchi.

14 Kiambatanisho Na.2
15 Ministry of Lands, Housing and Urban Development & Scandinavia Institute of African Studies (1994) Report of the Presidential Commission of Inquiry into Land matters, Vol. I

Baadhi ya mapendekezo ya tume ni pamoja na kuingiza suala la ardhi katika katiba ili kulipa ulinzi wa uhakika, kuondoa milki ya hatma mikononi mwa Rais, kugawa ardhi katika makundi ya ardhi ya kijiji, ya hifadhi na ardhi ya jumla, kuunda mfumo wa usuluhishi na utatuzi wa migogoro ya ardhi, kutungwa kwa sera na sheria ya ardhi inayobainisha mahitaji na maslahi ya makundi mbalimbali ya kijamii na kufafanua majukumu ya dola na wadau wengine katika ardhi. Ifahamike kuwa Tume ya uchunguzi ya masuala ya ardhi ya Prof Issa Shivji, ilitembelea Loliondo, kuchunguza migogoro ya Ardhi baina ya wafugaji na makampuni yaliyopora ardhi au wawekezaji zikiwepo mashamba binafsi.

### 2.1.6.3 Sera ya Taifa ya Ardhi na Sheria za ardhi za 1999

Sera ya Taifa ya Ardhi[16] na Sheria mpya za ardhi za 1999 ni matokeo ya mapendekezo ya Tume ya Rais ya Masuala ya Ardhi. Baada ya mawasilisho ya mapendekezo ya Tume, serikali ilitunga Sera Mpya ya ardhi ya 1995, na miaka mitatu baadaye yaani 1999, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga na kupitisha Sheria mbili za ardhi yaani, sheria ya Ardhi[17] na Sheria ya Ardhi ya Vijiji.[18] Sera ya Ardhi ilisisitiza kuhusu maeneo ya nyanda za malisho na kuelekeza utaratibu wa kuyatunza na kuyalinda uanzishwe kisheria ambapo maeneo yote ya wafugaji yanayotumika kwa ajili ya nyanda za malisho kama ilivyo eneo la Vijiji la kilometa za mraba 1500 la Loliondo na Sale.



7.3.0 RANGELANDS AND LIVESTOCK KEEPING:

There are growing social conflicts, environmental concerns and land use conflicts due to haphazard alienation of rangeland for large scale agriculture. These extensive alienations frequently disown pastoralists of their grazing lands.

7.3.1 Policy Statements:

(i) Security of tenure for pastoralists in pastoral land areas will be guaranteed by appropriate measures including gazetting to protect grazing land from encroachment.

(ii) Certificates of Village Land will be issued to protect common property regimes.


(iii) Underutilized or neglected former pasture land will be reclaimed and restored to pastoralists, when not in conflict with national interests.

(iv) When any activity other than pastoralism ceases in rangelands (eg. abandoned ranch) that land will revert to its original land use.

***Picha 2.1:*** *Lengo na Tamko la Saera ya Ardhi kuhusu Nyanda za Malisho kwa Wafugaji*

16 1995
17 Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999
18 Sheria ya Ardhi Na. 5 ya mwaka 1999

Sheria Namba 4 ya Ardhi hutumika kusimamia Ardhi ya jumla hasa maeneo ya mijini na Vijijini pale ambapo kuna ardhi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria Na. 4 ya Ardhi ya 1999, zikiwemo ardhi za uwekezaji na hivyo sheria hii ipo chini ya usimamizi wa Kamishina wa Ardhi. Sheria ya ardhi ya Vijiji imepeleka mamlaka ya maamuzi ya ardhi kwenye mikutano mikuu ya Vijiji ili kudhibiti utoaji holela wa Ardhi iliyokuwa ikitekelezwa na Halmashauri za vijiji bila ridhaa ya wananchi ambapo ilisababisha migogoro mikubwa katika maeneo yote nchini.





***Ramani 2.3:*** *Matumizi ya sasa ya ardhi katika tarafa za Loliondo na Sale*

Kwa mujibu wa Sheria ya ardhi ya Vijiji Halmashauri za Vijiji kwa kushirikiana na mikutano mikuu zimepewa mamlaka ya kupima ardhi ya Vijiji na kufanya mipango ya matumizi ya ardhi ambapo, wanapangilia matumizi yote ya ardhi ya kijiji kulingana na mahitaji na matakwa ya wananchi. Vilevile

Sheria ya Mipango ya matumizi ya Ardhi[19] inatambua halmashauri za Vijiji kama moja ya Mamlaka ya upangaji wa matumizi ya ardhi katika ngazi ya Kijiji kwa kushirikiana na Timu ya wilaya ya upangaji wa matumizi ya ardhi (PLUM) ambayo jukumu lake kubwa ni kushauri na kusaidia katika masuala ya utaalamu na si kufanya maamuzi katika upangaji wa matumizi ya ardhi ya Vijiji.


Mfano kwa upande wa Tarafa ya Loliondo na Sale, Vijiji vya Ololosokwan na Engaresero viliweza kurejewa kupimwa upya na kupata vyeti vya ardhi vya vijiji na kufanya mipango ya matumizi ya ardhi. Mpango huu wa Engaresero wa 2016 ni marejeo ya mpango wa 2008 wa matumizi bora ya ardhi. Kijiji cha Ololosokwan nacho kama inavyoonekana kwenye ramani kina mpango kina mpango wa matumizi ya ardhi toka mwaka 2008.




***Ramani 2.4:*** *Ramani ya matumizi ya ardhi ya Kijiji cha Engaresero 2016-2026*

***Chanzo:*** *Kijiji cha Engaresero, 2016*

19 Sheria Na. 6 ya 2007




***Ramani 2.5:*** *Ramani ya matumizi ya Ardhi ya Kijiji cha Ololosokwan 2008Chanzo: Kijiji cha Ololosokwan, 2008*

### 2.1.6.4 Hadhi/Uhalali wa Hati za Ardhi za Vijiji kisheria

Sheria ya Ardhi ya mwaka 1923 katika kifungu cha 9, kilimpa mamlaka Mkurugenzi wa Huduma za Maendeleo ya Ardhi kutoa hati za kumiliki ardhi za Vijiji. Sheria Mpya za Ardhi za mwaka 1999, vinaruhusu utoaji wa Vyeti vya ardhi vya Vijiji tofauti na hati za ardhi zilizotolewa kwa Vijiji kwa mujibu wa Sheria ya ardhi ya mwaka 1923,iliyofanyiwa marekebisho mara kadhaa baada ya uhuru. Vilevile Sheria hizo za ardhi zimeendelea kutambua hati hizo ambapo imeainishwa katika vifungu mbalimbali vya Sheria ya ardhi

ya Vijiji Na.5 ya mwaka 1999, kuanzia kwenye tafsiri ya maana ya ardhi ya Vijiji. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Kijiji kifungu cha 7 (1), Ardhi ya Kijiji inajumuisha:

- Ardhi yote iliyoko ndani ya mipaka ya Kijiji kilicho sajiliwa kwa mujibu wa kifungu 22 cha Sheria ya Serikali za Mitaa [Mamlaka za wilaya] Na. 7 ya Mwaka 1982
- Ardhi iliyotengwa kama ardhi ya kijiji kwa mujibu wa Sheria za uanzishwaji na makazi ya Vijiji ya Mwaka 1965
- Ardhi ambayo imewekewa mipaka kama Kijiji kwa sheria mbalimbali za kiutawala kabla ya kutungwa kwa sheria za ardhi za 1999 au kwa mujibu wa mifumo na misingi ya kupokea au ya kimila inayotumika Tanzania.
- Kutungwa kwa sheria za ardhi wanavijiji walikuwa wanatumia kama ardhi ya vijiji kwa matumizi mbalimbali ikiwemo shughuli za ufugaji kwa miaka 12 kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria.

Kifungu cha 7 (12) cha sheria ya ardhi ya Vijiji inatambua hati zote za milki ya ardhi ya Vijiji vilivyotolewa kwa mujibu wa sheria zingine kabla ya kutungwa kwa sheria hiyo[20]. Hivyo kwa mujibu wa vifungu hivyo vya sheria ya Ardhi ya Vijiji ya 1999, Vijiji vyote vya tarafa za Loliondo na Sale vilivyosajiliwa kwa Mujibu wa Sheria ya Serikali za mitaa [Mamlaka za wilaya] Na. 7 ya 1982 na kupata hati za kumiliki ardhi ni halali na vinaendelea kutambulika kisheria. Aidha ni dhahiri kuwa hatua ya Serikali ya kumega ardhi ya Vijiji kiasi cha kilomita za mraba 1,500 inavunja Ibara ya 24 ya katiba ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania[21] na sheria za ardhi badala ya kutimiza jukumu lake la kusimamia utekelezaji wake.


### 2.1.5.5 Sheria Ndogo za Vijiji

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kama ilivyo rekebishwa mara kwa mara, katika Ibara ya 145 (1) inasema “Kutakuwa na vyombo vya Serikali za Mitaa katika kila Mkoa, Wilaya, mji, na kijiji, Katika Jamhuri ya Muungano, ambavyo vitakuwa vya aina na majina yatakayowekwa na Sheria iliyotungwa na Bunge au na Baraza la Wawakilishi”. Ibara ya 145 (2) “Bunge au Baraza la Wawakilishi, Kadri itakavyokuwa, litatunga Sheria itakayofafanua utaratibu wa Kuanzisha vyombo vya serikali za Mitaa, miundo

20 Village Land Act, section 7 (12) that, A certificate or other document of registration issued to any village registered under the provisions of section 22 of the Local Government (District Authorities) Act Cap. 287* shall, where the Ministry responsible for Lands approves that it satisfies the conditions for the grant of certificate of village land, have the same effect and force as regards village land as a certificate of village land issued to a village under this section.
21 1977, Kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara.

na wajumbe wake, njia za mapato na utaratibu wa utekelezaji wa shughuli za vyombo hivyo". Tafsiri ya ibara hii katika uanzishwaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo ni pamoja na Halmashauri za Vijiji inaonyesha chimbuko la mamlaka ya Vijiji kuwa Katiba ya nchi[22], na pili ibara hii inaagiza bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutunga sheria zitakazo wezesha mamlaka hizo za serikali za Mitaa kutunga sheria ndogo ili kuwezesha utekelezaji na usimamizi rasilimali za wananchi katika maeneo ya Vijiji.

Kwa msingi huo wa Ibara ya katiba tajwa; bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitunga sheria ya Serikali za Mitaa [Mamlaka za wilaya] Na. 7 ya mwaka 1982, ambayo katika kifungu cha 168 inaruhusu Vijiji kutunga sheria ndogo ili kurahisisha usimamizi wa rasilimali na uendeshaji wa shughuli za vijiji. Katika kutekeleza matakwa ya Katiba na Sheria, vijiji katika Tarafa za Loliondo na Sale zilitunga na kutekeleza sheria ndogo za vijiji[23] ambazo zimewezesha kwa kiwango cha juu usimamizi na utunzaji wa rasilimali asili. Sheria hizi zinaainisha mipango mbalimbali za wananchi katika utawala, usimamizi na ulinzi wa ardhi ambayo imeendelea kuvamiwa na kuporwa kwa kiasi kikubwa kwa sababu ya ubora wake. [24]




***Ramani 2.6:*** *Usimamizi wa nyanda za malisho kijiji cha Ololosokwan kwa kutumia sheria Ndogo za Kijiji za 2000, kwa nyakati za kiangazi na masika*

*Chanzo: Kijiji cha Ololosokwan*

22 Kiambanisho Na. 3
23 Sheria Ndogo za vijiji vya Malambo, Ololosokwan, Olosoito/Maaloni, Oloipiri, Soitsambu na Engaresero
24 Ripoti ya TNRF, Integrating Pastoralist Livelihoods and Wildlife Conservation? Options for Land Use and Conflict Resolution in Loliondo Division, Ngorongoro District February 2011 https://www.tnrf.org/files/Integrating%20Pastoralist%20Livelihoods%20and%20Wildlife%20Conservation_FINAL_FINAL.pdf, imerejewa tarehe 4/5/2022.

## 2.2 Historia ya Sheria za Wanyamapori

Sura hii inachambua sheria za uhifadhi wa wanyamapori wakati wa ukoloni na baada ya huru na madhara yake kwa ardhi ya wafugaji wa kimasai. Uwepo wa mapori ya wanyama katika eneo la Sale na Loliondo ulikuwa ni wa muda mrefu toka miaka ya wakoloni wa Kijerumani hadi wakoloni wa Kingereza. Ilipofika miaka ya 1930, Serikali ya kikoloni ya Waingereza waliona umuhimu wa kuanza kutunga sheria za kulinda maeneo ya wanyama pori hapa nchini na pia kuweka utaratibu wa kisheria wa kufanya shughuli za kiwindaji. Kwa miaka yote hiyo ya nyuma wakati wa ukoloni mapori haya ya Loliondo na Sale yalikuwa katika maeneo ya wananchi yanayomilikiwa kisheria kama ilivyofafanuliwa hapo juu kwa lengo la kulinda na kuratibu shughuli za Wanyama pekee.

### 2.2.1 Sheria za Hifadhi wakati wa Utawala wa Wakoloni 1885-1959

Jitihada za kutaka kuanzisha maeneo ya uhifadhi na mapori tengefu kisheria zilianza rasmi na Wajerumani mwanzoni mwa karne ya 20. Mikakati yote hii zilijaribu kwa kiasi fulani kutambua umiliki wa kimila wa ardhi wa jamii asili. Mikakati hii kwa maeneo mengi ya Afrika Mashariki zilianzisha taratibu za kuweka mazingira ya jamii ya wamasai kuanza kusumbuliwa katika maeneo yao. Pamoja na kwamba ardhi ya wamasai Tanzania haikukaliwa na wakoloni, tishio kubwa lilikuja kuwa badaye ni taratibu za kisheria za uhifadhi wa rasilimali asili na mbuga za Wanyama kuanza kupewa kipaumbele na serikali za wakoloni.

Himaya ya Wajerumani (German East Africa ) ilianza kuweka mikakati ya kumiliki maeneo kuanzia mwaka 1885 hadi 19914 walipovamiwa na kuondolewa na Waingereza. Mfano mwanzoni mwa karne ya 20, Wajerumani walianzisha Sheria ya kusimamia Wanyama Pori iitwayo Game Preservation Ordinance ya mwaka 1908 hadi 1911.[25] Baadaye baada ya vita ya kwanza ya Dunia Waingereza walikuja na kutunga sheria ziingine nyingi baada ya vikao huko Waingereza kuamua kulinda Wanyama na maeneo yao kama ifuatavyo zenye kulenga kwenye usimamizi wa wanyama pori na uhifadhi:[26]

(i) Kuanzishwa kwa Idara ya Wanyamapori (Tanganyika Game Department in 1919)

(ii) Sheria ya Wanyamapori (The Game Preservation Ordinance 1921) iliyoanzisha pia Pori la Akiba la Serengeti kwa wakati huo wa 1929.

25 Ojalammi, S. (2006). Contested lands: Land disputes in semi-arid parts of northern Tanzania. PhD Thesis, University of Helsinki, Finland. Available at: http://ethesis.helsinki.fi/julkaisut/mat/maant/vk/ojalammi/conteste.pdf

26 Neumann, RP 2000, 'Land, justice, and the politics of conservation in Tanzania', in Zerner C (ed), People, plants, and justice: the politics of nature conservation, Columbia University Press, New York, pp. 117–143.

(iii) Sheria ya Ardhi ( Land Ordinance 1923 )

(iv) Sheria mpya ya wanyamapori ( New Game Ordinance ya 1948), Sheria hii ndiyo iliokuja na utaratibu wa kuanzishwa Hifadhi ya Serengeti (Serengeti National Park).[27] Hii ndiyo sheria ya kwanza iliyoanza kuleta maumivu makubwa hasa kwa ardhi za Wamasai waliokuwa wanaishi Serengeti, Ngorongoro na Loliondo. Mwaka 1959 Kutokana na sheria hii, Wamasai wakaondolewa maeneo ya Serengeti ya Mwaka 1959 na kuamishiwa maeneo ya Ngorongoro na Loliondo na kuungana na ndugu zao wengine.

(v) Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ya 1959- Sheria hii ilianzishwa na watawala kwa kikoloni ili kuhifadhi eneo la Ngorongoro na pia kuwalinda na kuendeleza jamii ya wamasai walikuwepo na waliohamishiwa eneo la Ngorongoro kupisha uanzishwaji wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

### 2.2.2 Sheria za Uhifadhi Baada ya Uhuru

Sura hii ndogo inachambua sheria za uhifadhi na usimamizi wa Wanyama pori zilizotungwa baada ya uhuru. Eneo hili linatizama haki za wafugaji kumiliki ziliadhirika kwa kiasi gani kwa ujio wa sheria hizi. Eneo hili linasaidia kujua hadhi ya kisheria ya maeneo ambayo sheria za uhifadhi na usimamizi wa Wanyama pori zilitungwa na kutumika. Katika sura hii ndogo Sheria ya Wanyama Pori ya 1974, pamoja na Sheria Mpya ya 2009 itachambuliwa kwa kina kwa lengo la kuangalia uhusiano wa sheria hizi na ardhi za vijiji.

#### 2.2.2.1 Sheria ya Wanyama Pori ya Mwaka 1974

Baada ya uhuru serikali ya Tanzania ilitunga sheria ya Uhifadhi wa wanyama pori ya mwaka 1974[28] na kuanzisha mapori tengefu ambapo Loliondo na Sale yalitangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 269 la 1974. Sheria ya Wanyama Pori ya mwaka 1974, imechambuliwa zaidi kwa lengo la kubainisha uhusiano na uwepo wa sheria hii na ardhi za vijiji. Uchambuzi wa sheria hii itaainisha jinsi mapori tengefu na mapori ya akiba yalivyo anzishwa kwa lengo la kusimamia rasilimali za wanyama pori kipindi cha nyuma bila kuathiri milki za kimila za ardhi katika ardhi za Vijiji wakati wa ukoloni na baada ya Uhuru. Kabla ya sheria hii ya wanyamapori kutungwa baada ya uhuru, kulikuwa na sheria ya Ukoloni iliyoitwa Fauna Game Ordinance, iliyoanzisha pori la akiba la Loliondo katika ardhi ya vijiji ambayo ilikuwa inatumika kwa taratibu za mila na tamaduni zao kama ilivyokuwa nchi nzima kabla ya ukoloni. Sheria ya Wanyama pori ya mwaka 1974 ilitambua aina tatu za mfumo wa ulinzi

27 Ole Nangoro, BN 1998, 'Branding the land: Maasai responses to resource tenure insecurity and social change', in Horn, F (ed), Economic, social and cultural rights of the Maasai, University of Lapland, Rovaniemi.

28 Na 12 ya Mwaka 1974

wa maliasili , Mapori ya Akiba ( Game reserves) Hifadhi za Taifa (National Parks ) na Pori tengefu (Game Controled areas). Mapori tengefu pekee ndiyo yalianzishwa katika maeneo ya Vijiji ambapo hayakuwa na mgogoro kwa kuwa hayakugusa milki ya ardhi ya Vijiji.

Ikumbukwe pia kwamba eneo hili la Loliondo ndilo ambalo wakoloni walionyesha kuwa makazi ya wenyeji baada ya uanzishwaji wa Hifadhi ya Serengeti. Lakini wakati wa ukoloni dhana ya mapori ya akiba yalianzishwa kwa lengo la kusimamia wanyamapori bila kuathiri matumizi na mila za usimamizi wa ardhi za wenyeji. Hata hivyo changamoto za kimaslahi kati ya vijiji vya wafugaji na makampuni binafsi za kitalii na kiwindaji zilianza pale Tanzania ilipoingia katika sera za mfumo wa soko huria na kuanza kubinafsisha hadi mashirika yaliyokuwa yanaratibu maswala ya rasilimali asili hapa nchini.Serikali iliruhusu hadi makampuni binafsi kuanza kusimamia shughuli za uwindaji.

Miaka hiyo kabla ya ubinafishaji mfano kazi za uwindaji zilikuwa chini ya Tanzania Wildlife Company (TAWICO) lakini baada ya miaka 1990 makampuni binafsi yalishamiri katika utalii wa uwindaji na ndio ujio wa Kampuni ya Kiarabu ya Kiwindaji ya (OBC) ulipoanzia katika eneo la Loliondo miaka ya 1992, na kupewa eneo lote la kilometa za mraba 4000 la Vijiji vya Loliondo na sale. Ujio wa Kampuni hii ya Kiarabu ilianzisha changamoto ya wananchi kutumia maeneo yao ya vijiji kinyume na sheria za ardhi na pia sheria hii ya Wanyama pori ya 1974. Migogoro mingi ilianza kuzuka baina ya kampuni hii na wananchi na pia baina ya kampuni hii ya OBC na watumiaji wengine wa ardhi ya vijiji kama makampuni mengine yanayofanya kazi za kitalii eneo hili. [29]

### 2.2.2.2 Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009

Mwaka 2009 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga Sheria Mpya ya Wanyamapori[30] ambayo ulileta mabadiliko katika usimamizi wa wanyamapori na uhifadhi. Katika sura hii ndogo, uchambuzi wa sheria ya Wanyamapori inaangazia na kuangalia madhara au matokeo ya mabadiliko haya kwa ardhi ya vijiji katika Taraza za Sale na Loliondo.

Mabadiliko yaliyotokea baada ya kutungwa kwa Sheria Mpya ya wanyama pori ya mwaka 2009, iliyofuta sheria ya zamani ya mwaka 1974. Kifungu cha 16 (5) cha sheria hiyo mpya ya mwaka 2009, kinamtaka kwamba Waziri Mwenye dhamana kuhakikisha anafanya mapitio ya mapori Tengefu na kutenganisha na ardhi ya Vijiji ndani ya mwaka (miezi 12) baada ya kuanza kutumika kwa

29 Framing Of Resource Use Conflicts in Loliondo Game Controlled Area- Tanzania -Wildlife Tourism, Conservation And Pastoralism Interface available at Https://Edepot.Wur.Nl/221913
30 Sheria Na. 5 ya 2009

sheria hiyo, ambapo Waziri hakuwahi kutekeleza kifungu hicho cha sheria cha kutenganisha ardhi ya Vijiji na Mapori tengefu. Sheria hii imepiga marufuku shughuli zote za kibinadamu katika maeneo ya mapori tengefu ambayo kimsingi yalikuwa yamepachikwa katika ardhi za Vijiji kwa kuwa lengo lake lilikuwa ni kusimamia rasilimali za wanyama pori na sio milki ya ardhi.

Pamoja na uwepo wa mgogoro wa ardhi ya Vijiji kwa takribani katika Tarafa za Loliondo na Sale kuanzia miaka ya 1992, mabadiliko hayo ya kisheria yamechochea kasi ya mgogoro baada ya kutekelezwa kwa jaribio la kutenga eneo halali la Vijiji lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1500, kupitia Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya wilaya ambayo ilifadhiliwa na Kampuni ya uwindaji ya OBC mwaka 2010, kwa lengo la kulinda malsahi yake ya uwindaji katika eneo hilo. Baada ya wananchi kugundua nia ya Kampuni ya OBC kumegewa ardhi ya Vijiji, mgogoro mpya iliibuka ambapo Kijiji cha Soitsambu mwaka 2010 ilitoa Notisi ya kusudio la kumuondoa OBC kwenye ardhi ya Kijiji kwa barua yenye kumbukumbu namba AR/KJ/55/402/4/13[31], kwamba ifikapo mwezi Desemba Kijiji hicho kitakuwa huru kupangia matumizi mengine katika ardhi hiyo ya Kijiji[32].

Matokeo ya Mabadiliko ya Sheria ya 2009 kwa Pori Tengefu la Loliondo Sheria iliyokuwa imetambua mapori tengefu ndani ya ardhi za wananchi ikaja kubadili hadhi ya mapori tengefu na kuondoa shughuli zote za kibinadamu bila kutambua eneo lote la Loliondo na sehemu ya Sale yalikuwa ni ardhi za vjiijiji vilivyokuwa na mapori haya tengefu.33 Wilaya zingine za kifugaji ambazo zimekuwa na mapori tengefu ndani ya ardhi ya vijiji ni Pamoja na Longido, Monduli na Simanjiro na vijjiji vyingi katika wilaya hizi zimepatiwa hati za umiliki.

Mabadiliko ya Sheria ya Wanayamapori yamebadili hadhi ya mapori tengefu na kuondoa shughuli zote za kibinadamu kama ilivyokuwa awali. Sheria hii kwa kutambua kuwa maeneo mengi yaliyokuwa na mapori tengefu ni ardhi halali za vijiji iliweka utaratibu katika kifungu cha 16 (4) hadi 16 (5) kwa waziri kutambua maeneo yote ya yenye mapori tengefu yaliyoko katika ardhi ya vijiji na kutangaza ndani ya mwaka mmoja toka baada ya kuanza kutumika kwa sheria hii kuwa yamekosa hadhi ya kuwa mapori tengefu. " For the purpose of sub-section 4 , The Minister shall ensure that no land falling under the village land is included under the game controlled areas' Section 16 (5)

---

31 Barua ya tarehe 5 januari, 2010, iliyoandikwa na Mwenyekiti wa Kijiji hicho James Lembikas ambayo nakala yake ilitolewa kwa DED Ngorongoro, Mbunge, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya, Dc, RC na katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

32 kuanzia 31/12/2010, Kijiji kitakuwa huru kwa kuwekeza ardhi yake kwa Makampuni mengine au kwa shughuli nyingine yeyote kwa manufaa ya jamii." ifikapo tareh 31st of Desemba, 2010

33 Wildlife Conservation Act No. 5 of 2009, Section 20(1) and 21(1), Wildlife Conservation Act of 2009, Section 16(5). The Wildlife Conservation Act of 2009 came into force in July, 2010.

Tafsiri yake ni kuwa , kwa kutambua kuwa maeneo mengi karibu asilimia 60 ya mapori tengefu hapa nchini yalikuwa katika ardhi ya vijiji, watunzi wa sheria hii waliona ni muhimu kuondoa mapori tengefu katika maeneo ambayo yalikuwa ni ardhi za vijiji kama ilivyokuwa kilometa za Mraba 4000 Loliondo na Sale. Bahati mbaya zoezi hili kwa upande wa Loliondo halikufanyika kama sheria ilivyoagiza, badala yake kumekuwemo na maneno mengi kuwa bado Loliondo nzima ni GCA kinyume na utaratibu wa sasa wa kisheria ambao hauruhusu mapori tengefu  kuchangamana na shughuli za kibadamu.  Matokeo yake ni kwamba kwa mujibu wa sheria ya Wanyama Pori ya sasa Loliondo hakuna tena pori tengefu inayotambulika kisheria.

### 2.3 Mifumo ya Kimila na Desturi za Kimaasai katika Usimamizi wa Ardhi na Maliasili

Sura hii ndogo inafafanua mila na desturi za Kimasai katika usimamizi wa ardhi na maliasili. Lengo ni kuonyesha kuwa sheria na taratibu za kimila pia zimekuwa na mchango mkubwa katika kuhifadhi maeneo haya kabla ya wakoloni, wakati wa wakoloni, hata baada ya uhuru hadi sasa.

#### 2.3.1 Mahusiano ya Mila za kimaasai na Wanyamapori

Pamoja na kwamba sheria za kikoloni na hata za Tanzania baada ya Uhuru zilitungwa ili kuweza kusimamia sekta ya ardhi na uhifadhi, ni muhimu kwa wadau wote kufahamu kwamba Mila, utamaduni na elimu ya asili zimekuwa nguzo kuu na muhimu  katika kuendeleza ardhi na maliasili katika tarafa za Loliondo na Sale.  Jamii ya wafugaji wa Kimaasai inategemea  mfumo wa asili wa matumizi ya pamoja ya ardhi unaotegemea misingi ya maarifa za desturi na mila za jadi.

Ardhi inatumiwa kulingana na mahitaji ya pamoja ikiwepo ufugaji, makazi na matambiko. Kwa utaratibu wa maarifa za jadi nyanda za malisho zinasimamiwa kwa aina ya matumizi kulingana na msimu (kiangazi, masika na kipupwe). Matumizi ya ardhi yanasimamiwa kwa kutumia mifumo ya asili ya mila na desturi chini ya uratibu na miongozo ya viongozi wa mila (Ilaigwanak). Mila na desturi ya jamii huzingatia uhifadhi wa mazingira, matumizi ya nyanda za malisho (maji na malisho) kwa ajili ya matumizi ya mifugo na wanyamapori. Mfumo huu ulijenga mahusiano mazuri ya asili baina ya wanyamapori, mifugo na watu tangu enzi na enzi.

Mahusiano baina ya mifugo na wanyamapori; mila na desturi ni nguzo kuu katika kuendeleza wanyama pori na rasilimali za asili katika tarafa ya Loliondo and Sale. Licha ya uendelevu wa utaratibu huu, mfumo wake wa usimamizi wa ardhi kwa mifumo ya asili ya nyanda za malisho umekumbwa na migongano mingi ya kisheria na za kisera za uhifadhi wa wanyamapori.

Uhusiano wa Jamii hii na wanyama pori ni wa kihistoria na ya kimila[34]. Sisi wamasai hatuwindi na hatuli nyama za wanyama pori tofauti na jamii zingine za Kitanzania na duniani kote kwa kuwa wanyama wamewekwa katika utaratibu wa mila ya koo za jamii. kwa mantiki hiyo kila aina ya wanyama wanapata ulinzi maalumu kutoka koo husika ambapo mtu yeyote akikiuka haki ya wanyama hao huadhibiwa kulingana na ukubwa wa kosa, ambapo makosa makubwa yanahitaji utakaso wa mitambiko ili kuondoa laana hiyo. Sababu hii ya kimila imeendelea kuimarisha mahusiano mazuri baina ya wanyama pori na watu katika jamii tangu enzi zote hadi sasa. Kitendo cha kuanza kutunga sheria na sera zinazolenga kuvuruga mahusiano haya na kwa ajili ya kuchukuwa ardhi ya watu wa jamii hii kwa sababu za kiuhifadhi ni kutengeneza mgogoro usioisha ambayo itakuwa na madhara makubwa kwa jamii husika na kwa taifa kwa ujumla.

**Jedwali 2.3:Mahusiano baina ya koo za Wamaasai na Wanyama pori**

| Na. | Koo za kimaasai | Aina ya wanyamapori wa koo husika |
|---|---|---|
| | Irmollelian (Mollel) | Faru, Chui, Mbweha |
| 1. | Laitayok | Tembo na Nyati |
| | Ilaiser/Laizer | Simba |
| | Ilaisi/Iltaar-osero/Ilt-anap-Owaru | Fisi, Nyoka (Cobra), Twiga Swala, Nyumbu |
| | Irmakesen/Irmamasita | Pundamilia na Tai |
| | Ilukumai | Nyani na Tumbili |

*2.3.2 Mifumo ya Asili ya Matumizi ya ardhi ya Nyanda za Malisho*

Ufugaji wa asili ni mfumo wa maisha unaotegemea nguzo kuu tatu, ardhi, mifugo na familia. Mfumo huu wa uzalishaji unahusu ufugaji wa mifugo aina ya ng'ombe, mbuzi na kondoo kwa ajili ya uzalishaji unaotegemea hali ya hewa na ubora wa nyanda za malisho.

Uratibu wa shughuli za ufugaji hubadilika kulingana na hali ya hewa na uoto wa asili wa nyanda za malisho. Hivyo shughuli za kuratibu ufugaji unahitaji mikakati na usimamizi dhabiti ili kuendana na nyakati na mabadiliko ya hali ya hewa ili kustahimili mabadiliko. Tofauti na ufugaji mwingine kama wa kuku, nguruwe na Samaki, ufugaji wa asili hutegemea misimu na nyakati tofauti ya upatikanaji wa malisho na mvua. Mabadiliko katika hali ya hewa unashawishi suala zima la ufugaji na mipango ya ufugaji wa asili.

34 https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/habari-ya-ndani/koo-za-kimasai-ngorongoro-zina-udugu-na-wanyama--2782572

Zaidi ya miongo miwili Nchi nyingi za Afrika zilianzisha na kutekeleza sera na sheria za ufugaji wa asili, na hasa katika kutambua mifumo halisi ya matumizi ya ardhi na usimamizi wa maliasili katika nyanda za malisho wanaoishi wafugaji. Sera na sheria hizi zinatambua haki za umiliki wa ardhi kulingana na taratibu, kanuni na desturi za wafugaji na kutambua rasilimali asili zinazo wezesha ufugaji. Mifano ya Nchi hizi za Afrika ni pamoja na Mauritania (2000), Mali (2001, 2010) and Niger (2012)[35].

Sera ya Umoja wa Mataifa juu ya Wafugaji, imesisitiza haja ya kuwashirikisha wafugaji katika nchi husika kutunga sera, sheria na kanuni za kuratibu na kuendeleza ufugaji wa asili kulingana na misimu ya malisho na mvua. Ushirikishwaji wa pamoja baina ya Wafugaji na Serikali utawezesha wataalamu toka wizara husika ikiwemo Wizara ya Maliasili, Ardhi na Mifugo kutambua na kudhamini uchumi wa wafugaji na mazao yatokanayo na mifugo.[36]

Mabadiliko ya tabia ya nchi haijasababishwa na ufugaji, na si kosa la wafugaji. Mabadiliko ya Tabia Nchi na ukame wa muda mrefu ni janga la dunia na changamoto kwa wazalishaji wote wanaotegemea rasilimali asili hasa inayotegemea mvua. Pamoja na janga hili la dunia katika uzalishaji, wafugaji wameendelea kuendesha Maisha yao kupitia ufugaji katika mazingira tete ya ukame na mabadiliko ya tabia nchi. Utaalamu na uzoefu wa mazingira unaotumika katika nyanda za malisho katika Tarafa za Loliondo na Sale hutokana na elimu ya jadi ya mazingira inayowezesha wafugaji kubuni na kutumia fursa za haraka zinazojitokeza kuendesha uzalishaji wa mifugo yao. Serikali na taasisi mbalimbali wanapaswa aidha kuboresha mifumo wa asili juu ya usimamizi wa ardhi na maliasili au kutoingilia wafugaji katika matumizi ya ardhi kwani kuwaingilia bila kujadiliana nao utaathiri na kuangamiza maisha ya wafugaji.

35 African Union. 2010. Policy Framework for Pastoralism in Africa: Securing, Protecting and Improving the Lives, Livelihoods and Rights of Pastoralist Communities. Department of Rural Economy and Agriculture, African Union, Addis Ababa.
36 ibid

SURA YA
TATU

# HISTORIA NA JITIHADA ZA UTATUZI WA MGOGORO WA ARDHI TARAFA ZA LOLIONDO NA SALE

## 3.0 UTANGULIZI

Sura hii inalenga kutoa ufafanuzi wa kina juu ya historia ya mgogoro, chanzo chake, madhara yatokanayo pamoja na jitihada zilizochukuliwa kutatua mgogoro katika tarafa za Loliondo na Sale. Lengo la sura hii ni kuwafahamisha wasomaji wa taarifa kuhusu historia na hali ya sasa ya mgogoro huu wa rasilimali. Sura hii itasomwa sambamba na sura zingine zilizotangulia.

### 3.1 Historia na Chanzo cha Mgogoro wa Ardhi Tarafa ya Loliondo na Sale

Taarifa na kumbukumbu zinaonyesha kuwa migogoro katika Tarafa za Loliondo na Sale ziliaanza kabla ya Uhuru wa Tanganyika, na imekuwa ikichukua sura tofauti kadiri muda unavyo kwenda. Kwa mantiki hiyo, uchambuzi wa matukio, sura ya migogoro ya ardhi katika Tarafa hizi zinaweza kupangwa katika vipindi tofauti vya kihistoria. Migongano hii kwa kiasi kikubwa imekuwa baina ya Wenyeji-Wafugaji wa Kimaasai na Wizara ya maliasili na Utalii kwa nyakati tofauti. Aidha, sababu za migogoro imekuwa ni mgongano wa maslahi ya maisha kwa wenyeji, na ya kibiashara/ uhifadhi kwa upande wa watawala na wawekezaji. Kwa mujibu wa nyaraka mbalimbali, mgogoro huu umegawanyika katika sehemu kuu tatu, ambazo ni kipindi cha utawala wa wakoloni, baada ya uhuru na baada ya ujio wa kampuni ya kiwindaji ya OBC mwaka 1992.

**Vyanzo vikuu vya Mgogoro huu**

- Dhana ya kikoloni ya uhifadhi wa maliasili (Fortress conservation) inayoendelea kutumiwa na Wahifadhi na Serikali
- Kuondolewa kwa wafugaji wa Jamii ya Kimasai kupisha uanzishwaji wa Hifadhi ya Serengeti 1958
- Mgongano kati ya Sheria za ardhi, Serikali za Mitaa na Sheria za wanyamapori
- Ujio wa kampuni ya Ortello Business Corporation (OBC)

- Mapendekezo ya kamati ya Matumizi Mseto ya ardhi ya Ngorongoro juu ya kumega eneo la Vijiji vya tarafa za Loliondo na Sale yenye kilomita za mraba 1500 kuwa chini ya NCA.

### 3.1.1 Kuondolewa kwa wafugaji wa Jamii ya Kimasai kupisha uanzishwaji wa Hifadhi ya Serengeti 1958

Mgogoro ulianza miaka 1950 baada ya serikali ya kikoloni kuwataka ndugu zetu na wazazi wetu waliokuwa wanaishi Serengeti kuondoka ili kupisha uanzishaji wa Hifadhi ya Serengeti. Mwaka 1958 makubaliano yalifikiwa baada ya mazungumzo ya miaka zaidi ya 8 na Jamii yetu na hatimaye kushurutishwa kimazingira kukubaliana na kuridhia mipaka ibadilishwe na maslahi mengine kupitia "Serengeti Compensation Scheme".

**Jedwali 3.1:Mchakato wa kuchukuliwa Maeneo ya Wamasai Serengeti**

| Mwaka | Tukio |
|---|---|
| **Kabla ya Uhuru** | |
| 1950 – 1958 | Mjadala kati ya serikali ya kikoloni na jamii ya wamasai kuhusu kuondoka Serengeti ili kupisha uanzishwaji wa hifadhi ya Serengeti ulianza na kuhitimishwa kwa Jamii ya wamasai kukubaliana kuondoka na kuhamia Ngorongoro pamoja na Loliondo na kuungana na wenzao waliokuwa wanaishi hapo kabla. |
| 1959 | Wamasai walikubali kusaini mkataba wa makubaliano ya kuondoka Serengeti baada ya kukubaliana na kuridhia mipaka na maslahi mengine kupitia mpango wa fidia wa Serengeti "Serengeti Compensation Scheme" |

Makubaliano yalipelekea kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti (1959); na Hifadhi ya Ngorongoro (1959) ambako serikali ilikubali kufanya majaribio ya kuwa na hifadhi yenye matumizi mseto ya ardhi (wanyamapori, shughuli za binadamu, na utalii). Katika makubaliano ambyo hadi sasa hatuna uhakika na uhalali wake, kupitia mpango wa serengeti ya fidia, serikali ilitoa ahadi lukuki kwa wafugaji endapo watakubali kuhama kwenda maeneo ya Loliondo na Nyanda za juu za Ngorongoro. Kwanza tulihaidiwa kupewa huduma za mifugo kama majosho, maji, na huduma zingine za kijamii. Pili, tulihaidiwa kuwa huko tuendako upande wa mashariki mwa Serengeti (Loliondo) endapo patatokea mgogoro baina ya Wamasai na shughuli za uhifadhi, haki zetu zitapewa kipaumbele zaidi. Baada ya sisi kuhamishwa baadhi ya ahadi hizo hazikutekelezwa na Serikali hiyo ya Kikoloni lakini na zingine kwa sasa haziheshimiwi na serikali ya sasa.

Kutokuheshimiwa na kutotambuliwakwa makubaliano haya ndiyo kumepelekea kuendelea kwa migogoro ya ardhi baina ya jamii ya wamasai na shughuli za uhifadhi. Hali hii imechangia jamii yetu ya Kimasai kuendelea kufukuzwa katika maeneo yao ya asili kwa lengo la uwekezaji wa utalii na uhifadhi.

## Agreement by the Maasai to vacate the Western Serengeti

We, the Laigwanak (elders) of the Ngorongoro and Loliondo division of the Maasai district, agree on behalf of all the Maasai living in these areas to renounce our claim to all those parts of the Serengeti plains lying within the Northern and Lake provinces which lie to the west of the line* shown to us by the District Commissioner, Maasai on the 13th and 14th March and the 20th April, 1958.

We understand that as a result of this renunciation we shall not be entitled henceforth in the years to come to cross this line which will become the boundary of the new Serengeti National Park and which will be demarcated. We also understand that we shall not be entitled to reside in or use in future the land lying to the west of this line, which we have habitually used in the past.

We agree to move ourselves, our possessions, our cattle and all our other animals out of this land by the advent of the next short rains, that is before the 31st December, 1958.

*Laigwanak:* Sgd.

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Seketa ole Pose | Ngorongoro |
| 2. | Tendemo ole Kisaka | Endulen |
| 3. | Ngoirien ole Mtunga | Moru |
| 4. | Olongoyu ole Goek | Ngorongoro |
| 5. | Pokidale ole Mausuusu | Moru |
| 6. | Loldunyai ole Murunga | Moru |
| 7. | Olmatapatoi ole Kekuka | Moru |
| 8. | Kissale ole Serupe | Makessio |
| 9. | Ndengoya ole Parmat | Loliondo |
| 10. | Keriko ole Lohumo | Loliondo |
| 11. | Olakeru ole Maleta | Loliondo |
| 12. | Munge ole Keyamba | Nainokanoka |

The above agreement was interpreted by me from English into Kimasai to the above-named Laigwanak today and I am satisfied that they have understood it and have signed it voluntarily.

Sgd. T. S. Colley
*Executive Officer*
*Maasai Federal Council*

Witnessed by us at Ngorongoro this 21st day of April, 1958.

Sgd. M. J. B. Molohan
*Principal Commissioner,*
*Northern Province*

Sgd. F. B. Townsend
*District Commissioner,*
*Masai District*

***Kielelezo 3.1:*** *Makubaliano ya MORU baina ya Viongozi wa mila (Malaigwanani) wa kimaasai 12 wa Loliondo na Ngorongoro na wakoloni 21st April, 1958*

*Chanzo: Shivji & Kapinga, 1998*[37]

37 Shivji & Kapinga. 1998 Haki za Wamasai waishio katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, HAKIARDHI/IIED


### 3.1.2 Mgongano wa Sheria za ardhi, Serikali za Mitaa na Sheria za Wanyamapori

Mgongano kati ya Sheria za ardhi, Serikali za Mitaa na sheria za uhifadhi wa wanyamapori juu ya matumizi ya ardhi[38]. Baada ya uhuru serikali ya Tanzania iliendeleza sera za kikoloni ambapo miaka kadhaa baadae yaani mwaka 1968 iliongeza mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kupitia Tangazo la Serikali (GN. 235/1968) na katika kifungu cha tano ikatamka mipaka na kuionyesha kwenye ramani Na. 14151 mipaka mipya ya Hifadhi ya Taifa Serengeti.

Mwaka 1974 serikali ilitunga sheria ya Uhifadhi wa Wanyama Pori ya mwaka 1974[39] na kuanzisha mapori tengefu ambapo Loliondo na Sale yalitangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 269 la 1974. Hata hivyo Sheria ya uhifadhi wa wanyama pori ya wakati huo haikukataza matumizi mseto ndani ya Mapori Tengefu na ndio maana ilikuwa rahisi kuanzisha mapori tengefu katika ardhi za vijiji ambayo viliandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria zingine za nchi.

Katikati ya mgogoro huu serikali ilitunga Sheria ya uhifadhi wa Wanyama pori ya 2009, ambayo ilikataza shughuli za kibinadamu ndani ya mapori tengefu. Mwingiliano, utata na mgogoro wa kisheria iliongezeka baada ya Serikali kutaka kutenga eneo halali la Vijiji lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,500 kama sehemu ya utekelezaji wa sheria hiyo ambayo majaribio ya utekelezaji yaliaza Katika Tarafa za Loliondo na Sale pekee nchini kabla ya kutangazwa kwa tarehe ya kuanza kutumika. Hata hivyo jaribio hili lilionekana kuwa kinyime hata sheria yenyewe ya Wanyama Pori ya 2009 iliyoagiza mabadiliko yoyote yafanyike ndani yam mwaka mmoja baada ya sheria hiyo kuanza kutumika.

38 Ole Nasha T. W. (2004) Reforming Land Tenure In Tanzania: For Whose Benefit?. HAKIARDHI, Dar es Salaam
39 JMT (1974) Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Namba 12 ya Mwaka 1974




***Ramani 3.1:*** *Ramani ya Tarafa za Loliondo na sale ikionyesha Vijiji vyenye Migogoro*

Vijiji hivyo vilivyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za nchi kama vile Sheria ya Kuandikishwa Vijiji, Kutambuliwa kwa Vijiji vya Ujamaa na Uongozi wa Vijiji ya 1975[40] na Sheria ya Serikali za mitaa [Mamlaka za Wilaya] Na. 7 ya 1982, kupimwa na kupata hati za ardhi kwa mujibu wa Sheria ya ardhi Sura ya 113 na Sheria ya ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999, kama ilivyo ainishwa hapo juu kwenye sura pili ya taarifa hii.

40https://www.tanzania.go.tz/egov_uploads/documents/The_Villages_and_Ujamaa_Villages_(Registration,_Designation__sw.pdf

Eneo hili la Vijiji linasimamiwa kwa mujibu wa sheria mbalimbali kama vile Sheria ya mipango ya Matumizi ya Ardhi Na.6 ya 2007, Sheria ya Nyanda za Malisho na Vyakula vya Mifugo ya Sura ya 180 ya Sheria za Tanzania.

Hata hivyo, Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 imefafanua katika kifungu cha 181 kuwa endapo itatotekea mgongano/mgogoro wa kisheria kati ya sheria hii ya ardhi na sheria zingine katika tafsiri ya matumizi ya ardhi, sheria hii itakuwa na nguvu zaidi[41]. Kitendo cha kumega Ardhi ya Vijiji katika Tarafa za Loliondo na Sale eneo lenye kilomita za mraba 1500, ni kuvunja sheria za ardhi na Katiba ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977[42], kama ilivyo fanyiwa marekebisho mara kwa mara.

Hivyo basi, Serikali itangaze rasmi kuwa ardhi za vijiji vilivyokuwa na mapori tengefu kabla ya sheria ya 2009 kwa sasa havina hadhi tena ya mapori tengefu ili kuondoa usumbufu unaondelea kwa sasa . Vilevile sheria hii inatarajiwa kuibua migogoro katika maeneo mengi nchini kwa kuwa mapori tengefu yalianzishwa katika ardhi za Vijiji zilizo sajiliwa, kupimwa kupata hati za ardhi/Vyeti vya ardhi za Vijiji na kufanya Mipango ya matumizi ya ardhi. Aidha kwa tafsiri ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyama Pori Na.5 ya 2009 katika kifungu cha 16(5), hakuna pori tengefu lolote Loliondo kwa kuwa haikuwahi kutangazwa kwenye Gazeti lolote la Serikali (GN) tangu kuanza kutumika kwa Sheria hiyo.

### 3.1.3 Ujio wa Kampuni ya Ortello Business Corporation

Mwaka 1992 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia ofisi yya Mkuu wa Wilaya Ngorongoro, Mhe Mbunge na mwenyekiti wa Halmashauri ilisaini Mkataba wa uwindaji na Mhe Brigadier Mohammed Abdulahim Al-Ali ndani ya ardhi ya vijiji vya Tarafa za Loliondo na Sale bila kupatikana ridhaa ya vijiji. Rejea mkataba ulioingiwa katika makundi tajwa hapo juu . Baadae shughuli zote za uwindaji kwa niaba ya Mfalme huyu zilianza kufanywa na kusimamiwa na kampuni iliyoanzishwa kwa malengo haya, kampuni hiyo ni Ortello Business Corporation (OBC).

41 Application of this Act, "On and after the commencement of this Act, notwithstanding any other written law to the contrary, this Act shall apply to all land in Mainland Tanzania and any provisions of any other written law applicable to land which conflict or are inconsistent with any of the provisions of this Act shall to the extent of that conflict or that inconsistency cease to be applicable to land or any matter connected with land in Mainland Tanzania"

42 24.-(1) Every person is entitled to own property, and has a right to the protection of his property held in accordance with the law. (2) Subject to the provisions of subarticle (1), it shall be unlawful for any person to be deprived of his property for the purposes of nationalization or any other purposes without the authority of law which makes provision for fair and adequate compensation

Annexure "D"

MKATABA WA AJILI YA KUHIFADHI NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA WANYAMAPORI ILIKULETA MAENDELEO YA VIJIJI KATIKA ENEO LA LOLIONDO GAME CONTROLLED AREA: SOUTH AND NORTH

Mkataba huu umetiwa sahihi leo tarehe ....20th November....mwezi Nov.....wa 1992.

KATI YA

MHESHIMIWA BRIGADIA MOHAMED ABDULRAHIM AL-ALI wa ............(katika mkataba huu atarejewa kama BRIGADIA) kwa upande mmoja.

NA

Halmashauri ya Wilaya ya NGORONGORO kwa niaba ya Vijiji vilivyotajwa hapa chini:

1. OLOLOSO KWAN
2. ESOIT - SAMBU / SOIT SAMBU -7
3. OLOPERI — OLOIPERI -7
4. OLORIEN / MAGAIDURU -2
5. OLOO - SOITO / LOOSOITO -2
6. ARASH


(Katika mkataba huu marejeo yatakuwa kwa halmashauri au vijiji vilivyotajwa hapo juu) kwa upande mwingine.

Kwa kuwa wanyamapori ni rasilimali yenye uwezo mkubwa wa kutengeneza fedha za kigeni kuwapatia wananchi kazi na hivyo kupandisha hali yao ya maisha endapo itashughulikiwa ipasavyo;

Na kwa kuwa wanyamapori katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro hawajashughulikiwa ipasavyo na hivyo kutoa mchango mdogo sana katika uchumi wa Wilaya hiyo, wananchi wake na Taifa kwa ujumla;

Na kwa kuwa BRIGADIA ameomba na amepewa kibali cha uwindaji wa binafsi kwa ajili yake yeye mwenyewe, marafiki zake, na wageni wake katika eneo la "Loliondo Game Controlled Area" (ona kiambatanisho "A" ambacho ni sehemu kamili ya mkataba huu) ambalo liko katika eneo la halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro.

Na kwa kuwa moja ya masharti ya kuzingatia kabla ya kuanza kunufaika na kibali hicho BRIGADIA analazimika kuingia katika ~~katika~~ mkataba wa namna hii na



SAHIHI.........
AHMED SAEED ABDULRAHAMAN ALKHATEEB
(KWA NIABA YA MHESHIMIWA BRIGADIA
MOHAMED ABDULRAHIM AL-ALI

SAHIHI......... 20/11/9
MKUU WA WILAYA
(KWA NIABA YA
~~VIJIJI~~ SERIKALI KUU
~~VILIVYOTAJWA~~
~~HAPO JUU~~)

MBELE YA:
SAHIHI.........
MHESHIMIWA R.P. KOILLAH
(MBUNGE WA ~~LOLIONDO~~) NGORONGORO.
KWA NIABA YA VIJIJI SITA (6)

NA:
SAHIHI.........
MKURUGENZI ~~WA~~ MTENDAJI
MAENDELEO YA
YA WILAYA (KWA
NIABA YA
HALMASHAURI YA
WILAYA YA
NGORONGORO)

SHAHIDI......... 20/11/92

SHAHIDI. JOSEPH N. MAAI
..PAULO L. NGURUMI
..ERNEST J. LAIZER
..JEROME J. KIWIA

***Picha 3.1:*** *Mkataba wa Serikali na Mfalme wa Uarabuni (UAE)*

Kwa sababu ya kukosekana kwa ridhaa ya wananchi kupitia mamlaka za vijiji, serikali ilivunja sheria za mikataba kwa kuchukuwa nafasi ya vijiji na kusaini mkataba kwa niaba yao bila ridhaa ya vijiji. Tukio hili linakuwa la pili katika mtiririko wa kuchukua nafasi ya jamii na au kufinya nafasi ya ushiriki wa jamii katika kuamua mustakabali wa usalama wa ardhi yetu.

Hali hii ilizua taharuki kubwa iliyojulikana kwa jina la 'Loliondo Gate Scandal'. Kampeni hii ilivuka mipaka ya Tanzania na kuhusisha mitandao, vyombo vya habari na watetezi wa haki za binadamu duniani. Wakati huo, mgogoro huu maarufu wa Loliondo ulihusu jamii kudai nafasi ya ushiriki katika maamuzi ya mpangilio na matumizi ya ardhi yetu.

Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii ilisimama kumtetea Mfalme kwa kisingizio kwamba ni mwekezaji mwenye faida kwa nchi yetu na hadhi ya kidipomasia. Kupitia mapishano haya kwa miaka yote, mgogoro huu umejengwa na kubebwa na dhana ya uhifadhi kwa upande wa serikali na mwekezaji, na usalama wa ardhi na malisho kwa upande wa jamii.

### 3.1.3.1 Mikakati na hatua za OBC kutengewa Ardhi ya Vijiji

Mwaka moja tu baada ya OBC kuanza kazi, Rasimu ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi Wilaya ya Ngorongoro (Ngorongoro District Land Use Framework Plan (1993 – 2008) ilitayarishwa kwa msaada wa OBC na kuanisha eneo (linalokadiriwa sasa kuwa ni km za mraba 1500) kuwa eneo linalopaswa kutumika kwa madhumuni ya Uhifadhi wa wanyama pori na utalii. Ni muhimu kutambua kuwa hata mpango huu wa matumizi ya ardhi, 1993-2008, haukuandaliwa katika mazingira ya ushiriki wa wananchi bali kwa msukumo wa kampuni ya OBC[43]. Na sababu hiyo mpango huu wa kwanza wa kutaka kuchukua ardhi ya vijiji kupitia mpango wa matumizi bora ya ardhi ulikwama.



***Picha 3.2:***
*Majengo ya Kambi ya OBC katika eneo la Vijiji*

Mwaka 1996, Kampuni ya OBC ilianzisha hatua za kuweka miundombinu katika ardhi ya vijiji vyetu kwa lengo la kufanikisha shughuli zake zikiwepo, ujenzi wa barabara, ujenzi wa kambi na uwanja wa ndege bila ushirikishwaji wa wananchi. Ujenzi wa miundombinu hizi, ziliibua tena hasira kwa wananchi. Hata hivyo, taratibu za kimazingira hazikuzingatiwa hasa baada ya kempu ya kudumu kujengwa katika chanzo cha maji ya mto Olasae.

43 Just Conservation - Grabbing Land for Conservation in Loliondo, Tanzania.



***Picha 3. 3:*** *Ndege kubwa ya OBC ikipakua mizigo katika kiwanja chake cha ndege katika eneo la Lima Loliondo mwaka 2009.*

Mgogoro wa Loliondo- katika Tarafa za Loliondo na Sale umekuwa ni mgogoro mkubwa na wenye kubadilisha sura na mikakati kwa nyakati tofauti. Kampuni ya OBC kwa kushirikiana na serikali ilifadhili Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya Wilaya ya mwaka 2010-2030[44], na kwa kutumia ushawishi wake wa fedha, rasimu hiyo ilibainisha eneo la km za mraba 1500 kama eneo la kutengwa kwa ajili ya uhifadhi/uwindaji. Hapa ndipo, namba hizi maarufu 1500 iliendelea kujitokeza. Pamoja na kwamba huwezi kutengeneza mpango wa matumizi bora ya Ardhi ya Wilaya kabla ya kushirikisha vijiji, mpango huu ulilazimishwa kutengenezwa na hatimaye kupata upinzani mkubwa wa vyombo vya maamuzi kama vijiji, baraza la madiwani, na hivyo kushindikana kutekelezwa[45].

Mpango huu wa 2010-30 ulikwama kupitishwa na kutekelezwa kutokana pingamizi kubwa ya jamii na viongozi wa jamii. Mpango huo ulikuwama kwa kwakuwa ulikuwa na hitilafu za kisheria hasa sheria ya mipango na matumizi ya ardhi.

Mabadiliko ya Sheria ya mwaka 2009 zilizoondoa mapori tengefu katika ardhi ya vijiji kama ilivyoelezwa katika sura ya pili ilidhamiria kuimarisha hoja kutaka eneo la km za mraba 1500 kwa ajili uwindaji.

Pamoja na kwamba mipango yote imekwama kupitishwa na Baraza la Madiwani[46], Wizara ya Maliasaili na Utalii iliaanza kutambua eneo hilo la vijiji

44 Hotuba ya Mhe. John Zefania Chiligati, (Mb.),Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, akiwasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya wizara ya ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi, kwa mwaka 2010/11.https://www.tanzania.go.tz/egov_uploads/documents/2010-2011_SWAHILI_sw.pdf, imerejewa tarehe 3/5/2022

45 https://ntz.info/gen/n01526.html, imerejewa tarehe 3 mei, 2022

46 https://www.youtube.com/watch?v=7knZOEVxO0k, Hii ni filamu inaonyesha msimamo wa madiwani wa Wilaya ya Ngorongoro wakikataa rasimu ya mpango wa matumizi ya ardhi ya Wilaya ya 2010. Wananchi pia wamepaza sauti zao wakionyesha msimamo kuwa hawako tayari kuondolewa katika maeneo ya Vijiji kupisha mwekezaji wa OBC.

kama ndio pori tengefu la Loliondo. Operesheni za mwaka 2013[47], 2014[48] na 2017[49] ni mikakati mojawapo iliyokuwa inatumia nguvu kubwa kutaka kulitenga eneo hili la vijiji kwa msaada mkubwa wa OBC.

Pia, kampuni ya OBC imekuwa ikithibiti eneo hilo la vijiji kwa kutishia mifugo isitumie eneo hilo, kuwatishia wachungaji na kusababisha taharuki kwa nyakati tofauti. Mgawanyiko wa kijamii pia imekuwa ni moja ya sifa kuu katika mgogoro huu, huku kampuni ikishiriki hujuma hii kupitia ahadi za uongo na rushwa. Kwa muda sasa kampuni hii pia imeanzisha kampuni yake ya mawasiliano ambayo kwa sehemu kubwa imeathiri upatikanaji wa mawasiliano kwa upande wa watanzania. Kwa ufupi, ili kuweza kutatua mgogoro huu wa Loliondo, ni muhimu kampuni hii kuondolewa kwa maslahi ya Taifa/Wananchi na kufungua mwanya wa majadiliano yenye afya kati ya wananchi na Serikali yao.

Kwa kuzingatia kuwa Rasimu ya Mpango huo ni ya muda mrefu wa mpangilio wa matumizi ya ardhi ndani ya Wilaya, Baraza la Madiwani liliweka msimamo wa kutopitisha rasimu hiyo kama sheria na taratibu zinavyotaka hadi pale marekebisho ya msingi yatakapofanywa ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wawakilishi wa wananchi ipasavyo katika kuandaa mpango huo.






***Picha 3.4:*** *Picha kushoto alievaa suti ni Waziri wa Maliasili na Utalii (2017) Prof. Maghembe akiwa na waandishi wa habari Jackton Manyerere, na Matinyi, na Picha ya kulia ni Waziri wa Maliasili na Utalii (2014-2015) Ndg Lazaro Nyalandu na akimpokea Sheikh Mohamme*

47 Operesheni Tokomeza ilitekelezwa Loliondo kwa lengo la kutisha watu na hasa wananchi waliokuwa mstari wa mbele katika utetezi wa Ardhi
48 Mwendelezo wa operesheni tokomeza
49 Operesheni nyingine ya kuondoa wenyeji katika ardhi hii ya kijiji

Hadi sasa rasimu ya mpango huo bado haijapitishwa na kuanza kutekelezwa wala kuzingatiwa katika matumizi ya mipango ya matumizi ya ardhi ndani ya Wilaya. Kwa mujibu wa vyanzo vya mbalimbali vya habari vinaonyesha kwamba mpango huu ulifadhiliwa na kampuni ya OBC kwa kiasi cha fedha za kitanzania milioni 157[50] kwa lengo la kutengewa eneo la Vijiji lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1500. Ushawishi wa kutoa fedha kwaajili ya kutengewa eneo la Vijiji ni kinyume na makubaliano ambayo hayakuwa na uhalali wa wananchi pamoja na Sheria za Nchi.




***Ramani 3.2:*** *Ramani ya mapendekezo ya matumizi Bora ya Ardhi ya Wilaya ya Ngorongoro 2010 kama ilivyondaliwa na Tume ya Mipango na Matumizi Bora ya Ardhi na Halmshauri ya Wilaya Ngorongoro*

50 Taarifa ya Haraka kwa Vyombo vya Habari Kuhusu Mgogoro wa Ardhi Loliondo ya tarehe 21 Novemba, 2014, inapatikana kwenye link hii,https://www.wavuti.com/2014/11/taarifa-ya-dharura-kuhusu-mgogoro-wa.html, imerejewa tarehe, 4/4/2022

### 3.1.3.2 Majaribio ya kuwaondoa Wananchi katika Ardhi ya Vijiji

Baada ya kushindikana kwa taratibu zingine za kisheria na kisera kuchukua eneo la km za mraba 1500, kampuni ya OBC na wandani wake wakabadilisha mbinu na kuanza kutumia nguvu za dola kutaka kutuondoa katika ardhi yetu. Nguvu hizi zimepelekea ukikuwaji mkubwa wa haki za binadamu kama inavyojitokeza katika sehemu mbalimbali za taarifa hapo chini. Tangu Kampuni ya OBC kuanza kufanya shughuli za uwindaji katika ardhi ya vijiji matukio mbalimbali yafuatayo katika jedwali 3.2 yalijitokeza;

**Jedwali 3.2: Matukio ya majaribio ya kutaka kuchukua ardhi ya Vijiji**


| Mwaka | Tukio | Matokeo |
|---|---|---|
| Baada ya Uhuru | | |
| 1992 | Serikali ya Tanzania iliingia makubaliano Na Mfalme juu ya ardhi ya Vijiji katika eneo lote la Vijiji vya Tarafa ya Loliondo na Piyaya na Malambo Tarafa ya Sale (km za mraba 4000) ambapo ilipelekea kuanza kwa Kashfa ya "Loliondo gate" | Chanzo cha Mgogoro hadi sasa |
| 1992 – 2008 | Licha ya Kampuni ya OBC kuendelea kufanya shughuli zake, bado vijiji viliendelea kutompa ushirikiano kwani hawana imani na kampuni hiyo. | Uhasama ukajengeka baina ya jamii na kampuni na kupelekea ukiukwaji wa haki za binadamu |
| 2008 | Kulikuwa na jitihada ya kujenga mahusiano na ushirikiano kati ya OBC na Vijiji ambayo kampuni ya OBC iliingia makubaliano (MOU) na vijiji 7 vilivyokuwa vinazunguka kambi/kitalu cha OBC kwa nia ya kutaka kumaliza mgogoro na mvutano uliokuwepo baina ya vijiji na kampuni. Makubaliano yalihusisha kampuni kutoa fedha kwa vijiji hivyo na kusaidia miradi mingine ya huduma za jamii. Hata hivyo pamoja na jitihada na nia njema makubalian hayo haikutekelezwa na kampuni. | • Utulivu wa muda mfupi ulipatikana lakini mwaka mmoja baadaye makubalino haya yalivunjika kutokana baadhi ya vifungu kutoheshimika.<br>• Makubalian yaliyokuwa yamefikiwa baina ya vijiji na OBC yalivunjika kutokana na hatua ya OBC kuhusika katika kusaidia operation ya kuwaondoa kwa nguvu mifugo, na kuchoma makazi ya wananchi |

| | | |
|---|---|---|
| 2009 | Sheria mpya ya Wanyama Pori Na. 5 ilitungwa na Bunge mwaka 2009, iliyofuta sheria ya wanyamapori ya mwaka 1974. Tofauti na sheria ya 1974, katika Sheria hii mapori tengefu yameainishwa kuwa ni maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uhifadhi wa wanyamapori na shughuli zote za binadamu haziruhusiwi zaidi ya utalii wa picha (non-consumptive tourism) na uwindaji wa kitalii (consumptive tourism). | Sheria hii ilianza kutumika kabla muda wake kuanza kwa kutaka kumega eneo la km za mraba 1500. Hi ilipelekea operation kubwa kubwakufanya mwaka 2009. Hapa ndipo nguvu za kidola zilianza kutumika kwa mara ya kwanza na kupelekea ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. |
| 2009 | Operesheni ya kuondoa kwa nguvu, mifugo na makazi kwenye ardhi ya Vijiji ndani ya Km za mraba 1500 kwa madai kwamba yapo ndani ya eneo la mwekezaji OBC ilitekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na OBC. | • Viongozi kadhaa wa NGOs walikamatwa kwa tuhuma za uchochezi.<br>• Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro Mh. Telele aliwasilisha hoja binafsi ndani ya Bunge kuomba uchunguzi wa kina ufanyike ili kujua madhila yaliyosababishwa na operesheni ya kuondoa mifugo, wahamiaji na kuchoma moto maboma.<br>• Bunge liliunda kamati teule iliyoongozwa na Mbunge wa Kongwa Mh. Job Ndugai (Mb).<br>• Waandishi mbalimbali wa vyombo vya habari vya ndani na nje waliendeleza kasi ya kuandika makala mbalimbali juu ya mgogoro wa Loliondo. Zaidi ya makala 20 ziliandikwa na gazeti moja pekee la JAMHURI |

| | | |
|---|---|---|
| 2010 | Rasimu ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Wilaya ya Ngorongoro uliandaliwa (2010 – 2030) – kwa uwezeshaji wa NLUPC, NDC na OBC - Mpango huu ulihuisha ule uliomalizika (1993 – 2008). Mpango huu ulipendekeza kutenga km 1500 na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji kwenye kata zote saba. | Mpango huu hata hivyo haukupitishwa na Baraza la Madiwani kwa walichoamini kuwa hawakushirikishwa katika uandaaji wake |
| Machi 2013 | Waziri wa Maliasili na Utalii Mh. Khamisi Kagasheki alitangaza kutenga eneo la km za mraba 1500 kutoka km 4000 za LGCA ili zisimamiwe na serikali kwa matumizi ya uhifadhi na uwindaji | Wizara ya Maliasili na wadau wake kutumia nguvu kubwa kusimamia hili tamko lake na kupelekea taharuki kubwa na ukiukwaji wa haki za binadamu |
| Mei 30, 2013 | Waziri Mkuu Mh. Mizengo Pinda (Mb) alitengua tamko la Waziri wa Maliasili na utalii kwa Barua Kumb. Na. PM/P/1/569/29 | Hali ikatulia kwa muda na utulivu ukarejea hadi badaye tena Wizaara ikaendelea na azma yake ya kutenga hilo eneo. Mikakati hii ya wizara ikazua kampeni kubwa ya kimataifa kupinga hatua hizi na hatimaye Bunge la Umoja wa Ulaya ilitoa Azimio la Kushauri Serikali ya Tanzania kusitisha azimio la kutaka kuchukua eneo la km za mraba 1500 |
| 2014 | Rais Mstaafu Jakaya Kikwete aliandika hakikisho katika akaunti yake ya 'Tweeter' hakikisho kuwa serikali haina mpango wa kuchukua la ardhi ya ya urithi wa wamasai. | Hali ikatulia kwa muda |
| 2015 | Television ya ITV iliandaa mfululizo wa vipindi vilivyorushwa na Jerry Muro ambavyo viliegemea upande mmoja na hivyo kukuza uzito wa mgogoro. | Ilianzisha migogoro na taharuki na kupelekea ukiukwaji wa haki ulilazimisha mashirika zaidi ya 20 ya haki za binadamu kutembelea eneo lenye mgogoro |

| | | |
|---|---|---|
| 2016 | Waziri Mkuu- Kassim Majaliwa, alidhuru Loliondo na kuunda Tume ya kutoa mapendekezo ya kumaliza mgogoro wa Loliondo na Sale. Mkuu wa Mkoa, aliteuliwa kuwa mweneyekiti wa Tume. Washiriki wengine ni pamoja na mashirika ya Umma ya uhifadhi, Wawekezaji na Jamii. | Kuundwa kwa Tume ya Pamoja baina ya Jamii na Wizara |
| Aprili 2017 | Tume ya Gambo kumaliza kazi ya kuandaa mapendekezo. | Taarifa iliwasilishwa kwa Waziri Mkuu lakini hadi sasa mapendekezo hayakufanyiwa kazi. |
| Julai, 2017 | Wananchi tukiwa tunasubiiri mrejesho toka ofisi ya Waziri Mku Operesheni ya kuchoma makazi ya wananchi na kuondoa mifugo katika eneo la Vijiji lenye km za mraba 1500 ilianza tena. | Ukiukwaji wa haki za binadamu kuendelea na mifugo zaidi ya 300 kutaifishwa |
| Agosti 2017 | Vijiji vinne (Ololosokwan, Kirtalo, Olorien na Arash kufungua kesi Mahakama ya Afrika Mashariki na kuomba zuio la mahakama ili uchomaji wa makazi kusimamishwa wakati kesi inaendelea. Mwezi Agosti 2018, Mahakama ilitoa zuio la mgogoro kuendelea wakati kesi inasikilizwa[51]. | Kusumbuliwa na kukamatwa waliofungua kesi |
| August 2018 | Kuomba zuio la mahakama kwa ajili ya kuzuia usumbufu wa waliofungua kesi na kuzuia operations zozote | Zuio lilitolewa na kuzingatiwa hadi mwaka hadi mwaka 2022 |


51 Reference No. 10 of 2017, Available at https://www.eacj.org/?page_id=5986&fwp_year=2017, visited on 9th May, 2022



| | | |
|---|---|---|
| Jan -Aprili 2022 | Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Ndg John Mongella alidhuru Loliondo na kukutana na viongozi wa Vijiji, kata na wa mila na kutangaza upya nia ya Serikali kumega ardhi ya Vijiji yenye ukubwa wa km. za mraba 1500 kwa kwa kile alichokidai kuwa maslahi ya Umma. Hoja kubwa ya wanchi ni kutafsiriwa vibaya kwa neno "maslahi ya ya umma" kwani sisi ni sehemu ya watanzania ambapo maeneo haya tumeyalinda na kutunza kwa gharama kubwa na hivyo maslahi hayo yanapaswa kwanza kutunufaisha sisi. | • Jaribio la Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori (TAWA) kuweka beacon katika ardhi ya kijiji cha Malambo hasa eneo la makazi na malisho Kitongoji cha Sanjan.<br>• Ziara ya Waziri Mkuu kutembelea Loliondo na kutoa fursa ya kuunda kamati ili kuwezesha kupatikana kwa maoni na mapendekezo ya wananchi kuhusiana na mpango wa uhifadhi endelevu katika eneo la km za mraba 1500- ikijumuisha Tarafa za Loliondo na Sale. |
| April 2022 | Waziri Mkuu alikubaliana na Ombi la Viongozi Wetu hasa Mh Mbunge na Mwenyekiti wa CCM Wilaya kuundwa kwa kamati yetu ya jamii ya kuandaa na kuchakata mapendekezo ya kutatua mgogoro huu | Kamati ya watu 35 ilindwa na kuanza kazi ya kuandaa taarifa ya mapendekezo |
| 24 May 2022 | Kuwasilisha taarifa zote mbili za Kamati ya Loliondo na Ngorongoro | |

### 3.1.4 Mapendekezo ya Kamati ya Mapitio ya Matumizi Mseto ya Ardhi ya Ngorongoro


Wizara ya Maliasili na Utalii katika jitihada za kumega ardhi ya Vijiji vya Loliondo na Sale, Mwaka 2019, iliunda kamati ya kufanya mapitio ya mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na kutoa mapendekezo ya namna ya maboresha uhifadhi ikiwa ni pamoja na kurekebisha mipaka na kuongeza maeneo mengine nje ya Mamlaka. Moja ya mapendekezo ya kamati ni kufanya marekebisho ya mipaka ya NCA na kuongeza maeneo ya Monduli, Sale, Longido na Loliondo ili kuboresha biashara ya utalii na uhifadhi ambapo ukubwa wa eneo ambalo lilipendekezwa ni kutoka kilomita za mraba 8,100 za sasa hadi 12,404. Mapendekezo hayo yaliongeza taharuki kwa wananchi wa Vijiji vya Tarafa za Loliondo na Sale juu ya ardhi ya vijiji ambayo ilikuwa na mgogoro kati ya Wizara hiyo na Malisali pamoja na Kampuni ya OBC.




***Ramani 3.3:*** *Ramani ya mapendekezo ya Kamati ya Ardhi Mseto Ngorongoro ikionyesha ardhi ya Vijiji vya Tarafa za Loliondo na Sale zliztopendekezwa kumegwa na kuwekwa chini ya NCA.*

Kamati ilipendekeza kumega ardhi ya Vijiji kwa upande wa Loliondo yenye ukubwa wa kilomita za mraba 1500. Ikumbukwe kuwa ardhi hii ya Vijiji imekuwa na mgogoro kati ya Wizara ya maliasili na Utalii, wananchi pamoja na kampuni ya uwindaji ya OBC kwa takribani miaka 30 bila suluhu. Mapendekezo hayo ya kamati yanalenga kuchochea mgogoro uliokuwepo na si kutatua kwa kuwa Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro ilishindwa kwa muda mrefu kutatua migogoro kati yake na jamii inayoishi ndani ya mamlaka.

Kwa upande wa Ziwa Natron ambapo inajumuisha Vijiji vya Kata za Engaresero na Pinyinyi, kamati ilipendekeza kumegwa ardhi ya Vijiji yenye ukubwa wa kilomita za mraba 2,804.14, ambayo itagusa pia maeneo ya Monduli na Longido kwa lengo hilo hilo la kuongeza eneo la NCA. Eneo hili pia ni ardhi halali ya Vijiji vilivyopimwa, kupata vyeti vya ardhi vya Vijiji (CVLs) na kufanya mipango ya matumizi ya ardhi ambapo ardhi yote imepangiwa matumizi. Vilevile katika maeneo ya makazi watu moja moja kwa kiasi kikubwa wamemilikishwa ardhi kwa taratibu za Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya 1999. Hivyo eneo hili kuingizwa kwenye mipaka ya Mamlaka ya Hifadhi ya ngorongoro ni kuvunja sheria za ardhi na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ibara ya 24.




***Ramani 3.4:*** *Ramani ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya iliyo kuwa iliyopendekezwa ikionyesha matumizi Kwa kanda ikiwemo eneo la Vijiji vya Loliondo vyenye Kilomita za mraba 1500.*

## 3.2 Jitihada za Kutatua Mgogoro wa Ardhi ya Loliondo

Mgogoro huu wa Loliondo ni mkubwa sana, ni mgogoro wa kitaifa na kimataifa. Awamu zote za Serikali, kuanzia awamu ya Pili zimekuwa na jitihada mbalimbali za kumaliza mgogoro huu. Awamu ya Nne na ya Tano ya Serikali ya Tanzania zilionyesha dalili iliyowekwa kwenye kumbukumbu hasa mitandao ya kijamii (angalia kielelezo namba 3.2) na vyombo vya Habari[52] za kutatua mgogoro huu. Aidha, maelekezo yao hayakuweza kufanyiwa kazi kwa wakati na muda wao wa uongozi ukawa umekwisha. Tulitegemea awamu ya tano au ya sita ya Serikali yetu kusimamia au kutekeleza maelekezo na ushauri wa awamu hizo.


Katika hali isiyokuwa ya kawaida, kila awamu imekuwa na utaratibu wa kushughulikia mgogoro huu bila kuzingatia historia na hatua zilizochukuliwa na awamu zilizopita.

52 https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/takukuru-yamshikilia-mkurugenzi-kampuni-ya-obc-2955912, imerejewa tarehe 3/5/2022

### 3.2.1 Jitihada za Rais Kikwete na Waziri Mkuu Mhe. Pinda

Zimekuwepo jitihada hasa zilizoonyesha kwa namna fulani serikali ilikuwa inaashiria kitu gani pamoja na kwamba ni baada ya makele yaliyopigwa na wananchi wa Loliondo na Sale na watetezi wa Haki za Binadamu ndani na nje ya nchi. Mfano mojawapo ni andika la Rais wa Awamu ya Nne aliyotuma katika mtandao wa Kijamii wa twitter akisema kwa kunukuu.

> *"There has never been, or will there ever be any plan by the Government of Tanzania to evict the Maasai people from their ancestral land". Kwa Kiswahili "Hakujawahi kuwa na wala hakutakuwa na mpango wowote wa serikali wa kuwafukuza watu wa jamii ya Kimasai kutoka katika ardhi ya mababu zao."*



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WAZIRI MKUU**

Anuani ya Simu "WAZIRI MKUU"
**Simu Nambari:** 2322904
e-mail: pm@pmo.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. **PM/P/1/569/29**

S.L.P. 980,
DODOMA

**30 Mei, 2013**

Mheshimiwa Magesa S. Mulongo,
Mkuu wa Mkoa wa Arusha,
S. L. P. 3050,
**A R U S H A.**

YAH: **MGOGORO KUHUSU ENEO LA PORI TENGEFU LOLIONDO (*LOLIONDO GAME CONTROLLED AREA*)**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009, na Tamko la Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu kupunguza ukubwa wa eneo la Pori Tengefu la Loliondo kutoka Kilomita za Mraba **4,000** hadi **1,500**, ni dhahiri kuwa Wananchi waliopo katika Vijiji vilivyo ndani ya Kilomita za Mraba **1,500** zilizotengwa kwa ajili ya uhifadhi kama nilivyovitaja, watatakiwa kuondoka katika maeneo hayo.

Kama utakavyoona, hapa ndipo penye tatizo kubwa. Kimsingi, Vijiji vyote hivi vimeanzishwa na Serikali na kupewa hadhi ya kuwa Vijiji, ingawa kwa mujibu wa Sheria ilibidi ardhi hiyo iondolewe kwenye hadhi ya Pori Tengefu kwanza kabla ya kuanzisha Vijiji hivyo. Kwa msingi huo, Vijiji hivi vimekuwa ni makazi ya Watu na kuwa na miundombinu ya kudumu ya kutoa huduma kwa Jamii. Hivyo, zoezi zima linalotarajiwa kufanywa chini ya Tamko la Wizara, litakuwa na athari kwa Wananchi hao na ustawi wao.

Wakati huo huo Waziri Mkuu Mizengo Pinda alitoa msimamo wa Serikali ya Awamu ya nne kuhusu Loliondo Mei 2013 kwa kuandika barua iliyotambua kuwa pamoja na kwamba nia ya serikali ni nzuri ukweli unabaki kuwa hii ni ardhi ya Vijiji na ni lazima kujipanga upya kama serikali kuona ni kwa njia gani maeneo haya yataifadhiwa bila kuathiri haki za wanavjiji wa eneo hilo. Baruah ii ilisitisha zoezi la kutwa eneo la km za Mraba 1500 kama ilivyo tangazwa na waziri wa Maliasili wa wakati huo , Balozi Hamisi Kagasheki.

***Picha 3.5:*** *Kielelezo cha barua ya Waziri Mkuu Mh. Pinda Juu ya msimamo wa Serikali kwa swala la Mgogoro wa Tarafa za Loliondo na sale tarehe 30/5/2013*

Pamoja na jitihada hizi zilizofanyika hasa katika awamu ya 4 ya uongozi wa Rais Kikwete hakuna suluhu ya kudumu iliyopatikana kutokana na ukweli kwamba kwa muda wote serikali na hasa Wizara ya Maliasili na mamlaka zingine za uhifadhi zimekuwa zikiegemea upande wa kampuni ya Uwindaji ya OBC kutokana na kile kinachoelezwa kuwa rushwa inayotolewa na kampuni OBC.

### 3.2.2 Jitihada za Rais Magufuli na aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii Kigwangalla

Aliye wahi kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii Mh. Dr. Kigwangalla aliwahi kunukuliwa na vyombo vya habari akidhibitisha haya na kusema kwamba Mkurugenzi wa OBC alimhonga mtangulizi wake (Prof. Maghembe) zaidi ya Dola laki mbili (200,000USD) na kwamba yeye (Mh Kigwangala) ni kijana mdogo angepewa dola laki moja tu[53]. Waziri Kigwangala chini ya uongoziwa wa Rais Magufuli ulifanikiwa kuthibiti rushwa na hila za kampuni hii dhidi thidi ya wananchi.

Mara zote jitihada za kutatua mgogoro huu zimekuwa zinakwama kwa kuwa chanzo cha mgogoro huu ambayo ni kampuni ya OBC imekuwa haiguswi katika jitahada za kutatua mgogoro huu hadi katika awamu ya Tano pale walipowajibishwa na Serikali na kupelekea uwepo wa hali ya amani na utulivu kwa muda. Awamu ya Tano chini ya Raias John Pombe Magufuli na Waziri wa Maliasili na Mkuu wa Mkoa wa Arusha , Mhe Mrisho Gambo walifanikiwa kwa kiasi kikubwa kuliko wakati mwingine wowote kutuliza mgogoro huu kwa kuchunguza malalamiko dhidi ya kampuni hii na kuchukua hatua za kisheria kama vile kuwatoa kwenye kitalu na kuwafungulia mashtaka ya uhujumu uchumi na rushwa. Wakati huu hali ya utulivu ilirejea eneo letu kwa kiasi kikubwa hadi pale kampuni hii iliporidishwa tena baadaye.

### 3.2.3 Makundi Mengine

Makundi mengi ya kijamii, jamii yenyewe pamoja na wadau wa maendeleo wameshiriki pia kwa njia tofauti tofauti kutafuta mwafaka wa mgogoro huu. Mashirika ya haki za binadamu na mashirika ya kifugaji yamekuwa yakijitahidi kutafuta njia mbalimbali za kutatua mgogoro huu bila kuadhiri maslahi ya uhifadhi na haki za watu. Wadau wa maendeleo pia kwa njia tofauti tofauti wamekuwa wakishauri na kusaidia njia mbalimbali za kutatua mgogoro huu. Ushiriki wa makundi yote haya pamoja na viongozi wa kiserikali na viongozi wa kijamii umesaidia kwa kiasi kikubwa kulinda eneo hili la vijiji lisiweze kupokonywa.

53 https://www.youtube.com/watch?v=W4pPfyK1GDY [Imerejewa 3/5/2022)

### 3.3 Madhara Yatokanayo na Jitihada za Kuchukua Ardhi ya Vijiji (sq km 1500) kwa Jamii

Wananachi wa tarafa za Loliondo na Sale hasa wale tunaoishi katika vijiji vilivyoko katika eneo lenye mgogoro tumekumbwa madhara makubwa kwa kipindi chote cha mgogoro huu. Jitahada nyingi zimekuwa zikifanyika kutaka kutuondoa katika maeneo yetu ya vjijiji hasa wakati wamiliki wa kampuni ya OBC wanapokuwa wamekuja nchini toka Falme za Kiarabu. Jitihada zote hizi za kutuondoa katika vijiji vyetu zimekuwa zikileta taharuki, hofu, ukiukwaji wa haki za binadamu, madhara kiuchumi, kimila na kijamii kama inavyofafanuliwa katika sura hii ndogo.

#### 3.3.1 Ukiukwaji wa Haki za Binadamu

Katika sakata hili la kutuondoa kwa nguvu katika maeneo ya Vijiji vyetu kwa nyakati tofauti (2009, 2013, 2014 na 2017) kumesababisha ukiukwaji mkubwa wa haki za wenyeji[54]. Aidha, ilitokea vifo vingi vya mifugo kwa kukosa malisho, maji na mengine kupotea. Ukiukwaji wa haki za binadamu katika eneo hili ambalo limeandikwa kwa wingi kwa miaka 30 sasa na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi kama inavyoonekana katika orodha ya marejeo ya taarifa hii. Kwa kuonyesha upana wa tatizo operation yani mwaka 2017 pekee zinaonyesha watu 138 waliweza pata changamoto mbalimbali kama inavyowasilishwa katika jedwali Namba 3.3.

***Jedwali 3.3:*** *Idadi ya wananchi wa Loliondo waliokamatwa na kuteswa Julai na Novemba 2017.*

| Na | Kijiji | Idadi ya watu waliokamatwa na kuteswa | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| | Ololosokwan | 12 | 4 | 16 |
| | Kirtalo | 11 | 2 | 13 |
| | Oloipiri | 40 | | 40 |
| | OLoosoi-to-Ngobereti | 21 | 6 | 27 |
| | Arash | 32 | 10 | 42 |
| **Jumla** | | **116** | **22** | **138** |

*Chanzo: PINGOs Forum (2017)*

54 View from the Termite Mound: Article about Loliondo land threats on Just Conservation's website (termitemoundview.blogspot.com)

### 3.3.1.2 Kuchomwa kwa Makazi na Mali za Wananchi

Katika matukio mengi yaliyokiuka haki za binadamu, uchomaji wa makazi na mali za wananchi ni moja moja ya matukio makubwa yaliyofanywa vyombo vya dola katika maeneo yetu. Makazi katika Maisha yetu ya kimila ni zaidi ya tafsiri ndogo inayofahmika kuwa makazi ni nyumba kisasa pekee. Makazi katika jamii yetu hujumuisha hadi maeneo ya kuhifadhia mifugo, ndama na mazingira yanayozunguka na kupelekea kuharibu mfumo wa maisha yetu. Imekuwa vigumu kupata takwimu za miaka yote ya mgogoro lakini takwimu za Mwaka 2017 zinaonyesha kati ya maboma 4698 maboma 1190 zilizochomwa. Kuchomwa kwa maboma haya kumepelekea robo ya wananchi wote wanaoishi katika eneo hili kuadhirika pamoja na mali zao ambazo nyingi za thamani za kimila.




***Picha 3.6:*** *Makazi ya wafugaji wa Loliondo yaliyochomwa moto wakati wa operesheni*

### 3.3.1.3 Kupigwa na Kuteswa

Operesheni zote nne (2009, 2013, 2014 na 2017) zimepelekea kwa wananchi kupigwa, kuteswa na wengine kuwa vilema kutokana na matumizi ya silaha za moto. Ni muhimu kufahamika kuwa wakati wote wa manyanyaso haya kama wananchi hatukuwahi kufanya jitahada zozote za kujitetea kwa njia za kupambana au kuchukua sheria mkononi. Mifano ya watu waliopata changamoto hizi kati ya wengine ni pamoja na Ngodidio Rotiken wa Kijiji cha Kirtalo 2009, na Parmoson Oloso wa Ololosokwan, 2017. Wakati mwingine serikali inatumia nguvu kubwa kuwaondoa wananchi katika eneo lao la vijiji hadi kutumia risasi za moto kinyume na sheria.



***Picha 3.7:*** *Parmoson Ololoso ( kushoto): wa Kijiji cha Olosokwan aliyepigwa risasi katika operesheni ya 2017 na maaskari waliokuwa wanafanya operesheni pamoja Ngoididio Rotiken (kulia) alipigwa risasi ya jicho na kikosi maalum cha polisi mwaka 2009*

### 3.3.1.4 Vitisho , Kukamatwa na Kubambikizwa Kesi

Katika operesheni zote au jitiahda zote za kutaka kutuondoa katika maeneo yetu, tumeshuhudia wenzetu wengi wakikamatwa na polisi na kubambikizwa kesi. Wananchi wenzetu wamekuwa wakikamatwa na kupelekwa katika vituo na polisi na wakati mwingine katika mahakama zilizoko nje ya Wilaya kama kule Mugumu Wilaya ya Serengeti. Kwa operesheni zote za miaka yote minne takriban zaidi ya watu 200 walikamatwa na kupelekwa katika vituo vya polisi na wengine kushtakiwa kabisa. Kwa mfano kwa nusu ya mwaka 2022 pekee zaidi ya watu 20 wameshakamatwa na wengine kutakiwa kurepoti mara kwa mara katika vituo vya polisi.

Matukio haya ya vitisho, kamatakamata na kubambikziwa kesi yamekumba zaidi wananchi, viongozi wao wa kisia, viongozi wa kimila, waandishi wa habari, mawakili na watetezi wa haki za binadamu[55]. Baadhi ya watetezi na viongozi wa wananchi wamefikishwa katika vituo vya polisi na wengine kutishiwa, kuhojiwa au kufunguliwa kesi za uchochezi. Lengo la vitisho kwa watetezi ni kutaka kuwanyamazisha wasidai au kushiriki katika kutafuta suluhu ya mgogoro huu wa ardhi hasa kwa upande wa wananchi.

55 THRDC (2016) Taarifa kwa Umma Kuhusu Kukamatwa Bwana Samweli Nangira, Mkurugenzi wa Shirikla La Ngonet-Loliondo

Vitisho hivyo kwa wanaharakati, waandishi wa habari na viongozi vimeleta tishio na taharuki kwa wananchi na kutukosesha uhuru wa kufanya majukumu yetu na kujadili mambo yanayohusu utetezi ambayo ni haki yetu kikatiba.



***Picha 3.8:*** *Mawakili wakiandamana baada ya wakili mwezao kukamatwa Loliondo akiwa katika majukumu yake ya uwakili (Wakili Shilinde Ngalula wa LHRC, akiwa anawatetea watu waliokamatwa Mahakama ya Wilaya, Ngorongoro.)*

Kwa mujibu wa Taarifa mbalimbali za THRDC, shirika ambalo limekuwa likitetea watetezi wa Loliondo wakati wote wanapokuwa katika shida zinaonyesha kuwa zaidi ya watetezi 100 wa kijamii wamekuwa wakisumbuliwa, wakitishiwa na kukamatwa kutokana na wao kuongoza wananchi kutetea ardhi yao[56]. Pia mashirika mengi ya kifugaji ya Loliondo yamekuwa yakitishiwa mara kwa mara hadi kufikia hatua ya kukimbia Loliondo na kwenda kufanyia kazi wilaya zingine za kifugaji. Haki za watetezi, wanasheria wanaoenda kutoa uwakilishi wa wateja wao na mashirika ya haki za binadamu zimekuwa zikivunjwa sana katika mgogoro huu wa Loliondo.

Vitisho, manyanyaso na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu uliendelea kuwa mkubwa hadi kupelekea Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) tarehe September 4, 2017, kutoa zuio la muda kusitisha operesheni ya kuwaondoa kwa nguvu wananchi katika maeneo wanayoishi na kuwachomea makazi (maboma) yao katika eneo la Loliondo wilayani Ngorongoro, ili kulinda haki za pande zote. Aidha mwenyekiti wa Tume hiyo, alisema Tume imeanza kufanya uchunguzi wa malalamiko hayo na kwa mujibu wa taarifa za wananchi hao.

56 THRDC (undated) Tamko kwa Umma Juu ya Hali ya Watetezi wa Haki za Wafugaji Loliondo

Katika operesheni iliyoanza Agosti 12 iliyotekelezwa kwa pamoja na uongozi wa Wilaya ya Ngorongoro, askari wa wanyamapori kutoka Hifadhi ya Taifa Serengeti (Senapa), Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCA) na Jeshi la Polisi kulikuwepo na uvunjwaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Wananchi hao wanadai wameondolewa kwa nguvu katika vijiji vyao halali vinavyotambuliwa kisheria, wamechomewa makazi yao isivyo halali na mifugo yao kuchukuliwa.



***Picha 3.9:*** *Jeshi la polisi lilipokuwa linadhibiti maandamano ya wananchi baada ya maakazi yao kuchomwa moto*

Wakati huo huo Mashirika ya haki za binadamu pia kwa nyakati tofauti waliweza tembelea maeneo ya Loliondo na kubaini ukikwaji wa haki za binadamu na kukemea. Safari ya Kwanza ilifanyika mwaka 2009 chini ya uratibu wa Mtandao wa Fem-Act na safari ya pili ilifanyika chini ya uratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC). Kwa nyakati zote mashirika ya kifugaji kama UCRT, PINGOs Forum, NGONET na PWC walikuwa mstari wa mbele kuibua ukiukwaji wa haki katika eneo la loliondo. Kwa taarifa zaidi kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu tembelea taariza zilizotolewa na mashirika tajwa hapo juu.

#### 3.3.1.5 Wananchi wa Tanzania kuitwa Wahamiaji kutoka Mataifa ya Jirani

Kwa zaidi ya miongo miwili vyombo habari na baadhi ya viongozi wa Serikali kwa nyakati tofauti vimeendelea kuripoti kuwa asilimia kubwa ya watanzania waishio katika tarafa hizi ni wahamiaji kutoka nchi mbalimbali zikiwemo Kenya na Sudan ili kuwatishia katika harakati za kudai haki zao za ardhi. Mfano Gazeti la Jamhuri lilikuwa likitumika kuandika matukio haya ya kusema watanzania wa Loilondo ni wakenya ili kulinda maslahi ya mwekezaji wa OBC. Kwa miaka mingi sasa OBC pamoja na Wizara ya Maliasili na

utalii wamekuwa wakitumia baadhi ya vyombo vya habari katika kufanya propaganda za kupotosha taarifa za ukweli kuhusu loliondo, ambapo imepelekea watu wengi kukamatwa na kusababisha kuchochea mgogoro zaidi. Zaidi ya asimilia 70% ya watu wa loliondo wametuhumiwa kuwa ni wakenya nasio raia wa Tanzania.



# Loliondo yageuzwa Kenya

Jamhuri · November 28, 2014 · 0 ·
5 min read

*Siri sasa yafichuka, asilimia 70 si Watanzania
*Uhamiaji Mkoa Arusha lawamani kwa rushwa

***Picha 3.10:*** *Kichwa cha Habari cha Gazeti la Jamhuri la mwaka 2014*

### 3.3.2 Madhara ya Kiuchumi kwa Wananchi

Kila jamii ya kitanzania inafahamika inategemea shughuli zipi katika kujiwezesha kiuchumi ambayo kwa sisi wafugaji shughuli kuu ya kiuchumi ni ufugaji asili. Eneo hili la Vijiji lenye mgogoro linategemewa kwa asilimia 90 kwa malisho ya mifugo katika Vijiji vyote vya Tarafa za Loliondo na Sale hasa katika Kata Nane zenye Vijiji zaidi 23 na mifugo takriban 973745. Mifugo imekuwa ikiondolewa kwa nyakati tofauti za operesheni katika eneo la mgogoro. Kama inavyofahamika katika jamii ya kimasai kuwa kitega uchumi chetu ni mifugo hii ni dhairi kuwa Operesheni hizo zilisababisha anguko kubwa la kiuchumi katika jamii yetu kwani ufugaji ndiyo shughuli kuu ya kiuchumi. Operation zote zimekuwa zikitekelezwa nyakati ngumu za kiangazi kitu ambacho inatupelekea tuamini kuwa ina nia yake ni kutufisili kiuchumi.



***Picha 3.11:*** *Makazi ya wenyeji wa Loliondo yakiungua moto na wenyeji wakijaribu kuokoa baadhi ya mali.*

### 3.3.2.1 Ukamataji wa Mifugo

Operesheni hizo pia ziliambatana na ukamataji wa mifugo nje ya eneo la Hifadhi ya Serengeti kwa kuwa kulikuwa ushirikiano wa maaskari wa SENAPA na Kampuni ya OBC ambayo ilikuwa inafanya hujuma na uchochezi katika mgogoro. Mwaka 2017, mifugo 290 zilikamatwa pamoja na watu 6 na kufunguliwa mashtaka katika Mahakama ya Wilaya ya Serengeti iliyoko Mugumu, kwa kesi ya jinai Na. 187 ambapo baada ya wananchi kutoridhika na maamuzi walikata rufaa kwenda mahakama kuu kanda ya Mwanza, ambapo walifungua shauri la jinai kati ya Noonkirimban Seret Sironga v. Republic[57]. Tarehe 11/01/ 2018 Mahakama ilitoa hukumu ya ushindi kwa wananchi na Hifadhi ya Sengeti iliamuriwa kurudisha mifugo ya wananchi iliyokuwa imetaifishwa kwa wamiliki halali.

57 (HC-Mwanza) Criminal Appeal No.387 of 2017

***Jedwali 3.4:*** *Idadi ya mifugo iliyokamatwa, kupigwa fini, kutaifishwa na kupigwa risasi*

| **Na** | **Kijiji** | **Idadi ya Kaya** | **Idadi ya Mifugo iliyo kamatwa** | **Idadi iliyotozwa faini** | **Idadi iliyotaifi-shwa** | **Idadi ili-yopigwa risasi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ololosokwan | 1300 | 4,150 | 3,522 | 628 | |
| | Kirtalo | 80 | 3,000 | 3,000 | | |
| | Oloipiri | 320 | 3,245 | 3,245 | | |
| | OLoosoi-to-Ngobeleti | 324 | 3,930 | 3,760 | | 170 |
| | Arash | 430 | 5,060 | 4,037 | | 1023 |
| **Jumla** | | **2,454** | **19,385** | **17,564** | **628** | **1,193** |

***Chanzo:*** *Pingos Forum (2017)*

### 3.3.2.2 Wananchi kukosa Mapato Kutokana na Mgogoro wa Kampuni ya OBC

Kabla ya mgogoro huu uliosababishwa na kampuni ya OBC kutokea katika eneo la tarafa Loliondo na Sale, vijiji vilikuwa vikijishughulisha na biashara ya utalii wa picha na kupata mapato. Kutokana na mgogoro huu makampuni hayo ya kitalii yaliondoka na hivyo kuathiri fursa na huduma za kijamii kama elimu, afya na ajira zilizokuwa zinatolewa kutokana na manufaa ya uwepo wa shughuli hiyo ya kitalii. Takribani makampuni 5 ziliondoka katika eneo la vijiji kwa sababu ya kampuni ya OBC na kusababisha hasara kubwa kwa vijiji kwa kukosa mapato, zaidi ya wanafunzi waliokatiza masoma na miradi mingi ya afya, maji kusimama na kusababisha wananchi kuchangishwa tena kwa ajili ya kumalizia.




***Picha 3.12:*** *Baadhi ya picha za mikutano ya wananchi wakipinga ardhi ya Vijiji vyao kumegwa kwa maslahi ya Kampuni ya OBC.*

Pamoja na rasilimali za vijiji kuendelea kuvunwa na kampuni ya uwindaji ya OBC, vijiji kutoka tarafa hizi hazikunufaika na uwepo wa kampuni hii ya uwindaji. Baadhi ya kampuni ambazo zilisitisha shughuli zao kutokana mgogoro huu ni zaidi nne (4) kama zinavyoonekana katika jedwali hapo chini.

***Jedwali 3.5:*** *Baadhi ya Kampuni zilizoondoka kutokana na mgogoro wa OBC*

| Na | Kampuni | Kijiji |
|---|---|---|
| 1 | NOMAD TANZANIA | Ololosokwan na Piyaya |
| 2 | SOKWE COMPANY LIMITED/ ASILIA | Ololosokwan na Piyaya |
| 3 | WILDLIFE EXPLORER | Arash, Piyaya |
| 4 | DOROBO TOURS & SAFARIS | Oloipiri, Oloirien/ magaiduru, Maaloni/Olosoto, na Arash |
| 5 | ROYAL AFRICAN SAFARIS | Soitsambu |

### 3.4 Mgogoro wa Vijiji na Kampuni ya Thompson Safari /TCL

Kampuni ya utalii wa Thompson Safari ya Boston, nchini Marekani iliwekeza katika kijiji cha Sukenya, Mondorosi na Soitsambu Kata ya Oloipiri na Soitsambu, Tarafa ya Loliondo. Eneo hili lenye ukubwa wa ekari 12,617 lilichukuliwa awali mwaka 1984 na serikali kwa ajili ya kuzalisha shairi kupitia shirika la Tanganyika Breweries Limited (TBL). Utwaaji wa eneo hili iligubikwa na rushwa na kuwa chanzo cha mgogoro unaoendelea hadi sasa. Thompson safaris ilinununa shamba hilo kwa kupitia kampuni yake tanzu ya Tanzania Conservation Limited (TCL), katika tenda iliyokiuka taratibu za kisheria. Mgogoro huu umekuwa ukijaribu kutatuliwa kwa njia za kisiasa na hatimaye kushindikana na kupelekwa mahakamani. Uhasama huu umesababisha ukiukwaji wa haki za binadamu kutokana na kampuni kutumia vyombo vya dola kuwachomea makazi na kuwapiga wanajamii[58].

58 Land Case No. 15 of 2011 (HC-Arusha)

SURA YA
NNE

# UCHAMBUZI WA HOJA ZA SERIKALI

## 4.0 UTANGULIZI

Sura hii inaeleza na kuchambua kwa kina hoja ambazo zimekuwa zikiwasilishwa na upande wa Serikali juu ya eneo la Vijiji vya Tarafa za Loliondo na Sale lenye kilomita za mraba 1500 kwa nyakati na awamu tofauti za uongozi wa nchi. Hoja hizi zimekuwa zikitolewa kama sababu ya kumega eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 1500 toka ardhi ya vijiji. Mgogoro huu umekuwa ukichukua sura tofauti kadri muda ulivyo kwenda ambapo viongozi mbalimbali wa Serikali pia wamekuwa wakitoa misimamo inayotofautiana na wananchi wakitoa misimamo yao.

### 4.1 Hoja ya Ushoroba

Serikali imekuwa ikisema mara kwa mara kuwa inapenda kumega eneo la km za mraba 1500 ili kulinda eneo hili ambalo ni mapitio na mtawanyiko wa wanyama. Mzunguko wa Nyumbu wahamao kutokea Masai Mara (nchini Kenya) kuja uwanda wa Serengeti hupita mashariki mwa hifadhi ya Serengeti pamoja na Ardhi ya Vijiji katika Tarafa za Loliondo na Sale, kusini katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCA) na magharibi mwa Hifadhi ya Taifa Serengeti.

#### 4.1.1 Uchambuzi wa Hoja za Serikali

Uhamaji wa wanyama hawa umekuwepo kwa muda mrefu hata wakati Wamaasai wakiishi Moru- ndani ya hifadhi ya Taifa ya Serengeti (kabla ya kuondolewa kwa mara ya kwanza) na maeneo mengine yote wanayopitia wanyama ambayo ni nje ya eneo lenye mgogoro. Vichocheo vikuu vinavyoongoza uhamaji wa nyumbu na wanyama wengine kama Swala, Pundamilia nk ni uwepo wa mvua na malisho. Jamii inaona kuwa uwepo wa jamii na mifugo haina madhara kwa mzunguko wa Wanyama kwa sababu zifuatazo:

- Kama inavyofahamika kuwa jamii ya kimaasai imekuwa na utaratibu wa jadi wa kupisha nyumbu kwa sababu mbili, mosi nyumbu wanaambukiza magonjwa mbalimbali na kusababisha vifo vya mifugo. Watafiti na wataalamu wa wanyamapori wameshindwa kuelewa/ au kwa makusudi jinsi tunavyotumia maeneo haya kwa pamoja kwa karne nyingi hadi sasa.

- Ni muhimu kujua kwamba eneo hili kwa kawaida lina matumizi mseto kati ya binadamu, mifugo na wanyama pori kabla na baada ya uhuru. Mfumo huu ni jumuishi, shirikishi na rafiki kati ya jamii na uhifadhi. Kwa muda wote mifugo, binadamu na wanyama pori wameishi pamoja bila madhara kwa kuwa maslahi ya pande zote yanazingatiwa na kuheshimiwa kwa taratibu za mila na desturi za jamii husika kama ilivyofafanuliwa katika sura ya pili ya taarifa hii.
- Kwa kipindi cha kuhama kwa nyumbu wafugaji huondoa mifugo yao ili kupisha wanyama kwani wanaweza kusababisha madhara ya magonjwa na wakati mwingine kuondoka na mifugo na kupotea kwa kuwa wanahama kwa makundi makubwa.
- Ifamike pia kwamba wanyama pori hupenda kuishi maeneo yaliyoko karibu na makazi kwa sababu za kiusalama na hivyo kujenga mahusiano mazuri na watu kama ilivyoelezwa kwenye Sura ya pili.
- Hata mapitio na mtawanyiko wa wanyama upo karibu maeneo yote ya Tarafa za Sale na Loliondo.Hivyo sio vyema kusema ni eneo tu la km za mraba 1500 ndio wanyama wanapita.

### 4.1.2 Maoni Yetu

- Jamii itaendelea kuheshimu utaratibu huu kwa kupitia mila na desturi pamoja na mipango ya matumizi bora ya ardhi za vijiji ambayo kwa mujibu wa Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Na. 6 ya 2007, maslahi ya sekta zote zinazingatiwa kwa kupitia mamlaka za upangaji ikiwa ni pamoja na Vijiji (VC, VGA na VLUM) na kwa ushauri wa timu ya wataalamu wa mpango wa matumizi ya ardhi ya Wilaya (PLUM).
- Tupo tayari kutumia wataalamu wetu pamoja na wataalamu wa serikali kuendelea kufanya tafiti jumuishi za mara kwa mara ili kubaini changamoto zinazojitokeza na kufanyia kazi ili kulinda mali asili pamoja na haki zetu kama wafugaji.
- Hoja ya kutenga km za mraba 1500 kwa ajili ya mapitio ya wanyama haiwezi kujitosheleza kwa kuwa mtawanyiko wa wanyama upo maeneo mengi ya wilaya.

## 4.2 Hoja ya Mazalia ya Wanyama

Kwa kipindi kirefu kumekuwa na mjadala na hoja kutoka Wizara ya Maliasili na wahifadhi kwamba eneo hili ni eneo ambalo wanyamapori huzaliana. Na hivyo kudai wananchi katika ardhi ya vijiji waondolewe ili kuacha Wanyama wazaliane na wakati mwingine ili watalii waweze kuja kuwinda bila usumbufu wa mifugo na wananchi waishio maeneo hayo.

#### 4.2.1 Uchambuzi wa hoja ya Mazalia ya Wanyama

Ifahamike kuwa katika hili, wanyamapori ambao huzaa kwa makundi makubwa na kwa wakati mmoja ni nyumbu, pundamilia na swala. Wakati wa kuzaliana kwa nyumbu wafugaji wanahama na mifugo yao yote kwa muda wa miezi zaidi ya 5 (Disemba hadi Aprili) ili kuruhusu nyumbu wazae na ndama kupoteza manyoya. Hii ni kwa sababu manyoya, kondo na utando (inkipa kwa Kimasai) ya nyumbu husababisha homa kwa mifugo ijulikanayo kwa lugha ya kiingereza kama Malignant Catarrhal Fever (MCF) isiyo na tiba na kupelekea vifo vingi kwa mifugo.

#### 4.2.2 Maoni Yetu

Kwa maneno mengine wafugaji hupisha maeneo yao ili nyumbu wazaliane na baada ya muda wanarudi kulisha katika maeneo haya baada ya hatari ya ugonjwa kutoweka. Utaratibu huu unaeleweka na kuheshimiwa na wafugaji wote. Sisi wafugaji tutaendelea kutambua, kuheshimu na kudumisha utaratibu huu wa mahusiano baina yetu na wanyamapori ambayo imekuwepo tangu enzi za babu zetu hadi sasa ikiwa ni sehemu ya uhifadhi endelevu.

### 4.3 Hoja ya Eneo la 1500 kuwa ni Eneo la wazi na si Ardhi ya Vijiji

Kumekuwa na hoja kutoka serikalini kwamba eneo hili ni eneo la wazi hakuna makazi na wala haalitumiki kwa namna yoyote na hivyo hata likimegwa hakuna watu watakao athirika. Wakati huo huo Serikali imekuwa ikidai eneo loto la lenye ukubwa wa kilometa za mraba 4000 si eneo la vijiji bali eneo la hifadhi.

Changamoto inayochangia mgogoro wa ardhi wa Loliondo kuendelea kuwa mkubwa ni kuhusu uelewa au msimamo wa baadhi ya viongozi wa serikali hasa Wizara ya Maliasili kuhusu eneo lote la liliolikuwa pori tengefu la loliondo na sale. Kwa muda mrefu kumekuwepo na mitazamo tofauti ndani ya taasisi za serikali au viongozi wan chi kuhusu hadhi ya kisheria ya eneo la Loliondo na sehemu ya Sale. Baadhi ya viongozi wanaamini km za mraba zote 4000 zinazochukua Tarafa ya Loliondo yote na Sehemu ya Sale ni pori tengefu pekee na hakuna ardhi ya Kijiji au ardhi ya wananchi wanayo miliki kimila au kisheria.

(a) Kutoa zawadi ya Ardhi kwa wananchi

Hivi karibu viongozi hasa Waziri wa Maliasili amenukuliwa mara kadhaa akisema wananchi wa Tarafa ya Loliondo na Sale, wanaopatikana katika eneo lenye km za mraba 4000 hawana ardhi wanayo miliki mmoja mmoja au kama Kijiji. Kwa mtazamo wao ni kwamba eneo lote la Loliondo ambalo

lilikuwa ni pori tengefu ndani ya ardhi ya vijiji kabla kutungwa kwa sheria ya wanyamapori ya mwaka 2009 sio ardhi ya vijiji. Mtazamo huu hauja zingatia historia nzima ya Tanzania, Ngorongoro na hasa jamii ya kimasai ambayo wamekuwa katika eneo hili kwa miaka zaidi ya 1000 sasa.

Serikali kupitia Waziri wa Maliasili nyakati zote imekuwa ikinukuliwa ikisema katika hizo km za mraba 4000 ambazo kwa sasa ndio aneo zima la Loliondo na sehemu ya Sale watatoa zawadi ya km za mraba 2500 kwa wananchi na kuchukua km za mraba 1500 kwa ajili huifadhi pekee[59]. Hili eneo za Km za Mraba 1500 ndio ambalo kwa sasa zinatumika kama kitalu cha uwindaji cha kampuni ya OBC na wakati huo huo ndio ardhi ya kata nane inayotumika kama nyanda za malisho ya mifugo.

(b) Kulinda uhifadhi

Serikali pia imekuwa ikisistiza kuwa ni lazima kuzichukuwa kabisa hizo km za mraba 1500 kwa malengo ya kuhifadhi mazingira, mapitio ya Wanyama na vyanzo vya maji vinavyotumika na Wanyama hadi katika mbuga ya Serengeti. Eneo hili la 1500 ndio pia eneo ambalo mapitio ya Wanyama toka Masai Mara kuja Serengeti na Ngorongoro yalipo. Msimamo wa Serikali umekuwa ni lazima shughuli za kibinadamu ziondolewe kabisa katika neo hili na kufanya sehemu hii kuwa sehemu ya hifadhi.

### 4.3.1 Uchambuzi wa Hoja ya Kuwa Eneo la 1500 km za Mraba si la Vijiji

Baada ya mikutano na majadiliano mengi ya wananchi kuhusu hoja hii ya hadhi ya ardhi yao kisheria, na kwa kupitia wanasheria wa kijami, msimamo wa sasa wa wananchi wa Loliondo ni kuwa kwa sasa Loliondo hakuna tena Pori Tengefu baada ya Mabadiliko ya Sheria ya Mwaka ya 2009. Wananchi wanaamini eneo lote la km za mraba 4000 kwa sasa hazina tena hadhi ya pori tengefu kama Sheria ya 2009 ilivyoagiza kuwa hakutakuwa tena na ardhi ya Kijiji itakayokuwa na mapori tengefu. Sheria iliagiza kuondelewa kwa mapori tengefu katika maeneo yote yenye ardhi za vijiji. Soma zaidi sura ya pili ya taarifa hii kuelewa uchambuzi wa kijamii kuhusu uhalali wa ardhi yenye mgogoro kwa sasa. Hoja zetu zingine kuhusiana na hoja hii kama ifuatavyo;

- Ni muhimu serikali na jamii ya watanzania kuelewa kuwa kihistoria eneo hili halikuwahi kuwa wazi tangu enzi za mababu, wakati wa Ukoloni, baada ya Uhuru hadi sasa kama ilivyoonyeshwa katika Sura ya pili ya taarifa hii. Sura hii imeeleza kwa kina hadhi ya ardhi ya Vijiji

59 See this link; https://www.maliasili.go.tz/highlights/view/government-clarifies-on-decision-to-provide-huge-tracks-of-land-to-loliondo, imerejewa tarehe 21 Mei, 2022

vya Tarafa za Loliondo na Sale lenye kilomita za Mraba 1500 kisheria kwa vipindi tofauti za tawala mbalimbali kuanzia kabla ya wakoloni na baada ya uhuru kwa kuzingatia uchambuzi wa Sheria mbalimbali za Ardhi, wanyama pori, Serikali za Mitaa na za malisho.

- Pia viongozi wa awamu zote zilizopita kuanzia Maraias, Mwaziri wakuu wameendelea kutambua kuwa ardhi yenye mgogoro ni ardhi ya vijiji lakini yenye rasilimali za umma (Wanyama)

- Kabla ya uhuru wananchi walikuwa wanakalia na kutumia maeneo hayo kimila ambapo walipata haki ya kisheria na ndiyo maana wakoloni miaka 1940-1950 walipokuwa wanataka kuanzisha hifadhi ya Serengeti walikuwa na majadiliano ya muda mrefu na viongozi wa mila wawakilishi wa jamii na hatimae kuingia makubaliano ya kuhama mwaka 1958, ambapo inathibitisha pasipo shaka kuwa hiyo ilikuwa ni ardhi yao na walikuwa wakimiliki kimila.

- Vilevile baada ya uhuru, Vijiji hivi vimeendelea kutambuliwa na Serikali kwa kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria mbalimbali ikiwa ni pamoja na Sheria ya Serikali za Mitaa [Mamlaka za Wilaya] Na.7 ya 1982, kupimwa na kupatiwa hati/vyeti kwa mujibu wa Sheria za ardhi ya 1923, na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya 1999. Soma zaidi sura ya pili ya taarifa hii.

### 4.3.2 Maoni Yetu

Kutokana na uchambuzi na historia ya kisheria ya eneo la Loliondo na Sale, na pia kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyama Pori ya 2009 ni wazi kuwa ardhi yote ya sale na loliondo ni ardhi za vijiji. Wakati huo huo ni ukweli usiopingika kuwa km za mraba 1500 ni ardhi ya vijiji na ni eneo muhimu sana la Vijiji kwa matumizi ya mifugo na pia watu.. Kwa kutambua maslahi mapana ya uhifadhi na pia Maisha ya wafugaji wa eneo hili tuna maoni yafuatayo:

- Serikali kwanza itambue kuwa eneo lote la tarafa za Sale na Loliondo kwa sasa ni maeneo ya vijiji kutokana uchambuzi na historia tulionyesha katika sura pili ya taarifa hii.

- Serikali pia itambue kuwa baada ya kutungwa kwa sheria ya wanyama pori ya mwaka 2009, kwa sasa hakuna tena pori tengefu katika ardhi ya vijiji vya Sale na Loliondo

- Mchakato wa kurejewa kwa mipango ya matumizi ya ardhi ya Vijiji ifanyike kwa haraka ili kuanisha matumizi ya ardhi katika Vijiji vyote itakayokidhi matakwa na maslahi ya wananchi, mifugo na wanyamapori.


- Kudhibiti ongezeko la watu kutoka nje ya wilaya katika mji mdogo wa loliondo ili kutoa nafasi ya wananchi wa maeneo yanayozunguka km za mraba 1500 kusogea katika mji huu ni kufanya biashara.

### 4.4 Hoja ya Kulinda vya Vyanzo vya Maji

Serikali imekuwa na hoja kuwa ni vyema kuchukua eneo la km za mraba 1500 na kufanya kuwa eneo pekee la uhifadhi kwa lengo la kulinda vyanzo vya maji vinavyotumika na Wanyama na pia kupeleka maji Hifadhi ya Serengeti na kulinda eccologia ya serengeti-mara. hata hivyo kumekuwepo na hoja ya serikali kuwa uharibifu wa vyanzo vya maji  unatishia uwepo na uendelevu wa ikolojia ya Ngorongoro, Serengeti-Mara kitu ambayo sio kweli.

#### 4.4.1 Uchambuzi wa Hoja ya Kulinda Vyanzo vya Maji

- Serikali haijawahi kutoa takwimu ya vyanzo vilivyokufa au kuharibika kwa sababu ya uwepo wa jamii ya wamaasai katika eneo hili kwa.
- Ni muhimu kusisitiza kuwa kwa kipindi chote cha maisha ya jamii kabla na baada ya Uhuru suala la ulinzi na utunzaji wa vyanzo vya maji limepewa kipaumbele kikubwa kwa taratibu za kimila kwa kuwa ni uhai wa binadamu, mifugo na wanayamapori.
- Miaka ya 1990 na 2000 Vijiji viliweka utaratibu wa kulinda vyanzo vya maji kwa kutumia Sheria Ndogo za Vijiji ambavyo vimeweka nguvu kubwa katika kuthibiti uharibifu wa vyanzo vya maji kwa maendeleo endelevu kama ilivyoelezwa kama sura ya sura ya pili.
- Mwaka 1992 Serikali ilitoa leseni ya uwindaji kwa Kampuni ya OBC ambapo ilijenga kambi za kudumu Kijiji cha Soitsambu/Kirtalo kwa sasa kwenye chanzo cha Mto Olasae  na kupelekea maji  kupungua kwa asilimia kubwa. Kuharibiwa kwa chanzo cha mto huu haukuwahi kuchukuliwa hatua yeyote na serikali dhidi ya mwekezaji huyo na badala yake, kumekuwepo na hoja ya uharibifu wa vyanzo vya maji na lawama lukuki kwa wananchi waliotunza kwa karne nyingi sana zilizopita.
- Hata hivyo kuna mito michache sana inayopeleka maji katika hifadhi ya serengeti. Wakati huo huo inafahamika kuwa mito mingi huanzia katika ukanda wa juu ya Loliondo hivyo kama lengo ni kulinda vyanzo vya maji kwa kuchukua km za mraba 1500 haitakuwa na uzito wowote kwa hoja hii. Rejea ramani ya vyanzo vya maji katika Tarafa ya Sale na Loliondo hapa chini;




***Ramani 4.1:*** *Ramani inayoonyesha mito katika tarafa za Loliondo na Sale*

Ramani hii inaonyesha kuwa hakuna mito mingi inayotoka katika eneo la km za mraba 1500 kupeleka maji katika Hifadhi ya Serengeti. Mito mingi ambayo serikali imekuwa ikitaja kama vyanzo vya haiendi serengeti zaidi ya Mto Pololeti kama inavyoonekana kwa ramani na nyingine zinaanzia nje ya eneo hili.

### 4.4.2 Maoni Yetu

- Jamii kwa maslahi yake na za kiikolojia, itandelea kushirikiana na serikali kuweka mifumo ya ulinzi na usimamizi wa vyanzo vya maji katika maeneo yenye vyanzo vya maji.
- Hoja ya kuondoa watu ili sheria za maji ziwezi kufanya kazi ni hafifu na ina maslahi ya wazi ya kumega ardhi ya wananchi kwa ajili ya mwekezaji OBC
- Endapo kuna uharibifu wa vyanzo vya maji popote Serikali iwajibike kutimia sheria za usimamizi wa maji kuweka utaratibu mzuri kwa kushirikiana na wananchi wa kulinda vyanzo vya maji.
- Kama kweli hoja ni kulinda vyanzo vya maji katika eneo hili , ni wakati muafaka sasa kwa kampuni ya OBC iliyojenga katika chanzo cha mto Olasae kuondolewa na kulipa fidia ya uharibifu.

### 4.5 Hoja ya Uharibifu wa Mazingira


Kwa muda mrefu serikali na baadhi ya vyombo vya Habari zimekuwa zikiendesha kampeni kuwa eneo hili la kilomita za mradi 1500 linaharibiwa na wenyeji wafugaji wa jamii ya Kimaasai na hivyo waondolewe ili kuhifadhi mazingira ya eneo hili. Madai yao ni kuwa kuna ongezeko kubwa la watu na mifugo katika eneo hili na wengine toka Kenya. Serikali mara kadhaa imesisitiza kuwa ili kunusuru Maisha ya Wanyama na utalii ni vyema eneo hilo la 1500 km za mraba zikatengwa na kuwekwa mbali na wananchi.

### 4.5.1 Uchambuzi wa hoja ya uharibu wa Mazingira

Tunatambu kabisa bila mazingira asili hata mila na shughuli zingine za ufugaji haziwezi kufanyika endapo mazingira asili yata haribika. Kwa miaka yote tumekuwa tukilinda na kuthamini mazingira yetu ya asili na ndio maana hadi leo kuna maliasili nyingi katika maeneo yetu. Hoja hii sisi wananchi tunaipinga kwa sababu zifuatazo;

- Mazingira yetu katika ardhi za Vijiji tumesimamia kabla na baada ya uhuru kwa mfumo wa kimila, na sasa Vijiji kwa utaratibu maalumu vimeendelea kusimamia uhifadhi wa mazingira hasa misitu kwa mujibu wa sheria ndogo za vijiji.
- Viongozi wa Mila pia wamekuwa nguzo muhimu katika uhifadhi wa mazingira kwani wana mamlaka ya kusimamia maeneo hayo muhimu kwa jamii katika shughuli za mila, malisho, wanyamapori, matambiko, dawa za asili, kambi za kula nyama (Orpul), vyanzo vya maji na matumizi mengine kwa manufaa ya umma.

- Hata hivyo ukifuatilia uoto wa asili kwa miaka iliyopita na kulinganisha na sasa kugundua kuwa uhifadhi wa mazingira katika eneo hili imeboreka maradufu tofauti na jinsi inavyo ripotiwa.




***Ramani 4.2:*** *Ramani inayoonyesha uoto wa asili katika Tarafa za Sale na Loliondo kwa nyakati tofauti*

- Asili yetu kama jamii ya kimasai tumekuwa marafiki wazuri wa mazingira na maliasili kwa kuwa tumekuwa na uratibu mzuri wa kulinda rasilimali asili kama ilivyofafanuliwa katika sura ya pili.

### 4.5.2 Maoni Yetu

- Sisi jamii ya kimasai tutaendelea kutumia taratibu zetu za kimila pamoja na zingine za kiserikali kulinda mazingira ya katika eneo hili
- Tutaendelea kutunza mazingira kwa kutumia sheria ndogo za vijiji hasa baada ya ardhi kupimwa na kuwa na mpango wa matumizi ya ardhi.

- Jamii inaona ni vyema kutambuliwa na kupongezwa kwa kuwa wahifadhi asili wa miaka yote.

### 4.6 Hoja ya Uwekezaji/Uwindaji na Utalii

Pamoja na kuwa haisemwi wazi, sisi wananchi wa Loliondo na Sale tunatambua kuwa eneo la 1500 km za mraba zinataka kuchukuliwa kwa lengo la kuhakikisha wawekezaji wanakuwa ama na umiliki wa eneo lote au kuendelea na shughuli za uwindaji kwa uhuru zaidi. Eneo hili limetaka kuchukuliwa mara kadha kwa hoja ya kulinda shughuli za utalii na uhifadhi.

#### 4.6.1 Uchambuzi wa Hoja ya Uwekezaji

Ikumbukwe kuwa eneo la Vijiji vya Tarafa za Sale na Loliondo kwa zaidi ya miongo mitatu sasa limetolewa kwa kampuni ya uwindaji ya OBC. Ifahamike kuwa tangu mwekezaji huyu alipopewa kibali cha uwindaji amekuwa na migogoro na vijiji vyote vya Tarafa hizo zenye ardhi. Pamoja na ukweli huu serikali kwa nyakati zote imeendelea kusisitiza kuwa kampuni hii iendelee na shughuli zake za uwindaji bila kujali mgogoro uliopo. Mawaziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii wamekuwa wakitembelea na kutetea uwepo na maslahi ya Kampuni hii kama ilivyofafanuliwa katika sura ya tatu.

Kampuni hii ya OBC imesababisha wawekezaji wengine wa Vijiji kuondoka na hivyo kukosa mapato yaliyokuwa yakipatikana kwa shughuli ya utalii wa picha. Kimsingi wananchi hawana shida na wawekezaji katika eneo hili hasa wale wanaozingatia taratibu shirikishi ya mipango ya matumizi ya Vijiji na hii inadhibitishwa na uwepo wa makampuni mengine kwenye maeneo ya Vijiji. Jedwali hapo chini linaonyesha wawekezaji wanaoendelea na shughuli za kitalii katika eneo lao.

***Jedwali 4.1:*** *Uwepo wa wawekezaji tofauti katika Tarafa za Loliondo na Sale*

| JINA LA KAMPUNI | | UWEZO | KIJIJI |
|---|---|---|---|
| 1 | & Beyond Klein's Camp | 10 Rooms<br>22 wageni<br>Bei ya kila mgeni USD 1050 | Ololosokwan |
| 2 | TAASA LUXURY LODGE | Rooms 20<br>Wageni 30<br>Bei kwa mgeni USD 630 | Ololosokwan |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | Thomson safaris Ltd | Room 12<br>Wageni 24 | Sukenya |
| 4 | Lake Natron Tented Camp | Rooms 8<br>Wageni 18<br>USD 75 kwa mgeni | Engaresero |
| 5 | Moivaro Tented Lodge and Campsites | Rooms 11<br>Wageni 20<br>Bei 120 USD kwa mgeni wa nje na USD 60 – mtanzania | Engaresero |
| 6 | Maasai giraffe Eco-lodge | Rooms 2<br>Wageni 4 & campsites | Engaresero |
| 7 | Halisi tented Camp | Room 10<br>Wageni 23 | Engaresero |
| 8 | Lengai lodge | Room 10<br>Wagen 22<br>Bei kwa mgeni USD 100 | Engaresero |
| 9 | World View Campsite | Campsites<br>USD 5 kwa mgeni | Engaresero |
| 10 | Lake Natron – Summit Africa | Room 10<br>Wageni 20<br>Bei ya mgeni – USD 250 | Engaresero |
| 11 | Mikuyu Rivers campsite | Wageni 60- kwa kuweka tents. | Engaresero |
| 12 | OBC | Haijulikani | Ukanda wote wa km za mraba 1500 |
| 13 | Maasai Boma | | Ololosokwan |

***Chanzo:*** *Idara ya Maliasili ya Wilaya Ngorongoro*

### 4.6.2 Maoni Yetu

Tarafa hizi mbili za Loliondo na Sale zimekuwa na wawekezaji wa aina mbalimbali katika sekta ya uhifadhi. Sisi Wananchi wa Tarafa hizi kamwe hatujawahi kuzungumzia uwekezaji kama hoja mbaya, la hasha. Haya ndiyo maoni yetu kuhusu uwekezaji,utalii na uwindaji;

- Tunapendekeza uwepo wa uwekezaji unaozingatia sheria, haki za wenyeji pamoja na usalama wa ardhi kwa kuwa umeleta manufaa mengi sana, kwa serikali na wananchi. Kati ya wawekezaji 12 hapo juu, jamii imejikuta ina mgogoro wa muda mrefu na OBC pamoja na kampuni ya utalii ya Thompson Safari chini ya kampuni yake Tanzu ya Tanzania Conservation Limited

- Kampuni ya OBC ina migogoro na Jamii, wawekezaji wengine na kusababisha ukanda huu kutokuwa na utulivu na maendeleo pia. Wawekezaji wengine 10 wanashirikiana na vijiji, halmashauri, Serikali kuu na baina yao ni OBC. Hivyo tunapendekeza Serikai imwondoe mwekezaji huyu kwa maslahi ya wananchi, Taifa kwa ujumla na kwa kuzingatia usalama wa ardhi ya vijiji.

SURA YA
TANO

# MAPENDEKEZO YA JUMLA NA HITIMISHO

## 5.0 MAPENDEKEZO YA WANANCHI

1. Serikali itambue kuwa eneo hili lenye kilomita za mraba 1500 katika Tarafa za Loliondo na Sale ni eneo halali la Vijiji kwa mujibu wa sheria za Nchi kama ilivyo chambuliwa katika Sura ya pili ya taarifa hii.


2. Sisi wananchi wa Vijiji Vya Tarafa za Sale na Loliondo tupo tayari kujadiliana na Serikali ili kutafuta suluhu ya kudumu kuhusu mgogoro huu ambao umedumu kwa takribani miaka 30.

3. Kimsingi, chanzo kikuu cha mgogoro huu kati ya wananchi na Wizara ya Maliasili na Utalii kimesababishwa na kuchochewa na Kampuni ya OBC, hivyo ili kuishi kwa amani katika Vijiji vyetu na kuendelea kuwa na mahusiano mazuri na Serikali yetu, kampuni hii iondolewe katika eneo hili la Tarafa za Loliondo na Sale ili tupate nafasi huru ya kujadili swala la uhifadhi na maendeleo ya wananchi kwa kushirikiana na Serikali yetu.

4. Kufanya mapitio ya mipango ya matumizi ya ardhi ya Vijiji ili kukidhi mahitaji ya sasa ya kijamii, kiuchumi, kimazingira na kiutawala kwa Mujibu wa Sheria za Mipango ya Matumizi ya Ardhi Na. 6 ya 2007 na Sheria ya ardhi ya Vijiji Na.5 ya 1999.

5. Wizara ya Maliasili na Utalii isitishe azma ya kumega sehemu ya ardhi ya vijiji kwa matumizi ya uhifadhi na uwindaji kwani eneo hili ni ardhi halali ya Vijiji husika. Serikali itambua na kuendeleza uhifadhi wa kijamii kwa malengo ya kulinda rasilimali asili pamoja na haki za ardhi wafugaji.

6. Tunapendekeza baada ya kufanyika kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa kila kijiji, Wananchi waunde Kamati Jumuishi ya vijiji vyenye mgogoro ili kuratibu shughuli zinazofanyika katika eneo



hilo ikiwa ni pamoja na shughuli za malisho ya mifugo, uhifadhi wa wanyamapori, utalii, utunzaji wa mazingira, ibada za kimila na utunzaji wa vyanzo vya maji.

7. Serikali ikatae pendekezo la kumegwa kwa eneo la ardhi ya Vijiji vya Loliondo na Sale lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1500 na eneo la Ziwa Natron inayojumuisha Kata za Pinyinyi na Engaresero kwa lengo la kuingizwa kwenye eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCA) kama ilivyopendekezwa na Kamati ya wahifadhi ya matumizi mseto ya ardhi yaani Multiple Land Use Model (MLUM) ya 2019.

8. Serikali itambue kwamba eneo hili ni muhimu kiuchumi kwa wafugaji wa Vijiji vya Tarafa za Loliondo na Sale ambalo linategemewa na watu zaidi ya 66,000, kwani kupoteza ardhi hiyo ni kuwarudisha wananchi katika umaskini na ufukara wa kutisha.

9. Serikali itambue kuwa eneo hili sio wazi bali ni nyanda za malisho ya mifugo. Wamasai wa eneo hili wanategemea kwa zaidi ya asilimia 90 shughuli za ufugaji asili kama chanzo kikuu cha mapato na chakula.


10. Tunashauri Serikali izingatie shauri linalohusu mgogoro huu ambalo lipo katika Mahakama ya haki ya Afrika Mashariki.

11. Tunaisihi Wizara ya Habari na Mamlaka ya Mawasiliano nchini kupiga marufuku vyombo vya habari visivyo fuata maadili ya uandishi ambyo vinatoa taarifa za uongo, upotoshaji na uchonganishi kati ya serikali na wananchi wa Tarafa za Loliondo na sale.

12. Tunashauri Serikali itambue haki za mashirika na watetezi wa kijamii na haki za binadamu ambao wamekuwa wakisumbuliwa mara kwa mara wanapojaribu kusaidia serikali na jamii kutatua changamoto hizi.

13. Tunahimiza Serikali ipige marufuku kamata kamata ya viongozi wa kijamii inayoendelea kwa sasa katika Tarafa za Sale na Loliondo. Kitendo hichi kinaendelea kuzua taharuki miongoni mwa jamii na pia kufifisha jitihada za pamoja za kutatua changamoto hizi.

14. Tunapendekeza kuundwa kwa Tume Huru ya kuchunguza ukiukwaji wa haki za binadamu na haki za wafugaji zilizofanyika kwa kipindi cha miaka 30 iliyopita katika eneo lenye mgogoro.



15. Tunapendekeza kuwa kuanzia sasa swala la mgogoro wa Loliondo na Sale uwe unakwenda kwa njia ya mazungumzo kupitia kamati hii ya jamii pamoja na serikali il kupunguza mivutano isiyokuwa ya lazima. Kamati hii itasaidia kuondoa mwanya wa watu wasiohusika na mgogoro huu na wanaotoka nje ya Wilaya ya Ngorongoro kutumika katika majadiliono ya kutatua mgogoro huu.

16. Kwa kuzingatia kuwa nchi ipo katika uchumi wa kati, serikali iboreshe na kufungua fursa mbali mbali za kibiashara kwa kuboresha miundo mbinu hasa masoko, Kiwanda cha kuchakata mazao ya mifugo, elimu za ufugaji wenye tija, mtandao wa barabara za lami nk. Hatua hii itatoa fursa kwa wananchi kupata fursa za kimaendeleo kwa haraka na kuchangia pato la taifa pamoja na kupunguza migogoro ya rasilimali.

17. Serikali ifanye jitihada za haraka kuwekeza katika Elimu ili kuendeleza watoto wa jamii hii. Hii ni Pamoja na serikali kujenga shule za Msingi katika kila kitongoji kilichopo Zaidi ya kilomita 7 kutoka kitovu cha Kijiji.

## 5.1 HITIMISHO

Taarifa hii ya wananchi wa Tarafa ya Sale na Lolindo imeelezaa kwa kina kuhusu mgogoro wa muda mrefu wa ardhi katika maeneo ya kata Nane za Loliondo na Sale zinazopakana na Hifadhi ya Serengeti. Taarifa hii imechambua kwa kina kiini cha mgogoro unaohusisha eneo la vijiji lenye ukubwa wa km za mraba 1500 pamoja na uhifadhi na wawekezaji wa uwindaji kwa upande mwingine. Uchambuzi huu umebaini kuwa ardhi yenye mgogoro ni ardhi ya vijiji kwa mujibu wa sheria za Tanzania na wananchi wanatumia maeneo hayo kwa shughuli za kifugaji pamoja na shughuli zingine za kimila.

Ripoti hii ya wananchi imebeba uchambuzi wa kina wa chanzo cha mgogoro huu wa muda mrefu pamoja na mapendekezo ya utatuzi. Na kwa kuwa Jamii iliwahi kuwasilisha taarifa za aina hii kwa Waheshimiwa Mawaziri wakuu (Mhe Pinda-2013 na Mhe Majaliwa-2017) tunashauri Serikali yetu iweze kuzingatie mapendekezo yetu ili tuweze kufikia mwisho wa mgogoro huu wa Loliondo. Tumebaini kwamba uwepo wa kampuni ya uwekezaji ya OBC ndio imekua chanzo cha migogoro hii isiyoisha. Tunapendekeza ikiwezekana shughuli za uwindaji zipunguzwe au kuachwa kabisa katika eneo hili la vijiji vyetu ili kupunguza mgogoro kati ya wananchi na wawindaji hasa wa kampuni ya OBC.

# 6. MAREJEO

**A: Sera, Sheria, Hotuba na Tamko**


The Land Act No. 4 of 1999.

The Land Act No. 5 of 1999.

The Land Use Planning Act, No. 6 of 2007

The Wildlife Conservation Act, No. 5 of 2009

Sheria ya Serikali za Mitaa, Tawala za Wilaya namba 7 ya Mwaka 1982.

The Ngorongoro District Land Use Framework Plan (1993 – 2008).

Land Tenure Ordinance No. 3 of 1923

The Game Preservation Ordinance, 1908.

The Game Preservation Ordinance 1921).

The New Game Ordinance ya 1948),

Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ya 1959.

The Rural Land Act, 1973.

The Wildlife Conservation Act No. 12 of 1974.

The Villages and Ujamaa Villages Act 1975

The Land Tenure (Village Settlements) Act 1965.

The National Parks Ordinace, 1948.

Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995.

Tangazo la Serikali. Na;245/269/1959/1974.

Tangazo la Serikali Na;235/1968.

NLUPC (2010) Rasimu ya Mpango wa Pili wa Matumizi ya Ardhi (Ngorongoro District Land Use Framework Plan (2010-2030).

Barua ya Waziri Mkuu wa Awamu ya Nne, Mhe Mizengo Pinda kwa Mhe Rais na Wananchi wa Ngorongoro ya Tarehe 30/5/2013

Ripoti ya TNRF, Integrating Pastoralist Livelihoods and Wildlife Conservation? Options for Land Use and Conflict Resolution in Loliondo Division, Ngorongoro District February 2011 https://www.tnrf.org/files/Integrating%20Pastoralist%20Livelihoods%20and%20Wildlife%20Conservation_FINAL_FINAL.pdf, imerejewa tarehe 4/5/2022.

Chiligati, J.Z (2010) Hotuba ya Mhe. John Zefania Chiligati, (Mb.),Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, akiwasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya wizara ya ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi, kwa mwaka 2010/11.https://www.tanzania.go.tz/egov_uploads/documents/2010-2011_SWAHILI_sw.pdf, imerejewa tarehe 3/5/2022

United Republic of Tanzania (URT) (1967) Land Acquisition Act Number 47 of 1967. Dar es Salaam, URT

URT (1994) Ministry of Lands, Housing and Urban Development & Scandinavia Institute of African Studies (1994), Report of the Presidential Commission of Inquiry into Land matters, Vol.I

Kigwangala H (2017) Tamko la Waziri wa Maliasi na Utalii Mh Kigwangala H (2017) https://www.youtube.com/watch?v=W4pPfyK1GDY

Kagasheki, H (2013) Tamko la Waziri wa Maliasili Mh Kagasheki Juu ya Loliondo (2013) https://www.maliasili.go.tz/highlights/view/government-clarifies-on-decision-to-provide-huge-tracks-of-land-to-loliondo imerejewa tarehe 21 Mei, 2022.

**B: Kesi za Mahakama**

Mulbadaw Village Council and 67 Others vs. NAFCO (1984) T.L.R. p. 15-27 HC-Arusha

Yoke Gwaku and 5 Others vs. Gawal Farms Limited and NAFCO (1988) Civil Case No. 52 of 1988 HC-Arusha (unreported)

Isata Ndekerei & 14 others vs. Tanzania Breweries Limited Farms 7) Magistrate Court of Arusha Case No. 74 of 1987

Ololosokwan Village Council vs. Tanzania Cattle Products and Conscorp Tanzania Limited Civil Case No. 31 of 1994.

Ololosokwan Village Council vs. Tanzania Cattle Products and Andbeyond Tanzania Ltd, Land Case No. 15 of 2011 (HC-Arusha)

Noonkirimban Seret Sironga v. Republic (HC-Mwanza) Criminal Appeal No.387 of 2017

Mondorosi Village Council, Sukenya Village Council and Soitsambu village Council Vs. Tanzania breweries LTD, Tanzania Conservation LTD, Ngorongroro District Council, The Commissioner for Lands and Attorney general (HC-Arusha) Land Case No. 26 of 2013

Ololosokwan Village Council & 3 Others vs. The Attorney General of the Government of the United Republic of Tanzania. Kesi namba 10 of 2017 (EACJ), Inapatikana https://www.eacj.org/?page_id=5986&fwp_year=2017, visited on 9th May, 2022

**C. Taarifa za Kitafiti na Machapisho**


Neumann, RP (2000), 'Land, justice, and the politics of conservation in Tanzania', in Zerner C (ed), People, plants, and justice: the politics of nature conservation, Columbia University Press, New York, pp. 117–143.

_____________(1998), Imposing wilderness: struggles over livelihood and nature preservation in Africa, University of California Press, Berkeley and Los Angeles

_____________ (1995a), 'Ways of seeing Africa: colonial recasting of African society and landscape in Serengeti National Park', Ecumene, vol. 2, pp. 149 169.

_____________(1995b), 'Local challenges to global agendas: conservation, economic liberalization and the pastoralists rights movement in Tanzania', Antipode, vol. 27, no. 4, pp. 363 382.

Ojalammi, S. (2006). Contested lands: Land disputes in semi-arid parts of northern Tanzania. PhD Thesis, University of Helsinki, Finland. Available at: http://ethesis.helsinki.fi/julkaisut/mat/maant/vk/ojalammi/conteste.pdf

Ole Nangoro, BN (1998) 'Branding the land: Maasai responses to resource tenure insecurity and social change', in Horn, F (ed), Economic, social and cultural rights of the Maasai, University of Lapland, Rovaniemi.

Shivji, I. G & Kapinga, WB 1998, Maasai rights in Ngorongoro Tanzania, Drylands Programme, IIED/Hakiardhi, London,

Shivji; IG 1998a, Not yet democracy: reforming land tenure in Tanzania, IIED/Hakiardhi, London.; Shivji, IG 1998b, 'Contradictory perspectives on rights and justice in the context of land tenure reform in Tanzania', Tanzania Zamani, vol. 4, no.1, pp. 57 96. 220

Shivji, IG 1994, Report of the presidential commission of inquiry into land matters, land policy and tenure structure, vol. 1, Scandinavian Institute of African Studies, Uppsala.

Shoo, RA & Songorwa, AN 2013, 'Contribution of eco-tourism to nature conservation and improvement of livelihoods around Amani nature reserve, Tanzania', Journal of Ecotourism, vol. 12, no. 2, pp. 75–89

African Union. 2010. Policy Framework for Pastoralism in Africa: Securing, Protecting and Improving the Lives, Livelihoods and Rights of Pastoralist Communities. Department of Rural Economy and Agriculture, African Union, Addis Ababa.

Shivji & Kapinga. 1998 Haki za Wamasai waishio katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, HAKIARDHI/IIED

Ole Nasha T. W. (2004): Reforming Land Tenure In Tanzania: For Whose Benefit? HAKIARDHI, Dar es Salaam.

Survival International (2009) http://www.survivalinternational.org/news/4974

Oakland Institute (2019) https://www.oaklandinstitute.org/sites/oaklandinstitute.org/files/pdfpreview/mlum-final-oct-2019.pdf,

PINGOs Forum (2012) Assessment of the Situation of Human Rights violations in Pastoralists, Hunter-Gatherers (Indigenious) Communities of Tanzania. Microsoft Word - Situational Assesment of Human Rights Violations in IPs in Tanzania.docx (pingosforum.or.tz)

PINGOs Forum (2017) Identification and Documentation of the Human Rights Violations against Pastoral Community in Loliondo, Ngoronrogo District, Arusha Region, Tanzania. Microsoft Word - Loliondo HR Documentation .doc (pingosforum.or.tz)

THRDC (2016) Taarifa kwa Umma Kuhusu Kukamatwa Bwana Samweli Nangira, Mkurugenzi wa Shirikla La Ngonet-Loliondo

THRDC (_) Tamko kwa Umma Juu ya Hali ya Watetezi wa Haki za Wafugaji Loliondo

**D. Vyombo vya Habari/Tovuti**

https://ngorongorodc.go.tz/historia

Mwananchi (15 Aprili 2015) Koo za Kimasai Ngorongoro zina udugu na wanyama? https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/habari-ya-ndani/koo-za-kimasai-ngorongoro-zina-udugu-na-wanyama--2782572

Wavuti (21 November, 2014) Taarifa ya Haraka kwa Vyombo vya Habari Kuhusu Mgogoro wa Ardhi Loliondo ya tarehe 21 Novemba, 2014, (https://www.wavuti.com/2014/11/taarifa-ya-dharura-kuhusu-mgogoro-wa.html imerejewa tarehe, 4/4/2022

Mwananchi (25 Februari 2019) Takukuru yamshikilia mkurugenzi kampuni ya OBC https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/takukuru-yamshikilia-mkurugenzi-kampuni-ya-obc-2955912, imerejewa tarehe 3/5/2022

Norduland, S View from the Termite Mound: Article about Loliondo land threats on Just Conservation's website (termitemoundview.blogspot.com )

Mwananchi (05 September 2017) Tume ya Haki za Binadami yazuia operesheni Loliondo https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/tume-ya-haki-za-binadamu-yazuia-operesheni-loliondo-2864456, imerejewa tarehe 3/5/2022

Jamhuri (22Aprili2015) Wakenya wavamia Tanzania http://www.jamhurimedia.co.tz/wakenya-wavamia-tanzania/

Jamhuri ( ) Loliondo yageuzwa Kenya. https://www.jamhurimedia.com.tz/loliondo-yageuzwa-kenya.

https://1.bp.blogspot.com/-QNqDNQvoyHA/WqjtGUcYFLI/AAAAAAAAMzE/DGcyt_3rI-IiqwEkaZ6TZ4yZfgiawPHKgCLcBGAs/s1600/loliondo_evictions.jpg. .

Conservation Watch/ Chris Lang ( 30 August 2017) "Forced evictions of Maasai people in Loliondo, Tanzania": Urgent Alert from the International Work Group for Indigenous Affairs https://medium.com/conservationwatch/forced-evictions-of-maasai-people-in-loliondo-tanzania-urgent-alert-from-the-international-work-8417b9c71fee.

VSF, (25 Machi 2015) The European Parliament condemns land grabbing in Tanzania https://vsf-international.org/european-parliament-condemns-land-grabbing-in-tanzania/

Mwananchi (14 Januari 2019) Wanne waliokamatwa kwa tuhuma za uchochezi waachiwa https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/wanne-waliokamatwa-kwa-tuhuma-za-uchochezi-waachiwa-2948718

Forestpeople (2016) Tamko kwa Vyombo vya Habari kuhusu kukamatwa kwa Watetezi wa Haki za Binadamu Loliondo 26 Julai 2016, Arusha https://www.forestpeoples.org/sites/default/files/private/news/2016/07/Loliondo%20Press%2026%20July%20Swahili.pdf

Ayo Millard (26 July 2016) Mawakili Arusha wameandamana kuelekea makao makuu ya jeshi la polisi (https://millardayo.com/arus67/)


Just Conservation (02 December 2012) Grabbing Land for Conservation in Loliondo, Tanzania. Just Conservation - Grabbing Land for Conservation in Loliondo, Tanzania.

TNRF (2011) Voices from Loliondo (https://www.youtube.com/watch?v=7knZOEVxO0k)

# 7. VIAMBATANISHI

## 1. Hati za Usajili wa Vijiji

### a) Kijiji cha Ololosokwan



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HATI YA KUANDIKISHWA KWA KIJIJI

Na. AR.KIJ. 403

Nathibitisha rasmi kwa HATI hii kwamba kijiji kijulikanacho kama ..........OLOLOSOKWANA.......... leo kimeandikishwa kama kijiji kwa mujibu wa Sheria ya Kuandikisha Vijiji, Kutambuliwa kwa Vijiji vya Ujamaa na Uongozi wa Vijiji, 1975.

HATI hii imetolewa na kutiliwa sahihi na mimi leo tarehe ..........15.......... ya mwezi ..........APRIL.......... 19.78..

H. Z. TALAWA
Msajili wa Vijiji

G P Dodoma 205/12-76/10m/1up

b) Kijiji cha Maaloni-Loosoito



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA


HATI YA KUTHIBITISHA HADHI YA HALMASHAURI YA KIJIJI KUWA SHIRIKA

Na. AR.VC.406

Nathibitisha rasmi kwa HATI hii kwamba Halmashauri ya Kijiji kijulikanacho kama..........LOSOITO..........ambacho kimeandikishwa kwa mujibu wa Sheria ya kuandikisha Vijiji, Kutambuliwa kwa Vijiji vya Ujamaa na Uongozi wa Vijiji, 1975, ina hadhi ya Shirika kwa mujibu wa Sheria hiyo iliyotajwa, kwa hiyo naitoa HATI hii ya uthibitisho kwa Halmashauri ya Kijiji hicho, na HATI hii itaanza kutumika tangu leo.

HATI hii imetolewa na kutiliwa sahihi na mimi leo tarehe ..........26.......... ya mwezi ..........Desemba,.......... 19.78

H.Z. TALAWA
Msajili wa Vijiji



**(c) Kijiji cha Soitsambu**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## HATI YA KUANDIKISHWA KWA KIJIJI

**Na.** AR.KIJ. 402

Nathibitisha rasmi kwa HATI hii kwamba kijiji kijulikanacho kama ......SOITSAMBU...... leo kimeandikishwa kama kijiji kwa mujibu wa Sheria ya Kuandikisha *Vijiji*, Kutambuliwa kwa Vijiji vya Ujamaa na Uongozi wa Vijiji, 1975

HATI hii imetolewa na kutiliwa sahihi na mimi leo tarehe

......15...... ya mwezi ......[illegible]...... 19[illegible]

[illegible]

*Msajili wa Vijiji*

G P Dodoma 205/12-76/10m/1up

## 2. Vyeti vya Ardhi

### a) Kijiji cha Ololosokwan

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Anuani ya Simu: "ARDHI"

Simu:Na. 2121241-9

Tafadhali unapojibu taja:

Kumb. Na. LD/ 244178

IDARA YA ARDHI,

P.O. Box 9230,

DAR ES SALAAM.

26 / Jan /2006.

Afisa Ardhi wa Wilaya

Wilaya ya Ngorongoro

S.L.P. 1

Loliondo

**Yah: CHETI CHA ARDHI YA KIJIJI.**

Nakutumia Cheti cha Ardhi ya Kijiji cha Ololosokwani kilichopo Wilaya ya Ngorongoro kwa usajili.

1. Nyaraka zifuatazo zinawasilishwa kwa ajili ya kusajiliwa.
   - Cheti cha Ardhi ya Kijiji (nakala2) ✓
   - Hati ya mabadiriko (nakala 2)
   - Hati ya kuachia Ardhi( nakala 2)
   - Hati ya kufuta Ardhi (nakala 2)

2. Mkataba wa — Pamoja na Cheti cha Ardhi ya Kijiji.

3. Tafadhali baada ya kusajili wasilisha nakala ya Cheti cha Ardhi ya Kijiji kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Ololosokwani Wilaya ya Ngorongoro kwa kumbukumbu zao.

Kny Kamishna wa Ardhi

Nakala : Afisa Mtendaji wa Kijiji.

Jina la Mpokeaji wa Nyaraka

Jina Michael Masawe

Saini [signature]

Tarehe 26/1/2006

Fomu ya Ardhi ya Vijiji Na. 16

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**SHERIA YA ARDHI YA VIJIJI, 1999**

**(Na. 5 ya 1999)**

**CHETI CHA ARDHI YA KIJIJI**

(Chini ya Fungu la 7)

Namba ya Cheti 1NGR

Kumb.Na. NGR/01

Leo tarehe ....25........ ya mwezi ...Januari..... mwaka 2006.

Hii ni kuthibitisha kuwa Halmashauri ya Kijiji (humu ikirejewa kama "Halmashauri") cha **OLOLOSOKWAN** katika Wilaya ya **NGORONGORO** inakabidhiwa kama mdhamini usimamizi wa ardhi yote iliyoelezwa katika jedwali lililoambatishwa (humu ikirejewa kama "ardhi ya kijiji") kadri ya nia na maana halisi ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji na kwa masharti yafuatayo:-

i) Halmashauri itasimamia ardhi ya kijiji kadri ya sheria za mila zinazohusu ardhi kwenye eneo husika.

ii) Halmashauri italinda mazingira kwa kuhifadhi rutuba ya ardhi na kuzuia mmomonyoko wa udongo;

iii) Halmashauri italinda haki za njia;

iv) Halmashauri italinda na kutunza mipaka ya kijiji;

v) Halmashauri itatunza na kukihifadhi kwa usalama cheti hiki;

vi) Endapo mipaka ya kijiji imebadilishwa au kurekebishwa, Halmashauri itatuma cheti kwa Kamishna ili kuidhinisha mabadiliko au marekebisho ya mipaka kwenye cheti;

vii) Halmashauri itatoa hati ya hakimiliki ya kimila na kutunza daftari la ardhi la kijiji.

## JEDWALI

Eneo lote lijulikanalo kama Kijiji cha **OLOLOSOKWAN** katika wilaya ya **NGORONGORO** lenye ukubwa wa HEKTA 51230 ( Elfu hamsini na moja mia mbili na thelathini ) Kama mipaka inavyoonyeshwa kwa wino katika ramani/mchoro uliambatanishwa hapa.

IMETOLEWA na Rais na imekabidhiwa kwa MKONO wangu na LAKIRI rasmi kuwekwa siku na mwaka vilivyoandikwa hapo juu.

Kamishna wa Ardhi

IMEWEKEWA LAKIRI halisi ya Halmashauri ya Kijiji

cha **OLOLOSOKWAN** mbele yetu:

1. Jina: JULIUS - SEIELO - KAURA

   Saini: ..............................

   Cheo: Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kijiji

   Anuani: P.O. BOX 13 LOLIONDO .............................. LAKIRI/MUHURI

2. Jina: [illegible] - JOHN - LETEMA

   Saini: ..............................


   Cheo: Katibu wa Halmashauri ya Kijiji

   Anuani: P.O. BOX 13 LOLIONDO

Nakala: Msajili

# 3. Hati ya Kumiliki Ardhi ya Kijiji


## a) Kijiji cha Ololosokwan





JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA


HATI YA KUMILIKI ARDHI

(Kifungu Na. 9 cha Sheria ya Ardhi)









## (b) Kijiji cha Oloipiri

HATI YA KUMILIKI ARDHI

(Kifungu Na. 9 cha Sheria ya Ardhi)

Imetolewa tarehe .............................. mwezi ........ Mwaka Elfu moja mia tisa na TISINI. ..............................

HATI NA 7/82

HII NI KUTHIBITISHA kwamba: HALMASHAURI YA KIJIJI CHA OLOIPIRI iliyosajiliwa chini ya Sheria ya "The Local Government (District Authorities) Act No. 7 1982 S.L.O. ..............................

(baadaye katika Hati hii itaitwa "Mmilikaji") inayo aki ya kumiliki Ardhi (baadaye itaitwa "Haki") juu ya eneo lililoelezwa mwishoni mwa Hati hii (baadaye litaitwa "Eneo") kwa muda wa miaka tisini na tisa kuanzia tarehe Moja ..................... mwezi: Julai ........ mwaka Elfu moja mia tisa na tisini ......... kwa mujibu wa Sheria za Ardhi na Kanuni nyingine zitakazotungwa chini ya Sheria hiyo na sheria nyingine zitakazotungwa badala yake pamoja na marekebisho yake, na chini ya Kanuni za Ardhi za Vijiji za mwaka 1986 na masharti maalum yafuatayo:-

1. Mmilikaji baada ya kulipa kodi ya ardhi hadi tarehe thelathini ya mwezi Juni, 1990 ........ atawajibika kulipa mbele kodi ya ardhi ya shilingi mia moja (Shs.100/=) ...... ifikapo tarehe ya kwanza ya mwezi Julai kila mwaka. Kodi hiyo inaweza ikabadilishwa na Waziri anayeshughulikia mambo ya Ardhi (baadaye aitwaye "Waziri") kila baada ya miaka kumi.

..... 47,100 HA .....

## (c) Maaloni-Loosoito

'A'

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HATI YA KUMILIKI ARDHI

[illegible]

HATI Na. 7259

[illegible]

MINISTRY OF LANDS, WATER, HOUSING AND URBAN DEVELOPMENT

LAND REGISTRY,
P.O. BOX 190
MOSHI
TANZANIA

Ref.No. LR/MS/T/7259/21 22th OCTOBER 1990

REGISTERED

To: MWENYEKITI
KIJIJI CHA LOSOITO

Title No. 7259 Land Office No. 1197

Plot No. ................ Block ................

I have the honour to enclosure herewith duplicate of the Certificate of Title numbered as above for delivery to the occupier of the above property.

2. Please endorse your signature on the enclosed form of receipt and return the letter to me in due course.

C.C. RLDO ARUSHA

D. S. Mwakilema
Gen. Assist. Registrar of Titles

DOCUMENT SIGNED ON 18-10-90

## (d) Oloirien-Magaiduru

Land Form 33C.

NGORDW/S/D. NO. 1196.

L.D. NO. ..........

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HATI YA KUMILIKI ARDHI

(Kifungu Na. 9 cha Sheria ya Ardhi)

Imetolewa tarehe .............................. mwezi ..........
Mwaka Elfu moja mia tisa na TISINI..............................

HATI Na.

HII NI KUTHIBITISHA kwamba: HALMASHAURI YA KIJIJI CHA OLOIRIEN/MAGAIDURU ....................................

(baadaye katika Hati hii itaitwa "Mmilikaji") anayo haki ya kumiliki Ardhi (baadaye itaitwa "Haki") juu ya eneo lililoelezwa mwishoni mwa Hati hii (baadaye litaitwa "Eneo") kwa muda wa miaka tisini na tisa kuanzia tarehe: MOSI ............................ mwezi: Julai ............... mwaka Elfu moja mia tisa na TISINI.......... kwa mujibu wa Sheria za Ardhi na Kanuni nyingine zitakazotungwa chini ya Sheria hiyo na sheria nyingine zitakazotungwa badala yake pamoja na marekebisho yake, na chini ya Kanuni za Ardhi za Vijiji za mwaka 1986 na masharti maalum yafuatayo:-


1. Mmilikaji handa ya kulipa kodi ya ardhi hadi tarehe thelathini ya mwezi Juni, 19.90....... atawajibika kulipa mbele kodi ya ardhi ya shilingi .914 mwaka (Shs.101/=)........ ifikapo tarehe ya kwanza ya mwezi Julai kila mwaka. Kodi hiyo inaweza ikabadilishwa na Waziri anayeshughulikia mambo ya ardhi (baadaye ataitwa "Waziri") kila baada ya miaka kumi.

2. Eneo hilo litatumiwa kwa shughuli yadhaa ikiwa ni pamoja na kilimo, mifugo, misitu, makazi, biashara na viwanda kufuatana na mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji.


3. Mmilikaji atawajibika:-

(a) Kuweka alama za mipaka ya eneo katika hali ya kuzuri, chini ya Halmashauri ya Wilaya ya: NGORONGORO ................ (baadaye itaitwa Halmashauri) na baadaye kuitunza mipaka hiyo katika hali nzuri ili wakati wote iweze kuonekana kwa urahisi.

## (e) Kijiji cha Arash



# (f) Kijiji cha Soitsambu



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HATI YA KUMILIKI ARDHI

(Kifungu Na. 9 cha Sheria ya Ardhi)

Imetolewa tarehe ... 15 ... mwezi ... 05 ... Mwaka Elfu moja mia tisa na ...

HATI Na. 7265 ...

HII NI KUTHIBITISHA kwamba HALMASHAURI YA KIJIJI CHA SOITSAMBU ... Local Government (District ...) ... No. 7 ya 1982 S.L.P. ...

(ambaye katika Hati hii itaitwa "Mmiliki") inayo haki ya kumiliki Ardhi (baadaye itaitwa "Haki") juu ya eneo lililoelezwa ... Hati hii (baadaye litaitwa "Eneo") kwa muda wa ... tarehe ... Julai ... mwaka Elfu moja mia tisa na ... kwa mujibu wa Sheria za Ardhi na Kanuni nyingine ... za Sheria hiyo na sheria nyingine zitakazotungwa ... marekebisho yake, na chini ya Kanuni za Ardhi ... ya mwaka 1986 na masharti yafuatayo:-

1. Mmiliki baada ya kulipa kodi ya ardhi hadi tarehe ... mwezi Juni, 19... atawajibika kulipa ... ya ardhi ya shilingi ... moja (Shs ...) ... mwezi Julai kila mwaka. Kodi hiyo inaweza ... na Waziri anayeshughulikia mambo ya ardhi (baadaye "Waziri") kila baada ya miaka mitano.

2. Eneo hilo litatumiwa kwa shughuli kadhaa ikiwa ni ... kilimo, mifugo, misitu, makazi, ... na vitendo ... na mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji.

3. Mmiliki atawajibika:-

(a) Kuweka mipaka ya eneo katika hali ya kuiri... Halmashauri ya Wilaya ya NGORONGORO ... (baadaye itaitwa Halmashauri) ... [illegible]



## 4. Sheria Ndogo za Vijiji

### a) Oloipiri

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA,**
**(SERIKALI ZA VIJIJI)**
**NA. 7 1982.**

**Zilizoundwa chini ya kisehemu cha 120 (1) na 163.**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO**

**KIJIJI CHA OLOIPIRI**

**Sheria ndogo za kutunza, kulinda na kutekeleza mpango wa matumizi bora ya Ardhi, Mazingira, maliasili na huduma mbalimbali za jamii katika Kijiji cha Oloipiri.**

Mpango huu umetayarishwa kwa ushirikiana kati ya Serikali ya Kijiji, Kamati ya Mazingira na Maliasili, Wataalamu kutoka wilayani, kata na Community Resource Team – 2000

**Uthibitisho** Muhuri wa Halmashauri ya kijiji cha Oloipiri umebandikwa kwenye sheria ndogo hizi kwa mujibu wa Mkutuno Mkuu wa Kijiji Uliofanyika tarehe 27 Novemba 2000, na umebandikwa mbele ya;

**Kerika Kursas**
**Mwenyekiti wa Halmashauri ya kijiji cha Oloipiri**

**Tuambei Leshoko**
**Ofisa mtendaji wa Halmashauri ya kijiji cha Oloipiri**

**NAKUBALI:**

**Mhe : Simon Soinda**
**Mwenyekiti wa Halmashauri wa wilaya ya Ngorongoro**

**K.M.C. Tingirawanyuma**
**Mkuregenzi Mtendaji wa Halmashauri wa wilaya ya Ngorongoro**

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA
YA NGORONGORO

## b) Soitsambu

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA.**
**(SERIKALI ZA VIJIJI)**
**NA. 7 1982.**

**Zilizoundwa chini ya kisehemu cha 120 (1) na 163.**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO**

**KIJIJI CHA SOIT-SAMBU**

**Sheria ndogo za kutunza, kulinda na kutekeleza mpango wa matumizi bora ya Ardhi, Mazingira, maliasili na huduma mbalimbali za jamii katika Kijiji cha Soit-Sambu.**

Mpango huu umetayarishwa kwa ushirikiana kati ya Serikali ya Kijiji, Kamati ya Mazingira na Maliasili, Wataalamu kutoka wilayani, kata na Community Resource Team – 2000

| | | |
|---|---|---|
| | wazee | onyo kali kwa wanawake na watoto |
| 9. Uchomaji mkaa | Kuchoma mkaa bila idhini ya Halmashauri | Faini ya shilingi 10,000/= kwa kila gunia na kunyanganywa mkaa |
| 10. Maeneo ya Malisho na Wanyamapori | Kujenga makazi ya kudumu, kulima, kuchoma moto na kukata miti | Faini ya shiligi 10,000/= Kama amejenga na kufukuzwa katika eneo hilo |
| 11. Makazi ya Kudumu na Huduma | Kulima, kujenga, kufanya biashara nje ya mpaka | Faini ya shilingi 10,000/= kwa kila kosa na kufukuzwa |
| 12. Mapito na Vivuko | Kujenga, Kulima | Faini ya shilingi 10,000/= kwa kila robo heka na kufukuzwa |

**Uthibitisho** Muhuri wa Halmashauri ya kijiji cha Soit-Sambu umebandikwa kwenye sheria ndogo hizi kwa mujibu wa Mkutuno Mkuu wa Kijiji Uliofanyika tarehe 12 Januari 2000, na umebandikwa mbele ya

M/KITI KIJIJI CHA SOIT SAMBU
NGORONGORO

**James Lembikas,**
**Mwenyekiti wa Halmashauri**
**ya kijiji cha Soit-Sambu**

AFISA MTENDAJI WA KIJIJI
SOITSAMBU

**Simon Mbusya,**
**Ofisa mtendaji wa Halmashauri**
**ya kijiji cha Soit-Sambu**

**NAKUBALI:**

**Mhe : Simon Soinda**
**Mwenyekiti wa Halmashauri**
**wa wilaya ya Ngorongoro**

CHAIRMAN
NGORONGORO DISTRICT COUNCIL

**K.M.C. Tingirawanyuma**
**Mkuregenzi Mtendaji wa**
**Halmashauri wa wilaya ya**
**Ngorongoro**

## c) Ololosokwan

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA.**
**(SERIKALI ZA VIJIJI)**
**NA. 7 1982.**

**Zilizoundwa chini ya kischemu cha 120 (1) na 163.**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO**

**KIJIJI CHA OLOLOSOKWAN**

**Sheria ndogo za kutunza, kulinda na kutekeleza mpango wa matumizi bora ya Ardhi, Mazingira, maliasili na huduma mbalimbali za jamii katika Kijiji cha Ololosokwan.**

Mpango huu umetayarishwa kwa ushirikiana kati ya Serikali ya Kijiji, Kamati ya Mazingira na Maliasili, Wataalamu kutoka wilayani, kata na Community Resource Team – 2000

| | | |
|---|---|---|
| | ya Halmashauri ya kijiji | kwa kila gunia na kunyanganywa mkaa na kufukuzwa eneo |
| 9. Maeneo ya Malisho na Wanyamapori | Kulima, kuchoma moto na kukata miti | Adhabu kwa taratibu za kimila au faini ya shilingi 20,000/= |
| | Kujenga makazi ya kudumu | Kuvunja makazi kwa gharama ya muhusika |
| 10. Makazi ya Kudumu na Huduma | Kukiuka masharti ya sheria ndogo | Faini ya shilingi 10,000/= kwa kila kosa na kufukuzwa |
| 11. Mapito, Vivuko na sehemu za chumvi | Kujenga, Kulima au Kufunga | Faini ya shilingi 10,000/= na kufukuzwa katika eneo au vyote viwili kwa pamoja |
| 12. Kilimo | Kuchunga mifugo kwenye mashamba | Faini ya shilingi 10,000/= |
| | Kufunga mashamba kwenye eneo la malisho | Kusimamishwa shughuli za kilimo na kutozwa faini ya shilingi 8,000/= |

**Uthibitisho**

Muhuri wa Halmashauri ya kijiji cha Ololosokwan umebandikwa kwenye sheria ndogo hizi kwa mujibu wa Mkutano Mkuu wa Kijiji Uliofanyika tarehe 12 Februari 2000, na umebandikwa mbele ya:

MWENYEKITI WA SERIKALI YA KIJIJI OLOLOSOKWAN

**Yohana Saing'eu**
**Mwenyekiti wa Halmashauri ya kijiji cha Ololosokwan**

AFISA MTENDAJI KIJIJI OLOLOSOKWAN

**Songoi Letura**
**Ofisa mtendaji wa Halmashauri ya kijiji cha Ololosokwan**


**NAKUBALI:**

**Mhe : Simon Soinda**
**Mwenyekiti wa Halmashauri wa wilaya ya Ngorongoro**

**K.M.C. Tingirawanyuma**
**Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri wa wilaya ya Ngorongoro**

HALMASHAURI YA NGORONGORO

16



## d) Maaloni-Oloosoito

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA.**
**(SERIKALI ZA VIJIJI)**
**NA. 7 1982.**

**Zilizoundwa chini ya kisehemu cha 120 (1) na 163.**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO**

**<u>KIJIJI CHA MAALONI-OLOOSOITO</u>**

**Sheria ndogo za kutunza, kulinda na kutekeleza mpango wa matumizi bora ya Ardhi, Mazingira, maliasili na huduma mbalimbali za jamii katika Kijiji cha Maaloni-Oloosoito.**

Mpango huu umetayarishwa kwa ushirikiana kati ya Serikali ya Kijiji, Kamati ya Mazingira na Maliasili, Wataalamu kutoka wilayani, kata na Community Resource Team – 2000

---

**hibitisho**

Muhuri wa Halmashauri ya kijiji cha Oloosoito-Maaloni umebandikwa kwenye sheria ndogo hizi kwa mujibu wa Mkutuno Mkuu wa Kijiji Uliofanyika tarehe 2[illegible] Novemba 2000, na umebandikwa mbele ya

MWENYEKITI WA KIJIJI
CHA LOSOI O-MAALONI
P. O. Box 1.

**Raphael Risie Long'ol**
**Mwenyekiti wa Halmashauri**
**ya kijiji cha Oloosoito-Malooni**

**Julius Lesinana Parmayo**
**Ofisa mtendaji wa Halmashauri**
**ya kijiji cha Oloosoito-Malooni**

OFISA MTENDAJI WA KIJIJI
LOSOITO/MAALON

**NAKUBALI:**

**Mhe : Simon Soinda**
**Mwenyekiti wa Halmashauri**
**wa wilaya ya Ngorongoro**

CHAIRMAN
NGORONGORO DISTRICT COUNCIL

**K.M.C. Tingirawanyuma**
**Mkuregenzi Mtendaji wa**
**Halmashauri wa wilaya ya**
**Ngorongoro**

HALMASHAURI YA WILAYA
YA NGORONGORO

5. **Kamati ya Viongozi na wataalamu juu ya Mgogoro wa Ardhi Tarafa ya Sale na Loliondo**

| Na | Jina | Kijiji/Kata | Cheo/Taaluma |
|---|---|---|---|
| | | **ILAIGWANAK** | |
| 1 | Simon Ndari | Malambo | Laigwanani |
| 2 | Samwel S. Leboo | Piyaya | Laigwanani |
| 3 | Lawrence N. Lyang'iri | Malambo | Laigwanani |
| 4 | John Kulinja | Malambo | Laigwanani |
| 5 | Ole Naing'isa | Ololosokwan | Laigwanani |
| | | **MADIWANI** | |
| 6 | Daniel K. Ngoitiko | Soitsambu | Diwani Kata ya Soitsambu |
| 7 | Rebeka Leshoko | Tarafa ya Loliondo | Diwani Vitimaalum - Tarafa ya Loliondo |
| 8 | Nairoshi Paulo | Tarafa ya Loliondo | Diwani Vitimaalum- Tarafa ya Loliondo |
| 9 | Mbeka Rago | Maaloni | Diwani Kata ya Maaloni |
| 10 | Njausi Ole Kursas | OLoipiri | Diwani Kata ya Oloipiri |
| 11 | Mathew E. Siloma | Arash | Diwani Kata ya Arash |
| 12 | Joel C. Resson | Malambo | Diwani Kata ya Malambo |
| 13 | Elias Ngorisa | Malambo | Diwani Mstaafu |
| 14 | Simon Nairiam | Piyaya | Diwani Kata ya Piyaya. |
| 15 | Moloiment Sange'u | Ololosokwan | Diwani Kata ya Ololosokwan |
| 16 | Kijoolu Kakeya | Tarafa ya Sale | Diwani Vitimaalum- Tarafa ya Sale |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 17 | Taleng'o Soyet | Tarafa ya Loliondo | Diwani Vitimaalum - Tarafa ya Loliondo |
| **WENYEVITI WA VIJIJI** | | | |
| 18 | Yohana Toroge | Kirtalo | Mwenyekiti wa Kijiji Kirtalo |
| 19 | Joseph Meing'atu | Olalaa | Mwenyekiti wa Kijiji Olalaa |
| 20 | Parmitoro Mbotony | Arash | Mwenyekiti wa Kijiji cha Arash |
| 21 | Issaya Munyere | Ormanie | Mwenyekiti wa Kijiji cha Ormanie |
| 22 | Moitiko Risando | Malambo | Mwenyekiti wa Kijiji Malambo |
| 23 | Samwel S. Leboo | Madukani | Mwenyekiti wa Kijiji Madukani |
| | | | |
| **VIONGOZI WA CCM** | | | |
| 24 | Ndirango Ole Senge | Loliono | Mwenyekiti wa CCM wilaya Ngorongoro |
| **WAWAKILISHI WA JAMII (WASIO VIONGOZI)** | | | |
| 25 | Mussa Toroge Timan | | Wawakilishi wa Jamii-Ololosokwan |
| 26 | Simel Elikana | | Mwakilishi wa Jamii - Arash |
| 27 | James Ndora | | Mwakilishi wa Jamii - Maaloni |
| 28 | Taiwap Ndalamia | | Mwakilishi wa Jamii Oloipiri |
| 29 | Rose Munga Naputi | | Mwakilishi wa jamii Malambo |
| 30 | Lemitoi Kakeya Olojiloji | | Mwakilishi wa Jamii Piyaya. |
| 31 | Babu L. Rotiken | | Mwakilishi wa Jamii Ololosokwan |
| 32 | Kooya Timan | | Mwakilishi wa Jamii |



| | | | |
|---|---|---|---|
| 33 | Noorkiropili Moko | | Mwakilishi wa Jamii |
| | **WATAALAMU WA JAMII** | | |
| 34 | Melau Alais | | Wakili na Mwanasheria wa Haki za Binadamu |
| 35 | Onesmo Kasale Olengurumwa | | Wakili na Mwanasheria wa Haki za Binadamu |
| 36 | Valentin Ngorisa. Olyang'iri | | Mtaalam wa Ardhi, Mazingira na Maliasili |
| 37 | Thomas Kairung | | Mtaalum wa Maliasili |
| 38 | Samwel Na'ngiria | | Maendeleo ya Jamii |
| 39 | Kondei Lawrence Makko | | Mwanasheria |
| 40 | Yannick Ndoinyo | | Mtaalam wa Uhifadhi na Maendeleo |
| 41 | Dr Kironyi Lekumok | | Mtaalamu wa Uchumi Kilimo na Biashara-Kilimo |
| 42 | Sinandei Makko | | Mtaalamu wa Mipango na Miradi |

